

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA NNE**

**Kikao cha Kumi na Tatu - Tarehe 19 Februari, 2004**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:**

Taarifa ya Kazi na Hesabu zilizokaguliwa za Bodi ya Usajili ya Wasanifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi kwa Mwaka wa Fedha Ullioishia tarehe 31 Desemba, 2002 (*The Annual Report on the Activities and Audited Accounts of the Architect and Quantity Surveyors Registration Board for the Financial year ended 31<sup>st</sup> December, 2002*).

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Shirika la Nyumba la Taifa kwa Kipindi cha Mwaka 2001/2002 (*The Annual Report and Accounts of the National Housing Corporation for the Financial year 2001/2002*).

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (*TAWIRI*) kwa Mwaka Ullioishia tarehe 30 Juni, 2002 (*The Annual Report and Audited Accounts of Tanzania Wildlife Research Institute for the year ended 30<sup>th</sup> June, 2002*).

Taarifa ya mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Shirika la Makumbusho kwa mwaka 2001/2002; pamoja na Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Shirika hilo kwa mwaka 2002/2003.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na.155

**Barabara ya Kati ya Uchindile na Mlimba**

**MHE. ABU T. KIWANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa ipo barabara iliyokuwa ikitumiwa na Wachina kusafirishia vifaa kwenye ujenzi wa Reli ya Uhuru kati ya Uchindile na Mlimba na kwa kuwa adha kwa wananchi ni nyingi ikiwa ni pamoja na kutoweza kupata huduma za jamii kama vile tiba wakati Reli ya Uhuru ikiwa imeharibika au ikiwa kwenye matengenezo na kutopata huduma ya Uongozi kutoka Wilayani Ifakara kwa kutoweza kufikika kwake na uongozi na Serikali na wageni wengine, ikizingatiwa kuwa barabara hiyo inahitaji ukarabati na madaraja machache tu ili kuchochea maendeleo yake kwenye Sekta ya Kilimo na Mifugo, hali ambayo Uchindile

ingeweza kabisa kuwa Switzerland ya Tanzania hususan kwenye Sekta ya Uzalishaji na bidhaa zote za mifugo:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kufufua barabara hiyo iliyokuwa inatumwa na Wachina kusafirishia vifaa kwenye ujenzi wa Reli ya Uhuru kati ya Uchindile na Mlimba ili kupunguza adha ya usafiri kati ya sehemu hizo mbili ambazo zinategemea reli tu kwa mawasiliano baina yao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mlimba - Uchindile ilikuwa ni njia ya mpito (*temporary-diversion access*) iliyotumika wakati wa matengenezo ya Reli ya Uhuru kwenye miaka ya 1975. Njia hii inayokadiriwa kuwa na urefu wa kilometra 100 hajjawahi kufanyiwa matengenezo makubwa toka Reli ya Uhuru ilipokamilika kwa sababu baada ya kukamilika kwa Reli ya Uhuru, njia kuu ya mawasiliano ya usafiri kati ya Mlimba na Uchindile imekuwa ni reli. Kutokana na kutokutumika kwa njia hii, miti mikubwa imeota kwenye eneo la njia na baadhi ya maeneo yamefunikwa na maporomoko yanayotoka kwenye milima na hasa ikizingatiwa kuwa barabara hii imepita kwenye mabonde na milima hadi Vijiji vya Kitete, Lugala na Uchindile. Njia hii kwa sasa haipitiki na ili kuhakikisha kwamba inapitika ni lazima ijengwe upya na sio kufanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua adha inayowapata wananchi wa Kata ya Uchindile kwa kukosa huduma ya usafiri wa barabara na badala yake kutegemea huduma itolewayo na Reli ya TAZARA tu. Pamoja na kutambua hilo, Serikali kwa wakati huu haina uwezo wa kujenga barabara hii. Gharama ya kujenga upya barabara hii inakadiriwa kuwa shilingi 1,500,000,000.

Aidha, upembusi yakinifu uliofanywa kupitia Mpango wa Barabara wa Huduma kwa Barabara za Wilaya (*District Roads Support Programme*) unaofadhiliwa na Serikali ya Usisi umeonyesha kuwa kwa sasa barabara hii haina umuhimu wa kwanza katika kufanyiwa matengenezo. Matokeo haya ya upembusi yakinifu hayaondoi hata hivyo nia ya Serikali ya kuwaondolewa watu wake adha mbalimbali wanazozipata. Serikali inaendelea na juhudi za kuona uwezekano wa kujenga barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Serikali inaendelea kufanya juhudhi mbalimbali kutatua tatizo hili, namwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa maeneo inapopita barabara hii kwanza, wawe wavumilivu na kuendelea kutumia huduma za usafiri zitolewazo na Reli ya TAZARA.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, gharama ya bilioni moja tunajua ni kubwa lakini huduma kwa wananchi pia ni kubwa na kama nilivyosema kwenye swal la msingi bila kupata usafiri wa reli na reli ikiharibika hawa watu hawana mawasiliano. Kwa hiyo, *alternative option* naomba Serikali ifikirie.

Je, Wizara ya TAMISEMI haifikirii kwa kutumia *Road Fund* ambayo sasa hivi ina bakaa kama ya milioni 36 ikatumia kwanza kufanya uchunguzi mwingine wa kushirikisha wananchi ili kupunguza hiyo gharama? (*Makofsi*)

Pili, kwa kuwa gharama ni kubwa, Waziri haoni kuwa pia angeshirikisha Wizara ya Ujenzi ili barabara ya kuhudumia watu kati ya Mlimba na Uchindile ikamilike? Kama kuna uwezekano wa kupata wafadhili basi kwa kutumia bakaa niliyosema hapo awali, taratibu zifanyike tutathmini, naamini kwa kutumia nguvu kazi za wananchi gharama itakuwa chini zaidi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, nimeeleza hapa katika maelezo ya awali kwamba kwa vyovoyote vile ujenzi wa barabara hii katika mazingira ya kiuchumi tuliyonayo sasa haiwezekani.

Gharama ni kubwa na hata kama tutajaribu kutumia nguvu za wananchi, si jambo jepesi kwa kilometra 100 tena ambazo barabara haipo kabisa. Itakuwa kwa kweli ni kuwadanganya wananchi kwa kudhani kwamba tunaweza tukasaidiana kutatua tatizo kubwa kama hilo na ndiyo maana nimemsihi kwamba kwa sasa kwa sababu Reli ya *TAZARA* ipo na inafanya kazi, tutumie njia hiyo ya usafiri kuwaondolea kero wananchi hawa. Lakini endapo itatokea dharura ya namna yoyote ile itakayosababisha ugumu wa wananchi hawa kusafiri katika eneo hilo, mambo ambayo yanatokea hata katika Reli ya Kati, Serikali itaingilia kati kuona ni nini ifanye.

Pili, suala la kuishirikisha Wizara ya Ujenzi katika ujenzi wa barabara hii, nalo haliwezekani kwa sababu tunazungumza fedha ile ile. Lakini kubwa zaidi ni kwamba upo utaratibu wa kutambua barabara ambazo zinahudumiwa na Wizara ya Ujenzi na barabara ambazo zinapata *Road Fund* kuititia TAMISEMI. Barabara hii sio moja ya njia ambazo inapita kuititia Wizara ya Ujenzi.

Na.156

#### **Watendaji Kata Kufanya kazi ya Ulinzi na Amani**

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika nchi yetu tunaaamini kwamba amani, utulivu na utawala wa sheria viko mikononi mwa walinzi wa amani hasa Watendaji wa Kata (*WEO*):-

- (a) Je, ni sheria ipi inayowapa madaraka Watendaji hao kufanya kazi ya ulinzi na amani na majukumu yao na mipaka ya mamlaka yao yamewekwa na sheria ipi?
- (b) Je, katika utendaji wa kazi, walinzi hao wa amani wanawajibika kwa nani na nani anadhibiti matumizi ya mamlaka yao?
- (c) Je, Watendaji hao wanatakiwa kuwa na ujuzi gani ili wafanye vizuri kazi hiyo muhimu ambayo ndiyo kioo cha utawala bora na utawala wa sheria na mara ya mwisho Watendaji hao wamepewa Semina au Warsha lini ili watimize vizuri wajibu wao?

#### **NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Willbrod Peter Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, madaraka ya Maafisa Watendaji wa Kata ya kufanya kazi ya ulinzi wa amani yametolewa chini ya kifungu cha 51(2) cha Sheria ya Mahakama za Mahakimu ya mwaka 1963, Sura ya 537 yaani *The Magistrate's Court Act. 1963 - Cap. 537* kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Mahakama za Mahakimu Na. 2 ya mwaka 1984. Chini ya Sheria hiyo Waziri mwenye dhamana amepewa madaraka ya kuteua Walinzi wa Amani ambao watafanya kazi hiyo katika maeneo yao ya kazi.

Kutokana na madaraka hayo tarehe 12 Septemba, 1975 Waziri Mkuu kuititia Tangazo la Serikali Na.189 (*The Magistrates Courts (Appointment of Justices of the Peace) Notice (No.2) 1975* aliwateua Makatibu Kata ambao kwa sasa ni Maafisa Watendaji wa Kata kuwa Walinzi wa Amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu yao na mipaka ya mamlaka yao yanatawaliwa na sheria mbalimbali zikiwemo, Sheria hiyo ya Mahakimu niliyoitaja kama ilivyorekebishwa, Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Na.7 ya mwaka 1982 (Kifungu cha 177(1), Sheria ya Serikali za Mitaa

(Mamlaka za Miji) Na.8 ya mwaka 1982 (Kifungu cha 91(1), Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Jinai Na.9 ya mwaka 1982 yaani *Criminal Procedure Act No.9 of the year 1985* na hasa kifungu cha 13(1)(a) na (b).

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa majukumu yao ya ulinzi wa amani, Watendaji wa Kata wanawajibika kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na Wilaya zilizomo katika maeneo yao ya kazi. Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tarafa na Wakurugenzi wa Halmashauri zetu wanao pia wajibu wa jumla wa kuhakikisha Watendaji wa Kata wanatekeleza ipasavyo majukumu yao yakiwemo ya ulinzi wa amani.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba Watendaji wa Kata wanakuwa na sifa zinazostahili, Serikali ilitoa Waraka wa Tume ya Utumishi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 1992 ambao unafafanua muundo wa utumishi wa Watendaji hawa pamoja na sifa zao.

Kwa mujibu wa Waraka huo, Watendaji hao, Afisa Mtendaji anatakiwa awe na elimu ya kiwango cha Stashahada ya Sheria kutoka Chuo Kikuu au Chuo kinachotambuliwa na Serikali au sifa sawa na hizo au Shahada ya kwanza katika Sayansi ya Jamii au Stashahada ya Juu katika Utawala yaani *Advanced Diploma in Public Administration* au Stashahada ya juu katika Utawala wa Serikali za Mitaa (*advanced Diploma in Local Government Administration*) kulingana na Daraja la Afisa huyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeandaa programu ya mafunzo ya miaka mitano ya kuboresha utawala wa utendaji kazi wa Maafisa Watendaji. Mafunzo haya ni ya wiki mbili mbili, yanatolewa katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo na katika Kanda na yalizinduliwa rasmi tarehe 22 Machi, 2002. Mafunzo haya yanaendeshwa kutokana na msaada wa Shirika la Maendeleo la Japan na Serikali ya Tanzania. Hadi sasa jumla ya Maafisa Watendaji wa Kata 2,303 kati ya Watendaji 2,537 wamepatiwa mafunzo kutoka Mikoa yote ya Tanzania Bara.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza na ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba mamlaka na madaraka yao yanatawaliwa na sheria nyingi mbalimbali na kwa kuwa sifa zilizotajwa za Makatibu Kata zikiwepo hasa za Stashahada na Shahada na kwamba hizi hazipo. Je, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atakiri kwamba kazi hizi ni vigumu kutekelezeka na hawa walioko kutokana na ugumu wa kazi yenye na kwa kuwa inahusu hasa haki za binadamu? (*Makofit*)

Pili, kwa kuwa masuala yaliyokuwa yanashughulikiwa na hawa ndio msingi hasa wa utawala bora na wa sheria katika nchi yetu na kwa kuwa sehemu nyingi hawa ndio muhimu kwa kweli kwa kuwa sio rahisi kuwa na Mahakimu kila Kata, je, sasa sio wakati muhimu wa Serikali kuanzisha utaratibu maalum wa hawa kutoa taarifa zao kwa maandishi angalau kwa Mahakimu na kwa Vyombo vyta Sheria vinavyohusika ili hukumu na hatua wanazochukua za ulinzi wa amani ziweze kudhibitiwa vizuri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Watendaji tulionao hivi sasa, sehemu kubwa kabisa hawana sifa hizo tulizotajta. Ni kweli vile vile kwamba kutokana na ukweli huo inawezekana kabisa majukumu yanayotendwa nao ndio maana hayaendi kwa kiwango ambacho kinaridhisha kwa maana ya kusimamia shughuli za maendeleo na ulinzi wa amani. Lakini nataka tu kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba hiyo ndiyo hali halisi tuliyonayo sasa kwamba kuwapata watu wenye sifa hizo sio rahisi, lakini tunajitahidi kuona ni namna gani tunaweza kuboresha mazingira ya hao waliopo ili waweze kutenda wajibu wao vizuri na ndio maana nimezungumzia suala la *training* ambayo inaendelea hivi sasa.

Pili, suala la Watendaji kutoa taarifa kwa Mahakimu, tunaloweza kusema hapa ni kwamba katika hali ya kawaida, kazi ya ulinzi wa amani inatakiwa kuwa ni ile inayohusiana na ukamataji wa wananchi, uwekaji wa wananchi katika selo na uwasilishaji wa wananchi hawa katika Vituo ama vya Polisi au Mahakimu kwa ajili ya kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Kwa hiyo, suala la kuwasilisha taarifa kwao si suala tena la kuagizwa lakini wanapaswa kuwa wanafanya hivyo na hasa pale Mahakimu wanapo-*demand* kwamba wanataka kujua kazi zao zinaendeshwa namna gani.

Na.157

### **Uimarishaji wa Michezo Mbalimbali**

#### **MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa mpaka sasa michezo kama vile mpira wa miguu, mikono, meza, riadha na kadhalika ni biashara nzuri na mfano mzuri ni ule wa nchi ya Brazil ambayo ina wachezaji zaidi ya 600 wanaocheza nchi za nje kwa malipo na hivyo kuiletea sifa nchi yao na pia kuleta fedha za kigeni, vile vile nchi kama Cameroon na Nigeria, Ghana na kadhalika wanao wachezaji wanaoshiriki michezo huko Ulaya na kwingineko na kujipatia kipato kizuri na kukuza uchumi wa nchi zao na kwa kuwa Serikali za nchi hizo hutenga fedha kwa ajili ya kuanzisha Shule na Vyuo vya Michezo ili kukuza na kuendeleza vipaji vya michezo kwa watoto kuanzia umri mdogo kwa kuwapatia mafunzo yanayohitajika kwa ajili ya kupata wachezaji wazuri:-

(a) Je, kwa nini Serikali yetu isianzishe utaratibu kama huo kwa faida ya Taifa letu na kwamba kwa kuwa eneo la michezo linaongeza uchumi wa nchi na ajira kwa vijana wetu kama likiendelezwa ipasavyo. Je, Serikali itakuwa tayari kubadilisha sera za michezo ziwe nzuri ili kupata viongozi wazuri kwenye vilabu vyetu kwa lengo la kuendeleza michezo hapa nchini?

(b) Kwa kuwa wachezaji wastaa fu kama vile Filbert Bayi, Shahanga na kadhalika wanavyo vipaji ambavyo vilijitokeza wakati wakishiriki michezo tangu wakiwa Shule za Msingi, Kati na Sekondari, je, Serikali inasemaje juu ya kurudisha michezo Shuleni kama vile UMITASHUMTA na UMISETA?

(c) Kwa kuwa Tanzania ni Mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mwanachama wa SADC na mionganii mwa nchi za Maziwa Makuu Matatu, je, Serikali itafanya jitihada gani ili tuweze kushiriki Kombe la Mataifa huru ya Afrika, Kombe la Dunia na kadhalika kama wenzetu wa Afrika ya Kusini, Kenya, Rwanda na kadhalika wanavyoshiriki?

#### **NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Sera ya Maendeleo ya Michezo ni nzuri na inajitosheleza katika masuala yote aliyoyazungumzia Mheshimiwa Mbunge. Kwa mfano, sera inaainisha namna ya kupata wachezaji bora wakiwa wameandalila tangu utotoni. Aidha, sera imeruhusu kuwepo kwa michezo ya kulipwa ikiwa ni njia mojawapo ya kukuza viwango vya michezo na kujipatia ajira. Hata hivyo, sera ikiwa ni suala la elimumwendo, itakuwa inahuishwa kila ikitokea umuhimu wa kufanya hivyo.

(b) Serikali haijafuta michezo katika Shule za Msingi na Sekondari ila imesitisha mashidano ya UMITASHUMTA na UMISETA.

(c) Tanzania imekuwa ikishiriki katika Mashindano ya Mataifa Huru ya Afrika, Kombe la Dunia kwa Mpira wa Miguu, Olimpiki, Jumuiya ya Madola na kadhalika. Upo ushahidi wa kutosha kuwa kwa baadhi ya michezo tumefanya vizuri. Hii ni kama ngumi, mpira wa mikono, riadha na mpira wa kikapu. Serikali inajenga eneo changamani la michezo ambalo litakuwa mahali pa kuzalisha na kuendeleza wachezaji. (*Makofit*)

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuna baadhi ya michezo tunayofanya vizuri, lakini ukweli ni kwamba mchezo wa mpira wa miguu bado hatujafanya vizuri kutokana na vurugu zinazotokea kwenye Chama cha Mpresa Tanzania na Jumamosi hii kuna Kikao ambacho kimeitishwa na *FIFA* kuhusu michezo. Je, Serikali inasemaje juu ya Kikao hiki ambacho kinaitishwa kukiwa na Vyama viwili vinavyogongana? (*Makofî*)

Pili, kwa sababu mpira wa miguu ni uchumi, ajira na siasa na kwa sababu *FIFA* ni chombo cha Kimataifa ndio kinachosimamia hii michezo duniani kote na mpaka sasa inaonesha Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo haijafikia muafaka mzuri na *FIFA*, je, Wizara yetu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, inashiriki vipi katika kutatua jambo hili? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI , MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mkutano wa tarehe 21 Februari, 2004 ulioitishwa na *FIFA*, Serikali imeshindwa kutoa tamko muda wote kwa sababu kama tunavyofahamu, *FAT* iko Mahakamani hivi sasa. Kwa sababu iko Mahakamani, imeshktakiwa, sisi kuzungumza jambo lolote la *FAT* tutakuwa tunaingilia kati mamlaka na uhuru wa Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bwana Ndolanga imesambaza barua kwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu wakionesa *agenda* tatu za Mkutano huo. Moja, kuondoa Kamati ya sasa inayoongozwa na Mwenyekiti Yahaya Mhata, *agenda* ya pili, kuirudisha Kamati yake yeze Ndolanga na *agenda* ya tatu, kuandaa Kamati ya Katiba. Lakini barua ambayo *FAT* ya sasa wameipata kutoka *FIFA*, hiyo hiyo aliyoundikiwa Bwana Ndolanga, haisemi hivyo. Yenyewe inaelezea kwamba Mkutano huo utaendeshwa na Dr. Joseph Mifsud wa *FIFA* na kwamba wanakuja kuunda Kamati ambayo itatuondoa katika kipindi hiki cha mgogoro. Kwa hiyo, mnawenza mkaona matatizo tuliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo mimi nisingependa sana kuilaumu *FIFA* kwa sababu *FIFA* anaingia tu hapa Tanzania inapotokea mtu kuita *FIFA*. Sasa tusizungumzie matokeo, tuzungumzie chanzo. Huyu anayekwenda kumwita *FIFA* na bado hasemwi inasemwa *FIFA*, hayo ndiyo matatizo. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maendeleo ya soka, kwa kweli hatuoni sababu kwamba umefikia wakati sasa wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuingilia suala hili. Kama nilivyosema, tatizo sio la *FIFA*, tatizo ni la Watanzania wachache wenye uroho na uchoyo wa fedha ambao ndio kila saa wanakwenda kuwaita *FIFA*.

Lakini mimi nasema muda sio mrefu watu wa Tanzania wameshaanza kuwafahamu ni wangapi na kwa majina yao, bila shaka mwisho wao umefika. Hata hivyo ukuzaji wa soka hautegemei tu sera. Mfano aliota Mheshimiwa Mbunge wa Cameroon, Cameroon wana *Soccer Academy 60* na mmoja wa Mbunge mwenzetu kule ameanzisha *Academy* yake inaitwa *Mount Cameroon Soccer Academy*, kuna *Botafogo Soccer Academy*, *Njalakwani Soccer Academy*, *Haji Breweries* na kadhalika. Kwa hiyo, ni watu wote, Serikali, wadau pamoja na watu binafsi. (*Kicheko/Makofî*)

Na.158

### **Kituo cha Polisi cha Madaba**

**MHE. HAROUB SAID MASOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa mnamo tarehe 16 Julai, 1996 Ndugu Vicent Nkalawe, Kiongozi wa Mbio za Mwenge mwaka huo aliweka Jiwe la Msingi kwenye jengo la Kituo cha Polisi cha Madaba katika Jimbo la Kinondoni kilichojengwa kwa nguvu za wananchi; na kwa kuwa Kituo hicho bado hakijakamilika na hivyo kimekuwa kama maficho ya vibaka:-

- (a) Je, Serikali haioni kwamba kutokamilisha ujenzi huo kunawavunja moyo wananchi waliojitolea nguvu zao?

- (b) Je, Serikali haioni kuwa kitendo cha kuacha kumalizia ujenzi kama huo kinadhoofisha ari ya Mbio za Mwenge katika kuhamasisha maendeleo?
- (c) Kama hali ya Kituo hicho bado iko hivyo, je, Serikali haioni kwamba iko haja ya kuikamilisha kazi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mnamo mwezi Juni, 1994 na sio Juni, 1996 kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema, Kiongozi wa Mbio za Mwenge aliweka Jiwe la Msingi jengo lililokusudiwa kutumika kama Kituo Kidogo cha Polisi yaani *Police Post* katika Mtaa wa Madaba, Kata ya Mzimuni, Manispaa ya Kinondoni.

Ujenzi wa jengo hili ulianzishwa na wananchi wenyewe kwa njia ya kujitolea chini ya usimamizi wa Bwana Bashwan. Hata hivyo, mwaka huo huo mwezi Desemba, msimamizi Mkuu wa Ujenzi yaani Bwana Bashwan alifariki na ujenzi wa jengo hilo ukasimama kwa muda mrefu sana hadi hivi karibuni yaani mwezi Desemba, 2003, ambapo wananchi wa eneo hilo waliunda Kamati mpya ya Ujenzi ili kufufua ujenzi wa jengo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inawapongeza wananchi wa Mtaa wa Madaba kwa kuchukua hatua ya kufufua mradi huu na katika kuwashamasisha na kuwaunga mkono wananchi hao, Serikali kuitia Manispaa ya Kinondoni, hivi karibuni imechangia shilingi milioni moja kwa ajili ya mradi huu.

Aidha, tunawaomba viongozi na wananchi wa Mtaa wa Madaba na wa Kata nzima ya Mzimuni na hasa wafanyabiashara, washirikiane kukamilisha jengo hilo na mara litakapokamilika Serikali inaahidi kuwasogezza karibu huduma ya ulinzi kwa kupeleka Askari Polisi na vitendea kazi husika katika Kituo hicho.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza namtoa wasiwasi Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kinondoni asidhanie nanyatia Jimbo hilo. Sasa nina swali moja la nyongeza. (*Kicheko/Makofsi*)

Kama alivyozungumza mwenyewe Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba jengo hilo lilianzishwa tangu mwaka 1994 na sasa ni takriban miaka tisa, haoni kama hali kama hii itaachiwa, majengo ambayo yanatumia nembo ya Wizara ya Mambo ya Ndani yatakuwepo mengi sana na hayatamalizwa?

Kwa hiyo, nini ushauri wake kwa sasa na yeye kwa upande wake kama ikiwa Manispaa imechangia, Wizara ya Mambo ya Ndani haioni kama ipo haja na wao wakachangia kitu angalau likamalizika mwaka huu? (*Makofsi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme kwamba mradi huu uliibuliwa na wananchi wenyewe wa Mtaa wa Madaba na wakaanza kuutekeleza na ndio utaratibu unaotumika kwa nchi nzima.

Katika kutekeleza mradi huu walifika mahali wakakwama lakini baadaye wao wenyewe wakagundua dosari hii na wameisahihisha na mpaka hatua hii jengo hili bado halina nembo ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Jengo liko chini ya wananchi mpaka hapo litakapokamilika ndipo watatukabidhi Wizara ya Mambo ya Ndani ili tutumike kama Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tunatazama juhudhi mpya na kasi mpya waliyoanza nayo baada ya kuunda Kamati mpya. Kwa hiyo, mchango wetu sisi kama Wizara ya Mambo ya Ndani utategemea juhudhi watakayoionesha wananchi wa Madaba hasa baada ya kupata ari hii mpya.

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri kwa swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud.

Mimi naomba kutoa shukrani zangu kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kutusaidia pale ambapo tumejenga Vituo vya Polisi, wametusaidia kutupatia mabati na vitu vingi tu vya kuendeleza Vituo vyetu vya Polisi...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge ongeza sauti.

**MHE. PETER KABISA:** Pamoja na kwamba Mheshimiwa Mbunge mwenyewe amekuwa akichangia mara kwa mara kwenye vituo hivi vyote, sasa nina swalii moja dogo la nyongeza. Bahati mbaya sana tunapojenga vituo hivi tunaambiwa kwamba vikishajengwa wale wafanyakazi wa vituo hivyo kwa maana ya Ofisa wa Polisi, sisi wananchi tuwapatie sehemu ya kuishi yaani kwa kulipia kodi ya nyumba zao. Naomba ufanuzi wa hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa tunapenda kupokea shukrani alizozitoa, ni wajibu wetu kama Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kusaidia kuunga mkono juhudzi za wananchi na ndiyo Sera ya Chama Cha Mapinduzi, ndivyo inavyosema kwamba pale ambapo wananchi wanaonyesha juhudzi basi Serikali itafika kuwaunga mkono.

Sasa kuhusu suala la wananchi kutakiwa kuandaa maeneo ya polisi kuishi, utaratibu huu si tu kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ndivyo inavyofanyika kwa Idara na Wizara mbalimbali, tunapojenga shule ya msingi tunakumbuka vile vile kujenga nyumba za walimu, tunapojenga zahanati, vile vile tunawajibika kujenga na nyumba za waganga.

Kwa hiyo na hili nalo la vituo vya Polisi ni hivyo hivyo, tunapojenga Kituo cha Polisi mahali tukumbuke vile vile kujenga na nyumba ambayo hao polisi watakapooshumia Kituo hicho watakapoishi. Kwa hiyo, ni utaratibu ambao kwa kweli unatumika katika Wizara mbalimbali na ni sahihi. Sasa kuhusu kuwalipia kodi askari polisi hilo halimo katika utaratibu. Tunachosisitiza ni kuandaa nyumba ambazo wataishi polisi.

Na. 159

#### **Ofisi ya Mkuu wa Polisi - Ludewa**

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa zipo jitihada za Serikali za kujenga Ofisi na nyumba za kuishi askari polisi katika nchi nzima:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaanza kujenga Ofisi ya Mkuu wa Polisi wa Wilaya mjini Ludewa na nyumba za kuishi askari Polisi kwenye vituo vya Ludewa na Mji mdogo wa Malangali?
- (b) Je, kuna mkakati gani wa kuokoa nyumba za kuishi askari polisi katika Kituo cha Polisi cha Manda zilizojengwa miaka thelathini iliyopita na hazijafanyiwa ukarabati?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mbunge wa Ludewa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inao utaratibu wa kujenga Ofisi za Polisi za Wilaya na nyumba za kuishi askari zenyé hadhi nchi nzima. Ujenzi wa Ofisi na nyumba za askari unafanywa kwa awamu kwa kadri Bajeti ya Serikali inavyoboreka kila mwaka. Hata hivyo, pale ambapo wananchi wanachangia kwa hali na mali, ujenzi huweza kukamilika kwa haraka zaidi.

Katika jitihada za kujenga nyumba na Ofisi za Polisi zenyenye hadhi hadi sasa Serikali imefanikiwa kujenga Ofisi na nyumba za askari zenyenye hadhi katika Wilaya 55, kati ya Wilaya 118 zilizopo nchini. Wilaya 66 zilizobaki ikiwa ni pamoja na Ludewa hazina majengo zenyenye hadhi.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inatambua kuwa Wilaya ya Ludewa ipo katika kundi la Wilaya 63 ambazo bado hapajajengwa majengo na Ofisi na nyumba za kuishi askari zenyenye hadhi. Kazi hii itafanyika kadri uchumi wa nchi unavyoruhusu.

Napenda kuchukua nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge ajaribu kuwahamasisha wananchi wake kutazama uwezekano wa kuanza kwa kile watakachokiweza wakati wakisubiri uwezo wa Serikali.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafahamu kuwa nyumba nyingi za kuishi askari sehemu mbalimbali nchini ni chakavu ikiwa ni pamoja na nyumba katika kituo cha Polisi cha Manda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua hivyo Serikali inaendelea kukarabati nyumba hizo kwa awamu kwa kadri Bajeti ya Serikali inavyoruhusu. Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Manda wawe na subira wakati Serikali inatafuta fedha za kukarabati nyumba za askari katika vituo mbalimbali pamoja na Kituo cha Manda, Wilayani Ludewa.

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini kwa kuwa nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumzia Sera ya watu kujitolea kwanza kujenga majengo, kwa kuwa eneo la Ludewa Mjini Makao Makuu ya Polisi wameshaanza kujitolea, je, ana kauli gani kwamba ni katika Bajeti hii atawea kuwaunga mkono?

Swali la pili, ni kwamba majengo ya Kituo cha Polisi Manda yalijengwa miaka 30 iliyopita na kwa kuwa uharibifu umekuwa mkubwa, na kwa kuwa sasa hivi Serikali inajaribu kuinua uchumi katika maeneo ya *Mbamba Bay* kutohana na barabara ile ya kutoka Mtwara, je, haoni sasa kuna umuhimu wa kukarabati majengo hayo ili kuweza kumudu uchumi unaokuja? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwapongeze wananchi wa Ludewa Mjini kwamba wameanza kujitolea kujenga Kituo cha Polisi, tunawapongeza sana na tutawasiliana nao tuone wamefikia hatua gani katika ujenzi huo ili na sisi tuone ni namna gani tutawaunga mkono. Kwa hiyo, fikisha hizo taarifa.

Pili, kuhusu kituo cha Manda, kama nilivyojibu awali kwamba vituo ambavyo ni chakavu na ninyi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwa kweli ni vingi sana na nchi nzima. Kwa hiyo, uwezo wa kuvikarabati vyote kwa mara moja hatunao, kwa mfano mwaka 2003/2004 katika Bajeti ya mwaka huu shilingi milioni 900 tu kwa kazi hiyo kwa nchi nzima. Kwa hiyo, napenda tu kumwomba tena Mheshimiwa Mbunge awe na subira, kwa hakika tutafika mpaka ukarabati pale Manda lakini ni lini sasa itategemea na hali ya Bajeti. (*Makofî*)

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona na kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa Wilaya ya Mwanga ina Kituo kimoja tu cha Polisi na ujambazi umeongezeka sana na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alikubali kuwasaidia wananchi wa eneo la Nyumba ya Mungu kukamilisha kituo cha polisi pamoja na vituo vingine vya polisi katika Kata ya Msangeni na Kata ya Lembeni, je, Serikali lini sasa itapeleka msaada huo kwa wananchi ambao wameshakamilisha upande wao wa kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, huyo aliyeuliza swalii alikuwa Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika Jimbo la Mwanga tuna kituo kimoja lakini ni moja ya vituo ambavyo ni vituo vizuri sana chenye askari wa kutosha na vitendea kazi vya kutosha.

Sasa kuhusu ujenzi wa vituo alivyovitaja kule Nyumba ya Mungu, Msangeni, Lembeni kama tuliviyokwisha wasiliana naye kwa njia ya barua kwamba Wizara kimsingi iko tayari kusaidiana nao, tukawaomba tu kwamba wawe na subira wakati uwezo unatafutwa. Kwa hiyo, naomba tu aendelee kuvuta subira, kwa sababu mahitaji ni mengi na raslimali ni chache, lakini kwa hakika kwamba kimsingi tunakubaliana kwamba tutasaidiana naye.

Na. 160

### **Shule ya Sekondari ya Murigha**

**MHE. LAZARO S. NYALANDU** aliuliza:-

Kwa kuwa Shule ya Sekondari ya Murigha iliyoko Wilaya ya Singida Vijijini ilijengwa na Wamisionari kwa zaidi ya shilingi 900,000,000/=; na kwa kuwa shule hiyo ilijengwa katika kijiji cha Msange.

- (a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuipatia shule hiyo umeme ili kuhamasisha elimu na kuchochlea maendeleo katika vijiji vya Msange, Ghata, Maghojoa, Mdilu na Jangwa?
- (b) Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kupeleka umeme katika shule hiyo?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Murigha iliyoko Wilaya ya Singida Vijijini kilometra 42 kutoka Singida Mjini, ilijengwa mwaka 1999 na Wamisionari wa Kanisa la Katoliki na inamilikiwa na Masista wa Maryknoll wa Kanisa hilo. Pamoja na umuhimu wa kuipatia shule hii umeme, mwenye wajibu huo ni mmiliki wa shule yaani mwenye shule hiyo.

Aidha, Serikali hajjawahi kuahidi kuipatia shule hiyo umeme. Pamoja na nia njema ya wamisionari ya kujenga shule hiyo ya Sekondari kwa gharama kubwa, ni vizuri sasa watekeleze mpango wao walioureka kwenye *Master Plan* yao wakati wa ujenzi wa kuipatia shule hiyo umeme wa nguvu za jua (*Solar Power*). Kwa mujibu wa mpango wa ujenzi wa hule hiyo, umeme wa aina hii ulionekana kuwa unagharama nafuu zaidi kuliko kuvuta umeme kutoka gridi ya Taifa ambayo iko kilometra 24 kutoka shulenii hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya waendelee kuwashawishi wamiliki wa shule hiyo ili waweke umeme ambaotu utahamasisha na kuchochlea maendeleo katika vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa uwezo wa shule hii ya sekondari ya Murigha kuweza kujiwekea umeme yenye ni mdogo na kwa kuwa kazi ya kuweka umeme katika maeneo haya ni kazi ya Serikali, wajibu ambaotu Waziri hawezi akaukwepa kama Serikali. Je, Serikali inasema nini kuhusu kuweka umeme Sekondari hii ya Murigha ili wananchi wa vijiji vyote nilivyovitaja vya Msange, Gata, Maghojoa, Mdilu na Jangwa wafaidi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swal la pili, kwa sababu elimu kama tunavyoifahamu sasa hivi Mheshimiwa Naibu Spika, inaendana sambamba na wanafunzi waweze kushiba ndiyo waende shulenii na kwa kuwa katika maeneo ambayo tumeyataja na maeneo yote ya Singida Kaskazini wananchi wana njaa ambayo haina mfano na siwezi kuielezea hapa Bungeni.

Je, Serikali haiwezi ikachukua ushauri wangu wa kuwalisha wanafunzi wa shule za Msingi chakula cha mchana, shule zote za Singida Kaskazini na shule zote za Tanzania? (*Makofî*)

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza pamoja na kwamba inawezekana kabisa uwezo wa shule hiyo ni mdogo kwa kujiwekeea umeme, lakini kama nilivyoeleza katika jibu la msingi kuna mgawanyo wa majukumu na mtu anapoanzisha shule huleta mipango yake Wizarani na hueleza katika mpango ule uwezo wake na ulipoletwa Wizarani mpango wa ujenzi wa shule hiyo walionyesha ndani ya *Master Plan* kwamba wataweka umeme wa *Solar Energy* iko katika *Master Plan* kwamba watafanya wao wenyewe. Sasa leo haiwezekani hilo likabadihika ghafla ukawa ni wajibu wa Serikali. Kwa hiyo, napenda nirudie tena kusema kwamba huo ni wajibu wa mwenye shule.

Swali la pili, kwamba kuna hali ya njaa katika eneo hilo, Serikali ingefikiria kutoa mlo kwa wanafunzi katika shule za msingi na tena iwe katika nchi nzima. Napenda kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna mgawanyo wa wajibu katika kugharimia elimu ya msingi Serikali inalipa mishahara ya walimu, inalipa gharama zote za shule, lakini na mzazi naye amebakiziwa wajibu wa kumvisha mtoto, kumlisha, kumpa malazi na kama kuna hali ya upungufu wa chakula basi suala hili la njaa lishughulikiwe kwa taratibu tulizonazo za kushughulikia tatizo la njaa. Haiwezi ikageuka mara moja ikawa ni Wizara ya Elimu na Utamaduni ndiyo ianze kulisha chakula. (*Makofî*)

Napenda nikumbushe kwamba jana au juzi tumepitisha *Supplementary Budget* na tuliweka fedha kwa utaratibu huo. Hatuwezi tukakurupua jipya nje ya ile *Supplementary Budget* tuliyopitisha.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa elimu sasa hivi inatiliwa mkazo na elimu ya sasa hivi haikamiliki bila mwanafunzi kujifunza kompyuta na kwa kuwa kompyuta zinahitaji umeme na kwa kuwa katika jimbo langu tunakusudia kujenga shule 13 na bahati mbaya hakuna umeme.

Je, Serikali ili watoto hao waweze kusoma vizuri ina mpango gani kupeleka umeme katika Jimbo la Busanda? Ahsante sana. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hili ni swali jipya kabisa la umeme Busanda. Lakini nadhani Mheshimiwa Waziri ana jibu.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kusema hivyo hivyo kwamba swali hili ni jipya mno na katika swali linalofuata nitakuwa na jibu linalohusu suala la umeme katika shule.

**NAIBU SPIKA:** Sasa twende kwenye hilo swali linifuata basi.

Na. 161

#### **Uanzishwaji wa Somo la Kompyuta Ngazi ya Msingi hadi Vyuoni**

**MHE. MARGARETH A. MKANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa matumizi ya teknolojia za mawasiliano kama Kompyuta hutumika katika kufundishia na kujifunzia na hivyo kurahisisha kazi kwa walimu na wanafunzi kwani huwezesha wanafunzi wengi kujifunza kwa wakati mmoja:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuanzisha somo la Kompyuta kikamilifu katika shule za msingi, sekondari hadi vyuoni?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kuchelewa kufundisha somo la Kompyuta katika shule za Serikali ambako ndiko wanafunzi wengi wasiomudu gharama za elimu kwingineko kuchelewa kufaidika na utandawazi ambao umeifanya dunia kuwa kijiji kutokana na matumizi ya mtandao wa mawasiliano katika kupata taarifa mbalimbali za dunia hivyo kuchelewesha jitihada za kujikwamua kutoka katika umaskini uliopo nchini?

#### **WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa namaanisha swali linalofuata linahusu kompyuta, nikasema umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwalimu Margareth Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kuwa matumizi ya teknolojia ya mawasiliano kwa Kompyuta yanaweza kurahisisha sana ufundishaji na kujifunza maarifa na stadi mbalimbali katika shule na katika vyuo. Kwa hapa nchini teknolojia hii imeanza kutumika katika taasisi mbalimbali hasa za ngazi za elimu ya juu na katika baadhi ya shule za awali, shule za msingi, shule za sekondari na vyuo vya ualimu kutokana na misaada isiyo ya kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haicheleweshi kufundisha somo la kompyuta katika shule za Serikali kwa makusudi. Kikwazo ni gharama na maandalizi yanayotakiwa yafanywe vizuri kabla ya kuanza kufundisha somo hilo.

Hata hivyo Wizara yangu kwa kuititia Taasisi ya Elimu Tanzania (*TET*) imeshaandaa Mitaala ya kufundishia somo la kompyuta kwa kutumia teknolojia ya mawasiliano ya kompyuta kwa ajili ya shule za sekondari na vyuo na inatumika sasa katika shule na vyuo ambavyo vinatoa mafunzo hayo na shule hizo zinaweza zikafanya mitihani ya Kitaifa.

Aidha, Wizara yangu imeamua kuanza kwanza na kufundisha somo la kompyuta katika vyuo vyote vya ualimu. Uandaaji wa mafunzo hayo utakamilika hivi karibuni ili kuwezesha utekelezaji uanze katika *intake* ijayo ya vyuo vya elimu ya ualimu (*TTC*) kwa lengo la kila anayefuzu katika vyuo hivyo awe na ujuzi wa kompyuta wa kawaida yaani kila anayetoka katika *TTC* awe *computer literate*. Baada ya kuwa na walimu wa aina hiyo ndipo tutawenza kuanza ufundishaji wa somo hilo katika shule zetu zote.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuniona. Pamoja na kwamba nashukuru jibu limeweza kuridhisha na kutoa mwanga kwamba tunaelekea wapi. Lakini kwa vile Serikali imekiri kwamba mpango huu umeanza kwa vyuo vya ualimu ndiyo wanafundishwa. Je, hawa walimu wanaomaliza sasa hivi ambao watakwendwa kufundisha kwenye maeneo ambayo hayana hata umeme elimu hii itakuwa na maana gani sasa hivi kama umeme haujaenezwa kwenye vijiji ambako ndiyo kuna shule hizo? (*Makofit*)

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikubaliane naye kwamba ni dhahiri hatuwezi kuanza kufundisha somo hilo la kompyuta mahali ambapo patakuwa hapana umeme. Kama inavyoolewaka tukianza kufundisha walimu walioko katika vyuo sasa hatutawenza kuanza ufundishaji wa somo hili nchi nzima. Tutakachofanya ni kuwapanga wale walimu vizuri. Wale walimu wenye ujuzi wa kompyuta tutawapanga kwenda kwenye maeneo ambapo katika shule kuna uwekano wa kufikisha umeme.

Kwa hiyo, tutaanza kwanza na pale ambapo inawezekana kuanza na wenzetu wa Wizara inayohusika na usambazaji wa umeme nina hakika tutakuwa na uhusiano kwamba kwa kadri tunavyopanua ufundishaji wa somo la kompyuta na wenyewe wataelekeza usambazaji wa umeme katika maeneo hayo na hatimaye itawezekana kufika katika shule zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna teknolojia ya kisasa kompyuta hazitumii umeme mwingu sana. Kwa hiyo, inawezekana kabisa kutumia *solar energy* ikaweza kuendesha kompyuta. (*Makofit*)

### **Viwango vya Leseni na Mrabaha kwa Makampuni ya Simu za Mikononi**

**MHE. RAYNALD A. MROPE** aliuliza:-

Kwa kuwa mojawapo ya vigezo vinavyotolewa na Tume ya Mawasiliano (*TCC*) kwa Kampuni inayotoa maombi ya leseni kutoa huduma za Mtandao wa Simu za mkononi ni uwezo wa Kampuni kulipia gharama za leseni pamoja na mrabaha, mapato ambayo yanakwenda moja kwa moja Serikalini:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba viwango hivyo vya leseni na mrabaha ni vya juu kiasi kwamba makampuni mengi hususani ya Watanzania yanashindwa kufanya biashara hiyo?

(b) Je, Serikali kwa kushusha viwango vya leseni na mrabaha si ingewawezesha Watanzania wengi kuingia katika soko hilo pamoja na kutoa ajira kwa vijana wengi wasomi waliohitimu masomo hayo na kukosa ajira katika sekta hiyo nyeti inayokua haraka?

(c) Je, kuwepo kwa Kampuni nyingi za kigeni zitoazo huduma hizo ambazo zina uwezo wa kulipia hakutaweza kuathiri usalama wa Taifa ikizingatiwa kwamba mawasiliano kupitia mitandao hii hufanyika bila udhibiti wo wote wa Serikali na hivyo kutoa mwanya kwa njama za kigaidi kufanyika kupitia simu za mkononi bila Serikali kufahamu?

### **NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kudhibiti kuingia kiholela kwa makampuni yasiyokuwa na uwezo, Serikali kupitia Tume ya Mawasiliano inatoa leseni kwa makampuni yenye uwezo kifedha na uzoefu wa muda mrefu katika kutoa huduma. Hii ni kuhakikisha kuwa huduma inayotolewa ni endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilishusha kiwango cha mrabaha kutoka 4% kuwa 1% kwa ajili ya simu za mkononi, hiv yokuyapa uwezo makampuni yanayotoa huduma ya simu za mkononi kuwekeza katika biashara hiyo ikiwa ni pamoja na kutoa ajira kwa wasomi wa Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa makampuni yenye uwezo kifedha hayaathiri usalama wa Taifa kwani yamepewa masharti katika leseni zao. Endapo yatabainika kukiuka masharti hayo, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao. (*Makofî*)

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningeomba kuongezea kwa kuuliza kwamba kwa kuwa hiyo Tume hajatoa rasmi kiwango maalum cha maingiliano ya simu za mkononi, je, ni lini kiwango kitatolewa ili wananchi wapate ahueni kidogo wasiendelee kuumia kama ilivyo sasa hivi?

Pili, je ushuru huu ulio juu mpaka sasa hivi kwa kiwango cha karibu asilimia 7, kwa nini kiwango hiki kisipunguzwe ili mawasiliano haya yaweze kuwafikia watu wengi zaidi na kwa sababu si anasa, sasa hivi mawasiliano haya ni kitu kimoja cha lazima? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Raynald Mrope kwamba, tayari tulishafanya *study* ya *inter connections* na ripoti imetoka lakini tunasubiri sasa Bodi mpya itakapokaa itaipitia na kutoa maoni yake na ninaamini fika Bodi hiyo itashauri vema namna ya *ku-deal* na bei za simu nchini.

### **Upatikanaji na Usambazaji Maji Mjini Lushoto**

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU** aliuliza:-

Kwa kuwa mara kwa mara nimeuliza na kuiomba Serikali isaidie kuimarisha upatikanaji na usambazaji wa maji mjini Lushoto na kwa kuwa mwaka 2003 Serikali ilitenga na kupeleka Lushoto shilingi milioni 13 kusaidia upatikanaji na usambazaji wa maji mjini Lushoto jambo ambalo hatuna budi kutoa shukrani, lakini kiasi cha fedha kilichotengwa hakikutosheleza kutatua tatizo hilo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza mradi wa maji kwa kuvuta maji kutoka Mto Kibohelo kupelekwa Lushoto ili kutatua kabisa tatizo la uhaba wa maji mjini Lushoto na maeneo yanayozunguka mji huo, kama vile Kwembago, Magamba, Doch na Ubiri?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Mji wa Lushoto na vijiji vinavyouzunguka mji huo kama vile Kwembago, Magamba, Doch na Ubiri vinakabiliwa na upungufu wa kukauka vyanzo vya maji, hasa wakati wa kiangazi. Kwa kiasi kikubwa tatizo hili hutokana na uharibifu wa mazingira hasa ukataji miti na ulimaji ovyo kwenye maeneo ya misitu yaliyokatazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Lushoto unapata maji yake kutoka kwenye vyanzo vya maji vya Kamfa na Kwembago. Chanzo cha maji cha Kamfa kinatoa maji kiasi cha mita za ujazo 432 kwa siku, wakati chanzo cha maji cha Kwembago kinatoa maji kiasi cha mita za ujazo 518 kwa siku. Vyanzo vyote viwili vinatoa maji kiasi cha mita za ujazo 950 kwa siku, wakati mahitaji ya maji kwa mji wa Lushoto ni mita za ujazo 1,800 kwa siku na hivyo kuacha upungufu mkubwa wa upatikanaji wa maji kwa ajili ya Mji wa Lushoto. Kutokana na upungufu huo, ili kukabiliana na upungufu uliopo Serikali ilibuni mradi wa kutoa maji mto Kibohelo unaokisiwa kugharimu shilingi milioni 863.

Kwa kuwa mradi huu ni wa gharama kubwa, Serikali inaendelea kutafuta fedha kutoka kwa wahisani mbalimbali ili kugharimia utekelezaji wa mradi huo. Aidha, Serikali inaangalia pia uwezekano wa kupata vyanzo vingine ambavyo ni vya gharama nafuu ili viweze kuongeza uzalishaji wa maji, wakati ambapo mradi wa mto Kibohelo unaendelea kutafutiwa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati juhud za kutafuta fedha kugharimia ujenzi wa mradi wa mto Kibohelo zinaendelea, Serikali imetayarisha mpango wa muda mfupi wa kukarabati chanzo cha Kwembago kwa gharama ya shilingi 3,944,000 na kukarabati bomba la kuvuta maji kutoka chanzo cha Kamfa kuelekea mjini kwa gharama ya shilingi 16,712,500. Serikali tayari imekwishatoa shilingi milioni 13 kwa ajili ya kazi hii. Serikali kuititia Halmashauri ya Wilaya, itatoa kiasi cha shilingi 7,656,500 katika kipindi cha mwaka 2004/2005, ili kukamilisha ukarabati uliobaki. Mpango huu wa muda mfupi, unatarajia kuongeza maji kiasi cha mita za ujazo 250 kwa siku na hivyo kuongeza maji kutoka mita za ujazo 950 kwa sasa hadi kufikia mita za ujazo 1,200 kwa siku. Kiasi hicho cha maji ni sawa na asilimia 67 ya mahitaji ya maji ya mji wa Lushoto.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina swal moja la nyongeza.

Pamoja na juhud za Serikali ambazo kwa kweli nashukuru na wananchi wa Lushoto wanaishukuru sana Serikali na hasa Waziri na Naibu wake ni katika eneo ambalo chanzo cha maji ya Kwembago yanatoka. Kwa bahati mbaya mwaka 1998 iliingia moto na kuharibu sana uoto wa asili.

Je, Serikali inakubaliana na ushauri wangu kuwasiliana na Wizara ya Maliasili na Utalii ili kukata miti ya *Eucalyptus* ambayo kwa jadi inanyonya maji badala ya kuongea maji ambayo inaota sana katika eneo hili ili kunusuru chanzo hiki cha Kwembago?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli baadhi ya aina ya miti ya *Eucalyptus* inachukua maji sana kwa siku kwa ajili ya *nourishment* ya mmea wenyewe. Lakini pia napenda kumwomba Mheshimiwa Henry Shekiffu ajaribu kuleta wazo hilo kwa kupitia Halmashauri ya Wilaya ambapo Idara ya Misitu na Maliasili ipo hivyo kuona uwezekano kama Wizara inayohusika inaweza kutoa kibali hicho cha kubadilisha miti hiyo ili iweze kukidhi mahitaji ya maji kwa ajili ya matumizi ya mji wa Lushoto. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada zake hizo hizo ajaribu kuzungumza na Halmashauri ya Wilaya ambao watatoa usaidizi mkubwa.

Na. 164

### **Huduma ya Maji - Mji wa Geita**

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na hali ya kurudi nyuma kimaendeleo katika sehemu zile ambazo zinazalisha Pato la Taifa kama vile maeneo yanayozalisha dhahabu, almasi, umeme na kadhalika na kwa kuwa Wilaya ya Geita ni mionganoni mwa maeneo yaliyosahaulika na inazalisha dhahabu kwa wingi inayochangia Pato la Taifa, lakini wananchi hawana maji ya bomba.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuupatia mji huo maji ya bomba?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Mabina, Mbunge wa Geita, kama ifuatavyo:-

Mji wa Geita hupata maji yake kutoka katika visima vifupi 6, chemchemi ya Lwenge na Bwawa la Nyamalembo. Pia viro visima vifupi kadhaa vya watu binafsi.

Ni kweli kuwa mahitaji ya maji kwa mji wa Geita wenyе idadi ya watu takriban 30,000 yanafikia zaidi ya mita za ujazo 2,100 kwa siku wakati uwezo wa vyanzo vyote vya maji nilivyovitaja ni mita za ujazo 100 tu. Mahitaji ya maji yanaongezeka kwa kasi kutoptaka na kukua kwa mji huo kunakosababishwa na shughuli za uzalishaji wa dhahabu kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi wa maji ya bomba uliopo mjini Geita wenyе chanzo chake katika Bwawa la Nyamalembo, lenye ukubwa wa mita za ujazo zipatazo milioni 1.05, ni wa zamani sana na umechakaa.

Kutokana na uchakavu wa mradi huo Halmashauri ya Wilaya ya Geita inakusanya mapato madogo tu yanayokadirwa kuwa shilingi 200,000/= kwa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya mradi wa maji mjini Geita imefanyika Januari, 2003 na kuwezesha kuandaa mahitaji ya kuimarisha huduma ya maji katika mji wa Geita. Tathmini hiyo imependekeza kufanya ukarabati wa nyumba ya mitambo, kununua mitambo mipy, kukarabati matanki 2 ya maji yaliyopo kwenye kilima cha Katoma na kuweka mabomba mapya kwenye mtandao uliopo kwa gharama ya shilingi 130,000,000/=. Ili kuondoa kabisa tatizo la maji katika mji wa Geita inapendekezwa kujenga mradi mkubwa ambao utatumia maji ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukubwa wa mradi, Serikali inawasiliana na wafadhili mbalimbali ili kupata fedha za kutosha kutekeleza mradi huo. Maombi ya fedha yamewasilishwa kwa wafadhili kama ifuatavyo:-

- Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADC*); maombi yaliwasilishwa Oktoba, 2002 na Agosti, 2003.
- *JICA*, maombi yaliwasilishwa Aprili, 2003.
- *China Africa Cooperation Forum*, maombi yamewasilishwa Novemba, 2003.

Majadiliano na wafadhili hawa bado yanaendelea.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba mji wa Geita hauna huduma ya maji na juzi juzi Serikali imesaini mkataba wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Shinyanga na mradi ule umegharamiwa kwa fedha za Serikali na kutoka Ziwa Victoria kuja Geita kuna umbali wa kilomita 22, je, Serikali haioni ni busara badala ya kuwategemea wafadhili ikachukua fedha zake binafsi ikajenga mradi huo kupeleka maji Geita? (*Makofit*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mji wa Geita una matatizo ya maji lakini ukiangalia uwezo wetu wa fedha wa ndani hauwezi kugharamia miradi yote ya maji ambayo inahitajika nchi nzima. Kwa hiyo, ndio maana tumetafuta njia nyingine mbadala na njia hizo ni kama mikopo kama nilivyooleza kutoka *ADB* tunajaribu kuona kama tunaweza kukopa na kukopa ina maana tutalipa. Kwa hiyo, uwezo wetu ndio unaotukwaza katika kutekeleza mahitaji ya wananchi wetu. Lakini nina hakika mazungumzo yanayoendelea hivi sasa yatatoa ufumbuzi wa upatikanaji wa maji kwa ajili ya mji wa Geita.

Na. 165

#### **Upotevu wa Fedha na Mali za Serikali**

**MHE. LEKULE M. LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa upotevu wa fedha na vifaa vilivyoombewa kibali cha kufutwa na Waziri wa Fedha pamoja na mapato ya maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa ni fedha nyingi mno kiasi cha kusababisha wasiwasi Bungeni au kuonyesha uwezekano wa mazingira ya wizi:-

- (a) Je, kwa nini fedha hizo nyingi ambazo zimepita mikononi mwa watu au waliohusika hawakuchukuliwa hatua haraka?
- (b) Kwa kuwa fedha hizo nyingi ambazo zimepotea kwenye Ofisi za Serikali, je, kwa nini wahusika wanaachwa kwa muda mrefu mpaka wapotee bila kuwajibishwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la upotevu wa fedha na mali za Serikali limewekewa utaratibu wa namna ya kulishughulikia kama tunavyoolekezwa na Kanuni mpya za Fedha (*Public Finance Regulations*) kuanzia Kifungu cha 13 hadi 22.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni na Sheria mpya za fedha zimeanza kutumika kuanzia tarehe 1 Julai, 2001. Kabla ya hapo, upotevu wa fedha na vifaa vilivyoombewa kibali cha kufutwa hapa Bungeni haukuwa wa uwazi kama ilivyo hivi sasa ambapo ufutaji wa potevu ni lazima uletwe Bungeni ili kupata kibali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba sasa kujibu swalii la Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa hatua za kisheria zilichukuliwa baada ya matukio ya upotevu kutolewa taarifa Polisi na watuhumiwa kufunguliwa kesi Mahakamani baada ya uchunguzi wa kina kufanyika. Aidha, matukio haya yametokea katika baadhi ya Wizara, Mikoa na Idara za Serikali zinazojitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufafanuzi zaidi mchangunuo wa potevu hii ya fedha na vifaa vya Serikali ambavyo ni shilingi 49,432,496,297.00 kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2002 na hatua zilizochukuliwa ni kama ifuatavyo:-

- Hatua za kisheria zimechukuliwa dhidi ya potevu ya shilingi 4,660,102,448.000, kati ya kiasi hicho shilingi 4,250,717,961.00 zimefutiwa mashtaka na kuchukuliwa hatua za kinidhamu kama kufukuzwa kazi na kadhalika.
- Potevu zenye thamani ya shilingi 4,744,665,548.00 ni za wahusika ambaao aidha waliofariki dunia, kustaafu, kutoroka kabla ya kuchukuliwa hatua zozote na potevu kiasi cha shilingi 40,077,729,201.00 zimetokana na wadaiwa kafilisika au kuwepo kwa mabadiliko ya kisheria.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, wahusika hawakuachwa wapotee bali hatua za kisheria zilichukuliwa kama ilivyoeleza hapo awali. Aidha, baada ya kufunguliwa kesi Mahakamani, waliopatikana na hatia walihukumiwa kifungo na wengine waliachiwa huru kwa kukosekana ushahidi dhidi yao hivyo kushinda kesi, wengine waliofariki dunia wakiwa kifungoni na wengine wamefariki dunia wakati kesi zikiendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na sababu zilizotajwa hapo juu isingewezekana kupata fidia ya potevu hizo na hivyo zimekuwa hasara kwa Serikali na ndiyo maana ya kuliomba Bunge kibali cha kufuta potevu hizo ili zisiendelee kuonekana katika vitabu vya Serikali.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya uwazi ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Kwa kuwa ukaguzi wa mahesabu ya Serikali yanafanyika kwa mwaka mmoja kwa mfano hesabu za mwaka jana zinafanyika mwaka huu, je, hiyo haisababishi fedha za Serikali kupotea kwa muda mrefu bila kugundulika?

(b) Kwa kuwa mikataba ya Serikali inabadilika na kusababisha fedha za Serikali kupotea kwa mfano mkataba wa *TTCL* jana tumesikia kwamba kutoka shilingi bilioni 60 zilizokubalika wakati wa mkataba sasa tunalipwa shilingi bilioni 5. Je, mikataba hii haikuwekwa kisheria? (*Makofit*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwa sababu hesabu zinachukua muda mrefu kukaguliwa hapo zamani yanaweza kutokea matatizo hayo lakini kama nilivyoeleza katika maswali ya nyuma likiambatana na lako mwenyewe la tarehe 1 Agosti, 2003 na la Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga la mwaka 2002 tulisema kwamba mfumo uliopo sasa hivi kwa *Integrated Financial Management System* wa kutumia *computer* unauzuia wizi au upotevu kukaa muda mrefu bila kujulikana kwa sababu ya *Expenditure Tracking System* ambayo imewekwa na Wizara ya Fedha, sasa hivi sio rahisi upotevu unaweza kuonekana pale pale na ndio maana sasa hivi unaweza kusikia kwamba Wizara au Idara fulani upotevu uliopotea umeweza kujulikana pale pale bila kuchukua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikataba, kweli inaweza kutokea na kama ulivyosema imetokea kwa *TTCL* lakini wakati unapotokea mzozo kwa kitu chochote kile cha mkataba baina ya Serikali na kampuni yoyote au baina ya Serikali na taasisi nyingine yoyote ile na kipengele kinachosema

kunapokuwa na mzozo kutakuwa na msuluhishaji wa Kimataifa wa mzozo ule wa kibiashara ambaye atatoa suluhishi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kuwa Kamati iliyochaguliwa na Serikali ili kuangalia mzozo huu wa *TTCL* na Serikali hatua iliyochukuliwa imechukuliwa kwa mujibu wa sheria kabisa na kwa mujibu wa mkataba ulitiwa saini na Serikali na taasisi au kampuni iliyohusika.

Na. 166

### **Uendelezaji wa Viwanja**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI** aliuliza:-

Kwa kuwa uendelezaji wa makazi ya Miji ni jukumu la Serikali; na kuwa kuwa ugawaji wa viwanja hufanywa katika mbuga, nyika, mapori na hata mashambani na aliyepewa *offer* hutakiwa kulipia gharama zote na kukiendeleza kwa muda maalum uliowekwa kisheria kwa kujenga na kufanya matumizi yalivyokusudiwa:-

- (a) Je, Serikali haijui kwamba haiwezekani kuendeleza kiwanja mahali ambapo hapapitiki kwa gari (hakuna barabara) na hakuna maji?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha hayo kwa kujenga barabara na kuweka maji kila inapotoa viwanja ili uendelezaji uweze kufanywa kwa haraka na gharama nafuu?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuweka miundombinu ya msingi ya kiuchumi na kijamii katika maeneo mapya ya miji yanayopimwa viwanja. Miundombinu hiyo siyo barabara na maji pekee, bali ni pamoja na umeme, mawasiliano, mifumo ya majitaka, mifumo ya maji ya mvua na huduma za kijamii za elimu, afya, burudani, maegesho ya magari na kadhalika. Tatizo linalosababisha ugawaji wa viwanja katika baadhi ya maeneo kufanyika bila kuweka miundombinu ni upungufu wa fedha unaosababishwa na ufinyu wa bajeti ya Serikali. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa ni kweli haiwezekani kuendeleza kiwanja mahali ambapo hakuna miundombinu ya msingi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kulikabili tatizo hilo, Serikali itaendelea kutafuta uwezo wa kifedha ili kufanya maandalizi muhimu katika maeneo yanayopimwa viwanja. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara yangu ilibuni mradi wa kupima viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es Salaam kwa kushirikiana na Halmashauri zake. Mradi huo unahusisha uchongaji wa barabara kwa kiwango cha changarawe kwa lengo la kila kiwanja kufikiwa na barabara.

Pia utafiti wa upatikanaji wa maji unafanywa kwa kushirikiana na mamlaka zinazohusika. Utaratibu huu tutauendeleza katika maeneo mengine na napenda kutoa wito kwa Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya kutenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya kuweka huduma muhimu katika maeneo yanayopimwa viwanja. Gharama za fedha zilizotumika, zinaweza kurudishwa kwa kujumuishwa katika gharama zinazolipwa na wanaogawiwa viwanja.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa amekiri kwamba Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo na miundombinu ile inayomgusa moja kwa moja mwenye kupewa kiwanja na inayogusa Serikali vile vile kama shule na

kadhalika, je, mwananchi anapokuwa tayari amepewa kile kiwanja na anatakiwa kukiendeleza ndani ya miezi 36 lakini hawesi kufika pale kwa sababu hakuna barabara, je, Serikali itamfidia ule muda anaopoteza katika kuendelea kusubiri barabara zile ziweze kuwepo?

(b) Kwa kuwa kabla eneo halijaweza kuwa mji huwa ni mahali ambapo watu wanajikusanya taratibu tu wakiwa wanafanya shughuli zao kwa mfano za biashara wakija asubuhi na kuondoka jioni baadaye wanaanza kuendeleza vibanda vidogo vidogo na baadaye wanaanza kuweka makazi wakati huo pale kuna Serikali za Vijiji, Mitaa, Vitongoji wanawaona tu wakiwa wanafanya hivyo lakini hawawakemei, je, Serikali itaweka utaratibu gani ili kuondo taratibu hizi kubomoabomoa na kuifanya Serikali itoe gharama kubwa za fidia kabla hiyo miji haijendelezwa kuwa imeshaweka taratibu za miundombinu pale inapoona wananchi wanaanza kuonyesha *interest* za kuhamia pale? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba kuna umuhimu wa kuweka miundombinu lakini pia ni lazima mwananchi aweze kuchangia, siku hizi hakuna kitu cha bure au kutumia Serikali peke yake kwa sababu fedha haipatikani kwa urahisi.

Kwa hiyo, anayepata kiwanja kwanza na yeche mwenyewe aweze kujianaa mahali ambapo anajenga lakini Serikali na Halmashauri ziko tayari kusaidia pindi wanapokuwa na fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi ambao wanaendelea kujenga au wanafanya biashara na kujenga vibanda vidogo vidogo baadaye ukawa ni mji, haya yote kinachotakiwa ni elimu kwa wananchi kutambua maeneo ambayo yamekatazwa kujenga nyumba bila kupima lakini wananchi wanaamua tu kwenda kujenga ili kuihodhi nafasi hiyo wakati wa bomoabomoa basi anasema anaomba fidia. Elimu hii ni sisi wenyewe Wabunge, Halmashauri zetu na pia wataalam wetu wazunguke katika maeneo husika kuhakikisha kwamba watu hawajengi kiholela kwa sababu wataleta tatizo baada ya kujenga kiholela watahitaji barabara ambayo haitawezekana, watahitaji maji haitawezekana kuitisha hata umeme. Kwa hiyo, hii elimu naomba endelee kutolewa na sisi sote na kuheshimu sheria zilizopo katika kujenga miji yoyote ile katika nchi yetu.

Na. 167

#### **Huduma ya Umeme**

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wengi wa Wilaya ya Mwanga wameomba na kulipia huduma ya umeme kwa muda mrefu; na kwa kuwa wengine wao wametekeleza masharti yote ya kuwekewa umeme lakini *TANESCO* imekataa kupokea maombi na malipo yao ili wapatiwe umeme; na kwa kuwa wanavijiji katika maeneo unapozalishwa umeme wa Bwawa la Nyumba ya Mungu wameombwa na kuahidiwa umeme kwa muda mrefu sasa:-

(a) Je, ni lini *TANESCO* itatekeleza mkataba kwa upande wake wa kuwapatia huduma ya umeme wananchi ambao wamelipia gharama zote zinazohusika kuanzia mwaka 1994 hadi 2002?

(b) Je, kuna sababu gani za msingi zinazoifanya Serikali ilipie gharama za kusambaza umeme katika maeneo kama Kituri, Mlevo na kadhalika na kuwashamasisha wananchi wajitayarische kupatiwa umeme lakini wanapokuwa tayari *TANESCO* ikatae kuwapatia huduma hiyo?

(c) Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa vijiji vya Njia Panda, Kiti cha Mungu na Handeni ambao wanaishi mahali ambapo umeme unazalishwa na ambao pamoa na ahadi nyingi, hawajapatiwa umeme hadi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Jumanne Abdallah Maghembe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwaka 1993 hadi 1998, Serikali ya Tanzania kwa ufadhili kutoka Serikali ya Japan ilitekeleza mradi wa kusambaza umeme katika Wilaya ya Mwanga. Mradi huo uliojulikana kwa jina la *Kilimanjaro II* ulitekelezwa kwa wananchi wengi waliopatiwa huduma hiyo ya umeme kwa kadri ya fungu la fedha lililotolewa na wafadhili. Kutokana na kumalizika kwa fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya mradi huo wananchi wote waliojitarisha hawakuweza kufikiwa na huduma ya umeme mradi ulipomalizika. Serikali kwa kupitia Shirika la Umeme *TANESCO* ilianza kutafuta fedha za kuendelea na kusambazaji umeme kwa wananchi ambao hawakufikiwa na haduma hiyo wakati wa utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha mwaka 1994 hadi 2002, *TANESCO* iliwasambazia umeme jumla ya wananchi 2,534 kati ya wananchi 2,736 walioomba na kulipia ghamara za kuunganishiwa umeme. Utekelezaji huo ni wa mradi ulikuwa ni wa asilimia 93. Aidha, walibakia wananchi kama 202 kati ya hao 2,736 ambao walilipia huduma ya umeme wakati wa utekelezaji wa mradi lakini hawakufikishiwa huduma hiyo ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya vijiji vilivyobaki wakati ule ilikuwa ni kijiji cha Kituri. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba hivi sasa kazi ya kufikisha umeme katika kijiji cha Kituri imeshaanza. Nguzo zimechimbiwa na kazi ya kusambaza nyaya imekwisha. Kinachosubiriwa ni *transformer* ambayo tayari imeagizwa kutoka *TANALEC*, Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kijiji cha Mlevo kilishapatiwa umeme tangu Februari, 2002 na jumla ya wateja 24 wanafahamika kuwa wameunganishiwa huduma hiyo ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jumla ya vijiji kama nane vinavyozunguka Bwawa la Nyumba ya Mungu. Kati ya vijiji hivyo vitano vimepatiwa umeme. Kijiji cha Kiti cha Mungu kilichotajwa na Mheshimiwa Mbunge ni moja ya vijiji ambavyo vimepatiwa umeme. Vijiji ambavyo bado havijapatiwa umeme ni Njia Panda, Shauri Moyo, *National* na Handeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, vifaa vyote ambavyo vinahitajika kwa miradi ya vijiji hivi vimepatikana na kazi ya kusambaza umeme inatarajiwa kukamilika katika mwaka huu wa 2004. Kwa mifano, kijiji cha Njia Panda na Shauri Moyo, umeme unatarajiwa kuwashwa mwezi wa Aprili, 2004. Kijiji cha *National* kazi ya nguzo tayari na shughuli zingine zinaendelea. Kazi katika jiji cha Handeni inatarajiwa kuanza mara baada ya kazi katika vijiji vingine kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, kwa jitihada zake za kufuutilia usambazaji wa umeme kwenye vijiji hivyo alivyovitaja katika swali lake.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na naishukuru sana Serikali kwa juhudhi kubwa ambazo zimefanywa katika kukamilisha miradi midogo midogo ya umeme katika Jimbo langu la Mwanga.

(a) Kwa kuwa tulipata msaada kupitia juhudhi zangu mwenyewe kama Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Mwanga tukaipatia *TANESCO* shilingi milioni 12 kwa ajili ya kununua vifaa vyta kusambaza umeme katika vijiji vyta *National* na Njia Panda na kwa kuwa tumehakikishiwa kwamba umeme huo utawashwa mwezi wa nne, ninapenda sasa nielewe ni lini katika vijiji vyta Kituri, Mbambua na Kiverenge *transformer* nako zitafika kwa sababu kazi ya kusambaza umeme inaendelea?

(b) Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri atupe mwanga ni lini wananchi 202 ambao wameshalipia gharama za kufungiwa umeme katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Mwanga watapewa umeme? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kama ambavyo nimesema katika jibu la msingi, nimempongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa juhudzi zake za kufuatilia suala la utekelezaji wa Usambazaji wa umeme katika Jimbo lake. Napenda nimhakikishie kwamba pamoja na juhudzi zake Serikali nayo katika gharama zote za kusambaza umeme imefanya jitihada kubwa na gharama zote ni shilingi milioni 150 na kijiji cha Kituri alichokitaji ni moja ya vijiji ambavyo nimesema kwamba ifikapo Aprili, 2004 tunatarajia kwamba umeme utawashwa pale.

Kitu ambacho kilikuwa kinasubiriwa ni suala la *transformer* ambayo kama inavyofahamika inabidi iagizwe kutoka *TANALEC*, Arusha na huchukua muda mpaka kupatikana kutokana maagizo mahususi ambayo *TANESCO* hutoa kwa utengenezaji wa transformer hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wananchi 202 ni katika juhudzi zote ambazo nimesema za kusambaza umeme kwamba hawa ndio watakaofikiwa na huduma ile ya kusambaziwa umeme mara mradi utakapokamilika katika vijiji vyote vilivytajwa.

Na. 168

#### **Wawekezaji Kwenye Migodi Kusaidia Wachimbaji Wadogo wadogo**

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi waliokuwa wanajihuisha na uchimbaji mdogo wa madini nchini baada ya maeneo yao kupatiwa wawekezaji; na kwa kuwa hatua hii imewafanya wananchi hao kukosa ajira/kipato na hatimaye kuishia kuwa fukara; na kwa kuwa Serikali imetoe matamko mbalimbali kuonyesha inavyofaidika na pato kutoka katika migodi hiyo; na kwa kuwa hakuna mikataba inayowabana wawekezaji kutenga pato kuimarisha huduma za jamii katika maeneo husika (isipokuwa kwa hiari yao):-

(a) Je, Serikali ina mpango gani mahsusii kusaidia wananchi hao waliozoea kuchimba madini kupata nafasi shirikishi na ikiwezekana wapewe hisa kwa kiwango kitakachoonekana kinafaa badala ya hali ya sasa ambapo inaonekana walikuwa makorokoroni wa madini hayo?

(b) Je, bila Watanzania kushirikishwa kama wadau kwenye sekta hiyo ya madini itawezekana vipi kusema wananaufaika na maliasili hiyo ya nchi?

(c) Je, Sheria ya Madini ya mwaka 1998 siyo kwamba inawakandamizi wazawa kuingia ubia na wachimbaji wa nje kama inavyofanyika kule Ghana ambako wananchi wa Ashanti ni wabia kwenye mgodi unaomilikiwa kwa pamoja na Wamerikani (*Anglo American*)?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahim W. Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kuitia Kamati ya ushauri wa madini imeanza mpango wa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Hivi sasa maeneo kadhaa yameshatengwa kama vile (Sakale) Muheza, Tunguli (Kilindi) na baadaye utaratibu unafanywa kwa hivi sasa kuweza kutenga eneo la Maganzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya yanapotengwa, huundwa Kamati maalum za ugawaji viwanja chini ya Uenyekiti wa Mkuu wa Wilaya. Wajumbe wengine wa Kamati hiyo huwa ni Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo husika, Mwenyekiti wa Halmashauri na wajumbe watatu wanaoteuliwa na Waziri wa

Nishati na Madini baada ya kushauriana na uongozi wa Mkoa. Kwa kuitia Ofisi za Madini iliyoko katika eneo husika wananchi hujulishwa wajitokeze kuomba leseni za madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge juu ya umuhimu wa kushirikishwa Watanzania katika sekta ya madini. Hivi sasa Watanzania wanashiriki kama wachimbaji madini, wafanyabiashara ya madini na watoaji huduma mbalimbali kwenye migodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wanafaidika pia na uchimbaji madini nchini kwa kupata mrabaha au mrabaha, kodi mbalimbali na huduma za jamii. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Madini iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu haiwakandamizi wananchi na kwa kweli Bunge hili halina tabia ya kutunga sheria ya kuwakandamiza wananchi wanapotaka kuingia ubia na wachimbaji wa nje bali baadhi ya wananchi wenye leseni za madini wanakuwa wepesi mno kuingia mikataba kwa malipo madogo na wawekezaji wa kutoka nje bila kuzingatia manufaa ya muda mrefu. Nchini Ghana, Serikali ya nchi hiyo ndiyo yenye hisa 19% kwenye Kampuni ya *Ashanti Goldfields Company Limited*. Wananchi wa Ghana hawana hisa moja kwa moja katika migodi ya kampuni hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo hayo, Serikali imeshachukua hatua za ziada. Tarehe 16 Februari, 2004 hapa Dodoma, Mheshimiwa Waziri Mkuu alizindua Kamati ya kudurusu Sera ya Madini. Pamoja na mambo mengine Kamati hiyo, chini ya Uenyekiti wa Dr. Jonas Kipokola, inatakiwa:-

- (a) Kuangalia upya Sera ya Madini hususan kuhusiana na ushiriki wa Serikali katika umiliki wa migodi kwa kulinganisha na nchi nyingine.
- (b) Kuchunguza mgawanyo wa mapato ya mauzo ya madini kati ya Kampuni na Serikali na kushauri iwapo viwango vya mrabaha, kodi na vivutio vingine vinahitaji kurekebishwa.
- (c) Kutathmini utoaji wa huduma za jamii unaofanywa na migodi, uharibifu wa mazingira na malalamiko ya fidia.
- (d) Kutathmini hatua ambazo Serikali imekuwa ikichukua katika kuwasaidia wachimbaji wadogo na chimbuko la mgogoro kati ya wachimbaji wadogo na wakubwa.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Katika jibu lake Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba Serikali iko kwenye mpango wa kukamilisha Sera ya Madini lakini kwa mazoea mambo haya huchukua muda mrefu na madini sio zao ambalo linakuwa *replaced*, je, sera hii itachukua muda gani ili wakati huo madini yasiwe yamekwisha kwenye migodi hiyo? (*Makofit*)

(b) Kwa sababu katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumzia pia mpango wa Serikali kuangalia uwezekano wa kumiliki *share* kwenye hii migodi.

Je, Mheshimiwa Waziri hajui kwamba kama mipango hii itachukua muda mrefu Serikali itakwenda kumiliki mashimo yaliyo tupu huko migodini? (*Makofit*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilichosema katika jibu langu la msingi ni kwamba imeundwa Kamati ya Kudurusu Sera ya Madini, si kwamba Serikali inatunga Sera ya Madini hivi sasa. Sera ya Madini ipo na tumekuwa nayo tangu mwaka 1997 na baadaye kutungwa sheria mwaka 1998 na Utaratibu wa Uchimbaji Madini mwaka 1999. Sera ipo, kinachofanywa ni kudurusu sera hiyo kutokana na malalamiko ambayo yamekuwa yakitoka katika sehemu nyingi ikiwemo katika Bunge hili na ndiyo maana Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi wakati wa Bunge la Bajeti kwamba Serikali ingetazama upya suala hili na ndiyo maana ikaundwa Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuhusu mpango wa Serikali wa kutathmini upya na je, hatutakuta mashimo matupu.

Kwanza napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba Kamati hii ambayo imeundwa haitarajiji kuchukua muda zaidi ya mwaka huu wa 2004. Lakini nataka niseme pia kwamba nchi yetu katika suala zima la uchimbaji mkubwa wa madini ndiyo kwanza imeanza kazi hiyo kwa kiwango hiki ambacho tunacho hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina utajiri mkubwa wa madini karibu katika kila eneo na Serikali imeunda Kamati hii kama nilivyosema awali kwa nia au kwa mintarafu ya kuhakikisha kwamba yale yote ambayo tunatakiwa tunufaikie nayo katika sekta ya madini na hususan katika kupiga vita umaskini yanapatikana. Ni nia ambayo inatekelezwa kutokana na ahadi ambayo ilitolewa hapa Bungeni.

Na. 169

### **Barabara ya Katoma - Kanyigo hadi Kashenye**

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Katoma-Gera-Kanyigo hadi Kashenye katika Jimbo la Nkenge ni muhimu sana katika kuunganisha Tarafa ya Kiziba na njia ya Bukoba.

Je, ni lini Serikali itakarabati barabara hiyo kwa kiwango cha juu ili kurahisisha usafiri katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Katoma-Gera-Kanyigo-Kashenye yenyе urefu wa kilometa 41 ni barabara ya Mkoa na inahudumiwa na Wizara yangu kuititia Wakala wa Barabara (*TANROADS*), Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii imekuwa ikipatiwa matengenezo muhimu kila wakati kwa lengo la kuifanya iendelee kuitika bila matatizo. Baadhi ya matengenezo hayo ni kama haya yafuatayo:-

Katika mwaka wa fedha 2000/2001, sehemu ya barabara hii kati ya Katoma hadi Kanyigo yenyе urefu wa kilometa 30 ilipatiwa matengenezo maalum kuititia mradi wa *Kagera Road Maintenance (KAROM)*. Matengenezo hayo yaliyogharimu kiasi cha shilingi milioni 154.8/= yalihusisha kazi za ujenzi wa makalvati, kuchonga barabara na kuweka changarawe kwenye maeneo korofí.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2001/2002, kipande kilichobakia chenyе urefu wa kilometa kumi kati ya Kanyigo hadi Kashenye pamoja na eneo la Bonde la Kajai lenye urefu wa kilometa 1.4 vilifanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe kuititia mradi wa *Kagera Agriculture and Environment Management Project (KAEMP)*. Matengenezo hayo yaligharimu kiasi cha shilingi milioni 310.7/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, barabara hii vilifanyiwa matengenezo ya kawaida kwa gharama ya shilingi milioni 8.4/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, hadi kufikia robo ya pili, Serikali imeifanya matengenezo ya kawaida barabara hii yaliyogharimu shilingi milioni 8.6/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha barabara hii inakuwa imara zaidi, Serikali imeandaa mpango wa kuikarabati barabara hii kwa kutumia fedha zinazotolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika

(ADB). Matengenezo haya yatahusisha kuchonga na kuiwekea tabaka la changarawe barabara yote, kuimarissha madaraja ya Tingatinga ya Kajai na ujenzi wa makalvati maeneo yanapohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkandarasi wa kutekeleza kazi hizi ameshapatikana na yupo katika hatua za maandalizi na anatarajia kuanza kazi mwezi Februari, 2004. Matengenezo haya yanatarajia kugharimu jumla ya shilingi milioni 713.2/= na yanatarajiwa kukamilika ndani ya miezi kumi. Kwa hapa nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia kwa karibu sana juu ya barabara hii. (*Makofit*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumemaliza maswali, hili la mwisho halikuwa na la nyongeza, kweli kulikuwa na hatari ya kukosa muda wa kuuliza maana muda umefika. Sasa kuna matangazo.

Nimepata *ki-note* hapa wanaulizia wale ambao walikuwa na maswali siku ile ambayo Mheshimiwa Rais alikuja kuhutubia Bunge. Nadhani ufanuzi mzuri sana ultolewa na Mheshimiwa Spika, kuhusu hili. Narudia kwa wale ambao pengine hawakuwepo siku ile, yale maswali bado yataendelea kupangwa kwa kadri nafasi itakavyopatikana, kama yatabaki basi Bunge lijalo yataendelea kwa utaratibu huo.

Sasa matangazo, Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara anawatangazia wajumbe wa Kamati hiyo kuwa kutakuwa na kikao leo Alhamisi, tarehe 19 Februari, 2004, saa tano asubuhi. Kikao kitafanyika chumba cha Kamati Namba 133 ghorofa ya kwanza.

Pia Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, anawatangazia wajumbe wake kwamba kutakuwa na mkutano saa tano asubuhi hii katika chumba Namba 227, ghorofa ya pili, *wing C*.

Vile vile Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Njelu Kasaka, anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati kujadili taarifa ya kazi ya mwaka 2003. Kikao kitafanyika saa tano asubuhi, chumba Namba 428 na 432. Sijui watafanyaje, naona vyumba viwili hapa, lakini nadhani wenyelele wameelewa.

Sasa mikutano ya Kamati za Vyama mbalimbali. Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Katibu wa Kamati ya Wabunge wote wa CCM, anawatangazia wajumbe wa Kamati hiyo kuwa kutakuwa na mkutano leo jioni baada ya kuahirisha Bunge jioni.

Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, *Chief Whip* wa *Opposition* anawatangazia wajumbe wa Kambi hiyo kukutana leo saa saba mchana, Ofisi za Kambi ya Upinzani.

Kuhusu mikutano ya Vyama mbalimbali vya Wabunge, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mwenyekiti wa *TAPAC*, anawatangazia wajumbe au wanachama wa Chama hicho kwamba kutakuwa na mkutano saa saba mchana baada ya kuahirisha Bunge asubuhi hii.

Baada ya matangazo haya sasa tunaendelea, Katibu.

## KAULI ZA MAWAZIRI

**Tamko la Ufanuzi juu ya Kampuni ya Kahama Mining Corporation kutumia Maeneo ya Kijiji bila kujali Mazingira**

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa maelezo kuhusu hoja ya Mheshimiwa Emmanuel Kipole, Mbunge wa Msalala ya tarehe 13 Novemba, 2003 kwamba Waziri wa Nishati na Madini atoe tamko la ufanuzi juu ya Kampuni ya *Kahama Mining Corporation Limited* kutumia maeneo ya Vijiji kwa shughuli za mgodi bila ya tahadhari ya uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Kampuni ya *Kahama Mining Corporation Limited* ilipewa *Special Mining License No. SML 44/1999*, yenye eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 51.48 kwa ajili ya kuchimba dhahabu katika eneo la Bulyankhulu Wilayani Kahama.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 38(5) cha Sheria ya Madini ya Mwaka 1998, Kampuni ilifanya na kuwasilisha taarifa za uchambuzi wa athari za mazingira yaani *Environmental Impact Assessment* kwa mradi kabla ya kuanza kuchimba. Jamii ya karibu na mgodi na uongozi wa Wilaya ya Kahama pia ulishirikishwa kutoa maoni yao juu ya manufaa na madhara ya mradi kiuchumi, kijamii na kwa mazingira. Katika taarifa hiyo kampuni ilidhihirisha kutumia barabara itokayo Bulyankhulu, Busoka hadi Isaka kusafirisha mitambo na vifaa vya ujenzi na matumizi ya mgodi kutoka Isaka pamoja na kusafirisha udongo (*concentrate*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa matumizi ya barabara hiyo kampuni iliomba na kupata kibali kutoka Serikalini cha kuiboresha barabara hiyo kutoka katika kiwango cha barabara ya vumbi (*earth road*) kwenda katika kiwango cha barabara ya changarawe bila ya kuweka vikwazo kwa watumiaji wengine. Vile vile kampuni itaendelea kuifanya matengenezo ya mara kwa mara barabara hiyo kwa kipindi cha uhai wa mgodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Mheshimiwa Mbunge imesisitiza kuwa wananchi wengi wameathirika na wanaendelea kuathirika kiafya na kisaikolojia na kwamba yapo matukio mengi ya maradhi ya *TB*, vikohoz, macho na kadhalika ambayo yameripotiwa na yanaendelea kuripotiwa katika zahanati na vituo vya afya kutokana na vumbi linalosababishwa na misafara mirefu ya maroli yanayobeba udongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia hali hii Wizara yangu kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi ya Usimamizi wa Mazingira iliamua kupeleka timu ya wataalam Wilayani Kahama kutathmini kiwango cha tatizo, madhara na kupendekeza tahadhari za kulikabili tatizo hilo. Tunafurahi kuwa timu hiyo ilipata ushirikiano mzuri kutoka kwa uongozi wa Mko, Wilaya, wananchi pamoja na Mheshimiwa Mbunge na uongozi wa *Kahama Mining Limited*. Kutokana na majadiliano yaliyofanywa na wadau mambo yafuatayo yalidhihirishwa:-

(a) Kero ya vumbi kwa wananchi wanaishi kando kando ya barabara hiyo ipo. Vumbi hili halisababishwi na magari ya *Kahama Mining Company* tu bali na magari yote yanayopita katika barabara hii. Hata hivyo kero hii inaonekana zaidi kwa magari yanayobeba udongo kwa sababu yanasaferi katika msururu wa magari kumi na moja hadi kumi na tatu na hivyo kusababisha kiwango kikubwa cha vumbi kwa wakati mmoja. Magari haya hufanya safari mbili kwa wiki.

(b) Hakuna orodha ya watu wanaofahamika walioathirika na vumbi hilo.

(c) Magonjwa ya kifua kikuu, kikohoz na macho ingawa yamedhihirika kuwepo lakini hayana uhusiano wa moja kwa moja kwamba yanatokana na vumbi. Hakuna utafiti uliofanyika kuthibitisha hili. Maelezo ya kitaalam yamebaini kuwa vumbi haliwezi kusababisha *TB* kwani vijidudu vya ugonjwa huu haviwezi kuishi kwenye vumbi.

(d) Malalamiko ya madhara ya vumbi hayakuwahi kuwasilishwa rasmi kwenye vikao vya uongozi isipokuwa katika mikutano ya hadhara ambayo aliifanya Mheshimiwa Mbunge hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba sasa nitoe maelezo yenyenye kujibu vipengele vya hoja ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a) Serikali haikubaliani na kitendo cha wananchi kuathirika au kuendelea kuathirika na vumbi. Ili kupunguza tatizo la madhara ya vumbi linalotokana na magari ya kampuni ya *Kahama Mining Corporation* yaani yanayobeba udongo, Kampuni imeshauriwa naimeahidi kuangalia upya utaratibu utakaotumiwa kwa magari hayo. Aidha, Kampuni imetakiwa ifanye mapitio ya mpango wake wa kuiboresha mazingira ili kuweka wazi tatizo la vumbi linalotimuliwa na magari haya na iainishe njia mbadala za kutatua tatizo hilo.

(b) Uchambuzi uliofanywa haujabaini vipengele vya sheria vilivyokiukwa na Kampuni ya *Kahama Mining Corporation Limited* katika kutumia barabara ya Bulyankhulu-Busoka kwa kusafirisha udongo kutoka mgodini kwenda Isaka. Kampuni kabla ya kuanza uchimbaji ilifanya *environmental impact assessment* ya mradi ambayo kimsingi inajumuisha shughuli zote za mradi ikiwa ni

pamoja na matumizi ya barabara ya Bulyankhulu mpaka Busoka kusafirisha udongo kwenda bandari ndogo ya Isaka.

(c) Kampuni inatumia barabara hiyo na inayo haki kama wafanyakyo watumiaji wengine kusafirisha mazao na mizigo yao kwenda kwenye soko. Kwa misingi hiyo Serikali haiko tayari kutoa tamko la kuzuia Kampuni ya *Kahama Mining Corporation Limited* isiitumie barabara inayopita katika Vijiji vilivytajwa na Mheshimiwa Mbunge kwani kufanya hivyo itakuwa haijatenda haki.

(d) Kampuni haijaongezewa eneo la leseni yake kujumuisha maeneo ya Vijiji vilivyopo kandokando ya barabara vilivytajwa na Mheshimiwa Mbunge. Kampuni kutumia barabara hii haina maana kuwa maeneo ya barabara hiyo yanakuwa ni sehemu ya leseni yake kwani hata watumiaji wengine wanafanya hivyo.

(e) Barabara iliyotajwa ni kati ya barabara zinazosimamiwa na Mkoa chini ya *TANROADS*. Jukumu la kuiwekea lami barabara hiyo ni la Serikali na ghamraza za kuweka lami kwa kilomita moja ni hadi shilingi milioni 200/=. Hivyo kuiweka lami barabara ya Bulyankhulu mpaka Busoka yenye umbali wa kilometra 76 itagharimu kiasi cha shilingi bilioni 15.2/=. Kiasi hiki ni kikubwa, Serikali itaendelea na mpango wake wa kuboresha miundombinu na pale hali ya mapato itakaporuhusu barabara hii nayo itaboreshwa kwa kuwekewa lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

## HOJA ZA SERIKALI

### HOJA YA KUJADILI HOTUBA YA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHESHIMIWA BENJAMIN W. MKAPA

(*Majadiliano Yanaendelea*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mchangiaji wetu wa kwanza leo asubuhi naomba kueleza yafuatayo:-

Kwanza kuna idadi ya wachangiaji sasa imebakia kwenye 37. Hii ni idadi kubwa sana. Sasa ningependa kutoa ushauri ufuatao kama Waheshimiwa Wabunge mtaukubali basi itakuwa rahisi. Kwa sababu wote tuna nia ya kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Rais, ili kila mtu apate nafasi sasa nashauri mkikubali ni vizuri, kwamba wachangiaji wachukue dakika kumi, kumi. Tukipunguza zile shukrani, ahsante na hongera, ukipata dakika kumi za hoja nzito tunaweza kabisa kumaliza kuchangia haya. (*Makofi*)

Sawa, nadhani makofi haya yanaashiria kwamba tunakubaliana dakika kumi kumi. Naona wote tumekubaliana.

**WABUNGE FULANI:** Sawa.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, wachangiaji wa kwanza wa tatu ni hawa wafuatao, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare pia ajiandae.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** *Speaker's guidance.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tungeomba uelewa kwamba, je, ni utaratibu kubadilisha muda wa kuchangia hoja sawa na ambavyo labda inatokea kwenye semina, maana yake hili ni Bunge?

**NAIBU SPIKA:** Wewe unasemaje Mheshimiwa, unakubaliana na muda huo au hapana? Wewe mwenyewe unasemaje maana nimehoji wote sikuona mkono.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Nakubaliana sawa, lakini ilezwe rasmi na ikubalike Kikanuni ili tutengue Kanuni.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, hata kama unakubaliana, unasema tutengue Kanuni. Basi tutamtaka Waziri au wewe mwenyewe toa hoja ya kutengue Kanuni.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zinazelea wazi kukiwa na hoja, yoyote kati yenu anasimama, anaomba kutoa hoja, inaafigikiwa au haiafikiwi. Ndiyo maana nimesema kama unaona una tatizo toa hoja, tutengue Kanuni, tumalize kazi. Mheshimiwa Lwakatare.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Natengua Kanuni sasa kwa siku hii ya leo.

**NAIBU SPIKA:** Kanuni ya ngapi? (*Kicheko*)

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Hiyo hiyo ambayo hukutusomea wakati unatengua. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amekubali tuendelee. (*Makofit*)

Waheshimiwa Wabunge, kazi ya Spika ni kuongoza utaratibu bora na namna ya kuendesha, nikahoji wote mkaesema sawa, nikatazama, ndiyo maana nilikuwa naangalia macho hivi kuona nani asingependa hilo, kwa sababu jambo lenyewe ni jema kwamba kila mtu apate nafasi, basi nadhani ndiyo maana mlinikubalia kuwa wepesi. Sasa Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, endelea.

**MHE. CHARLES M. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuwa mchangiaji wa kwanza katika siku hii ya leo kuhusiana na hoja ya Serikali kuhusu kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na mabadiliko ambayo yametokea sasa hivi nimefanya uamuzi wa haraka, nitapunguza cha kuchangia lakini kwa kuwa nimerejea hivi karibuni naona pongezi sitozipunguza kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu bali nitapunguza uchangiaji na kwa sababu siku bado zipo *Inshallah* nina afya yangu nzuri nitaongea siku zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Mbunge wa *SADC*, Mheshimiwa Sophia Simba kwa kuchaguliwa kwake.

Naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Kamishna Asha Ngede wa Kamisheni ya Bunge. Pia kwa kuchaguliwa Wabunge wa Bunge la Afrika niwataje tu haraka haraka, Mheshimiwa Mama Balozi Getrude Ibengwe Mongella, Mheshimiwa Amani Warid Kabourou, Mheshimiwa Athuman Janguo, Mheshimiwa William Shija na bila kumsahau Mheshimiwa Remidius Edington Kissassi. Wote hawa nawapa pongezi kwa kuchaguliwa na Bunge lako Tukufu ili kuweza kutuwakilisha Wabunge na Taifa kwa ujumla katika maeneo hayo muhimu na nawatakia kila la kheri katika ufanisi wa shughuli zao. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawapongeza Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano kwa kuchaguliwa kuingia tena katika Bunge hilo. Kwa hesabu zangu nadhani zaidi ya nusu ya Wabunge waliokuja tena hapa walikuwepo. Karibu nusu lakini nadhani haipungui theluthi moja kuna Wabunge wengine ambaa ni wapya hao pia nawapa pongezi za dhati. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale ambaa tulikuwa nao pamoja mimi nilikuwepo humu ndani kwa kipindi cha kama miaka miwili hivi, nilikuwa Mbunge lakini kwa faida ya wale wapya naomba tu kutumia dakika moja au mbili kujitambulisha kwao maana katika siasa hakuna anayejulikana sana hata siku moja. Kwenu Waheshimiwa wapya mimi naitwa Charles Makongoro Nyerere, nilikuwa Mbunge katika Bunge hili kwa kipindi kilichopita kupitia Kambi ambayo katika lugha rasmi hapa ndani inaitwa Kambi ya Upinzani. Lakini mimi kimoyomoyo nasema ahaa, bwana wewe kumradhi, ndiyo Kambi iliyonipandisha chati.

Kwa hiyo, nilikuwa huku kwa Kambi iliyonipandisha chati kwa kipindi cha miaka miwili tukifanya kazi pamoja. Halafu baada ya miaka miwili kukatokea mvua zinaitwa mvua za *El-Nino*, mvua zile ziliharibu miundombinu ya Serikali zikasomba madaraja ya Serikali yakaenda, mifugo ya wananchi imekwenda, mimea ya wananchi ilikwenda na Ubunge wangu fyee, ukaenda. Leo zimekwisha nimerejea Inshallah namshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuungana na Mheshimiwa Richard Ndassa, kumtakia kheri na afya njema Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Bujiku Sakila, kwa ajili yake yeze binafsi, Taifa letu pamoja na wananchi wa Jimbo la Kwimba. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa pongezi za kipekee kwa ndugu yangu, rafiki yangu Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa huyu mtanisamehe tulikuwa naye kwenye Kambi iliyonipandisha chati mimi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo amerudi ana nafasi nzuri kweli kweli.

#### **WABUNGE FULANI:** Sasa unaionomba?

**MHE. CHARLES M. NYERERE:** Ahaa, siiombi, yeze ni kielelezo kizuri kuwa CCM hakina mizengwe wala ubaguzi. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wastaifu, wastaifu wana watoto wao na watoto wao wanaendelea kuzaa na wastaifu wapo katika maeneo mengi. Wapo waliostaafu Udiwani, Ubunge, Urais na kadhalika.

Mimi nikiwa nje nilikuwa nikiitwa Mbunge mstaaifu, naomba kutoa salaam za kipekee kwa Mheshimiwa Mbunge Dr. Hussein Mwinyi wa Mkuranga kwamba anatuwakilisha vizuri sana watoto wa wastaifu. Kwa sababu taarifa nilizonazo anapenda watu, ni mkarimu, ni mchapakazi na ni makini. Nasema kwa wale watoto wa wastaifu, Mheshimiwa Dr. Mwinyi, anatuonyesha mfano mzuri, namtakia kila la kheri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba kutoa pongezi kwa Baraza la Mawaziri. Wakati Mheshimiwa Rais anajiandaa kuunda Baraza hili la Mawaziri alisema kwamba ataunda kikosi cha askari wa miavuli. Nimeamini Baraza hili la Mawaziri kweli ni kikosi cha askari wa miavuli ambao wanatekeleza majukumu yao vizuri na wanamsaidia Mheshimiwa Rais vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba moja kwa moja kusema kwamba hotuba ya Rais naiunga mkono mia kwa mia. Naunga mkono Wabunge wote kama walivyochangia. Kwa kifupi na bila kujaribu kurejea yale ambayo wameyazungumza naweza kusema tu kwamba, Hotuba ya Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa inalindwa zaidi na vitendo vyta Serikali yake na ujumbe ambao naomba kusema tu kwamba kwa ndugu zetu ambao mpo karibu zaidi kutokana na kazi zenu mwambieni ujumbe wake kwamba kwa nini hatusemi, ujumbe umefika, mimi nitasema sana kila nikipata nafasi, nitakuwa makini, nitasema sana mafanikio ya Serikali ya Mheshimiwa Benjamin Mkapa kwa umakini mkubwa. (*Makofî*)

Kwa kifupi amani na utulivu katika nchi yetu vimeendelea kuendelezwa na ushahidi mzuri na pongezi nyingi tunatoa kwa muafaka uliopatikana baina ya Chama Tawala na CUF kule Zanzibar. Uboreshaji wa miundombinu unaonekana sipendi kurudia na Wabunge wameshashukuru lakini mfano mmoja ni daraja la Mto Rufiji. Leo nitakuwa sikosei kusema kwamba wafanyakazi wa Serikali, Serikali ya Mheshimiwa Benjamin Mkapa imewaongezea heshima, leo wafanyakazi wa Serikali ukilinganisha na kipindi fulani hapa nyuma, kutokana na hali yetu mbaya, sina Serikali ninayoilaumu huko nyuma, lakini nasema kutokana na hali yetu mbaya heshima ya mfanyakazi wa Serikali ilikuwa ndogo, lakini leo ukifika sehemu ya mapumziko ukamwambia mfanyakazi wa Serikali karibu soda na yeze anakwambia na wewe karibu chochote. Tofauti kidogo imeonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mashaka na wafanyakazi wa Mahakama kwamba hali yao bado ni mbaya. Nikipata nafasi nitazungumza lakini leo sasa nataka nizungumze hili moja tu kama mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Rais anazungumza na Bunge katika hotuba yake aligusia kwamba anasikitishwa na hali ya udhaifu wa Vyama vyta Upinzani kwamba Vyama vile yeye asingependa vitawale daima. Lakini inapokuwa Vyama hivi vyta Upinzani ni dhaifu sana anajisikia uchungu.

Kwa sababu udhaifu unapokuwa katika Upinzani kwa kiwango hicho basi ni sawasawa kwamba unakuwa ni mzaha na ule Upinzani haufanyi kazi ambayo ilikusudiwa katika nchi yoyote yenye Vyama vingi vyta Siasa. Mimi nina machache ya kuongeza.

Mheshimiwa Rais huko nyuma aliwahi kusema, wakawaambia yeye si kazi yake hiyo. Inawezekana kwa sababu hakuwepo lakini mimi nilikuwepo katika Kambi ya Upinzani, nitapitia tu maoni yangu ya kuweza kuchangia kwamba katika Kambi ya Upinzani mimi nina mashaka sana jinsi ambavyo Vyama vyta Upinzani vilivyo na Waheshimiwa Wabunge ndani ya Bunge ikiwa kama wanawaheshimu na kuwathamini kiasi gani Waheshimiwa Wabunge wao, hilo linanipa mashaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni uzoefu wangu kwamba Mbunge wa Chama cha Upinzani akishachaguliwa akaapishwa hapa, anaporejea kwenye Kambi yake kuna kusimangwa simangwa hivi na kuna kuoneana kijicho. Mbunge anatakiwa aheshimiwe na Mbunge anatakiwa atumwe kazi. Lakini kuna hali hiyo kwa Waheshimiwa Wabunge Wanawake anaporudi kule anaweza akakuta wanawake kwenye Chama anachokwenda wanamsimanga, wewe umeingiaje huku au wewe mbona unajidai.

Kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge wanaume nao pia wanaonekana wanasimangwa simangwa, mbona mnatudharau, vitu vyta namna hiyo. Katika muda mchache ambao tayari nimekuja katika Chama Tawala ninachowenza kusema ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wanaheshimiwa na ni vizuri Viongozi wa Vyama vyta Upinzani wakajifunza kuishi kwa kuheshimiana. Kwa sababu *let us be very serious*, kama wewe ni chama cha siasa umeandikishwa tu huna Mbunge Bungeni, sasa heshima yako iko?

Pili, kuna suala la ruzuku. Ruzuku mimi naamini sana kwamba Mbunge wa Upinzani anaihitaji zaidi kuliko Mbunge wa Chama Tawala kwa sababu Mbunge wa Chama Tawala wananchi wamekwishamkabidhi dhamana ya kuongoza nchi *infrastructure* iko naye. Mbunge wa Upinzani anahitaji hiyo ruzuku kwa sababu ndiyo anajijenga, unamnyima ruzuku anakwenda kule yuko hoihoi, akirudi kwenye Chama chake kuwaeleza viongozi wakuu kwamba nikumbukeni kwenye hii ruzuku ninahitaji, utadhani ameomba kazi ya kumpikia Mwenyezi Mungu chai. Wanamvinzia huyu, tunamngoja akosee, akikosea kidogo tu huyu wanamtuhumu kwamba natumiwa na CCM, mfukuze Chama akose Ubunge, huna Waheshimiwa Wabunge heshima yako iko wapi wewe Chama cha Upinzani? Kama huna Waheshimiwa Wabunge wamekaa humu Bungeni? (*Makof/Kicheko*)

Tatu, ni masuala ambayo huko nyuma yalikwishazungumza kuingiliana katika maeneo. Juzi mimi sikuwepo nilikuwa katika Elimu ya Watu Wazima nchi za nje, lakini nilikuwa nafuatalia uchaguzi mdogo uliokuwa ukifanyika visiwani. Ni vizuri tu Upinzani mkaamua kwamba ni afadhalii haya maeneo ya nchi nzima ukamwachia tembo. Tembo anapofanya shughuli zake si mambo yake makubwa? Waachieni CCM na lakini, nyie katika maeneo fulani fulani, ndugu zangu mimi nilikuwa huko, hakuna haja ya kuingiliana. Wenzetu wa *CUF* kule wanapofanya uchaguzi halafu unaona kuna Vyama vingine vimeingia ingia kule kule unaenda kufanya nini? Kule waachie *CUF*, waachie CCM na wao *CUF* nao wakija huku waambie kumradhi tuliwaachia kule.

Sasa mnajua mnapoanza kwenda kuwachokonoa chokonoa kule na wao watakuja kuwachokonoa chokonoa huko katika maeneo ambayo kwa kweli ni ya kwenu. Nisiwape maarifa? Lakini najaribu kumsaidia Mheshimiwa Rais kwa maana yeye walimwambia si kazi yake basi ngoja niifanye mimi hii kazi. (*Makof*)

Kuna jambo lingine la mwisho, kuna tabia ya Vyama vya Upinzani kuwatisha Wabunge wao kwamba wewe unajua bila sisi usingechaguliwa, naomba iwe ukweli na iwe bayana Mbunge wa Chama cha Upinzani anapokuja hapa au kwa Viti Maalum na hasa anapotokea kwenye Jimbo wewe kiongozi wangu ni mpiga debe tu walionileta hapa ni wapiga kura wananchi, tuwaheshimu wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba basi niseme yanatosha nisizidisha muda. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunitambua na kumipa nafasi hii na mimi niseme machache tu kuhusu Hotuba ya Mheshimiwa Rais Benjamina William Mkapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaingia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais na mimi naungana mkono na wenzangu walionitangulia kwa kuwapa pongezi wenzetu. Kwanza, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa hotuba yake fupi yenye mafundisho mazuri. Pili, pia natoa pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kwenda kutuwakilisha katika Bunge la Afrika na Mama Sophia Simba naye kwa kwenda kutuwakilisha katika *SADC*.

Sasa baada ya pongezi hizo nadhani kuwa niongelee tu machache kuhusu hotuba yenye ya Mheshimiwa Rais. Hotuba ya Mheshimiwa Rais Benjamina William Mkapa ilikuwa ndefu, lakini kila mmoja alitaka kuendelea kuisikiliza. Nadhani kuna wachache walioendelea kuisikiliza hata alipomaliza *speech*. Waliendelea kusikiliza hiyo *speech* inakwendaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nitayazungumzia machache tu yale ambayo naona kuwa ni ya muhimu kwangu mimi na kwa nchi yenye. Imebaki miezi 20 kumaliza kipindi hicho na yeye alisema kweli ndege ameishaiweka kwenye *runway* nadhani karibu iondoke na sisi tuliooko hapa alituomba Bunge lisaidie kuinua hiyo ndege iweze kupaa kuanza kusafiri mwendo mkali na itakuwa juu kuelekea huko. Mheshimiwa Rais alieleza mengi, lakini na mimi nimeyagawa katika makundi mawili tu. Zile huduma za jamii nitaziongelea kwa ufupi, halafu ya pili ni ya uchumi wenye kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za jamii ambazo aliziongelea Mheshimiwa Rais ilikuwa elimu, afya, maji, na barabara za vijiji. Alishaweka mikakati sasa kinachohitajika ni msukumo wa kuweka vitu hivyo viende haraka zaidi. Mbinu zimeishawekwa za kufanya msukumo huo na mengi yameongelewa kwenye elimu na kwenye afya. Lakini mimi nadhani kuwa nizungumzie hasa elimu. Elimu ndiyo msingi wa maendeleo na ufunguo wa kila mtu anayetaka kwenda mbele.

Sasa elimu iko ya *primary*, elimu iko ya sekondari halafu iko elimu ya juu. Kwa upande wangu nataka nisisitize kuwa elimu ya msingi imeshaundiwa utaratibu na inaendelea vizuri, lakini elimu ya sekondari nasikia inaundiwa utaratibu. Awali kabisa hizo mbili zioainishwe, idadi ya watu na *quality* pia ya elimu. Idadi ya watu ni rahisi kwa kujenga madarasa na kwa kujenga nyumba za walimu. Lakini kuoainisha kuwa *primary* iwe hivi, kiasi kadhaa na sekondari wapokee watoto kadhaa hiyo ndiyo inakuwa mambo ya mahesabu pale.

Sasa zamani ilikuwa ukishamaliza elimu ya sekondari mtu unapewa ajira, kwa hiyo, elimu yetu ilikuwa imejengeka kwa kuajiriwa, tulikuwa tunawaelimisha vijana na wakimaliza wanaajiriwa kufanya kazi. Lakini hali hiyo sasa haipo tena, ni elimu ya kujitegemea kufanya kazi wewe mwenyewe, kuajiri au kuajiri nyie wenye katiaka vikundi na kadhalika.

Kwa hiyo, hapo itabidi Serikali na sisi wote tuanze kufikiria upya. Kufikiria kuwa "A" ni silabi zile tulizokuwa nazo zitafaa kwa elimu kwa watoto watakaokwenda kujitegemea baada ya kumaliza elimu yao ambayo hiyo itakuwa jambo kubwa tulififikirie, na silabi zetu zitazamwe kuwa huyu akimaliza *primary* au sekondari anaenda kujitegemea. Hilo moja.

La pili, ni lazima tuongeze ule umri angalau kwa mwaka mmoja ikiwezekana kwa *primary*. Zamani *primary* ilienda mpaka *middle schools* ikaenda mpaka darasa la nane, miaka nane ya *schools*, siku hizi ni miaka saba. Sasa wale wanaotoka toka *primary* ni wadogo bado, sasa kujitegemea inakuwa

ngumu. Labda tungefikiri pia tuweze kuongeza mwaka iwe miaka minane ya *primary* ndipo twenda sekondari kama kawaida miaka 6, halafu Vyuo Vikuu. Nilidhani hiyo ndiyo moja ya silabi pamoja na kuongeza umri.

Halafu la tatu, muhimu kama kweli tutaenda kujitegemea itakuwa lazima tuongeze shule za ufundi. Maana baada ya sekondari watu waweze wengi zaidi kwenda katika shule za ufundi kuliko *University*, maana *University* tutawapangia wachache, hata Mheshimiwa Rais alitaja watu 55,000 baada ya miaka kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa mbinu kali sana tutafikia hiyo. Lakini tukiweza kujenga *Polytechnics* na *Institute za Technology* huenda hapo tutaweza kuwapa vijana wengi wakaenda huko na wakitoka huko watakuwa katika hali ya kuweza kujitegemea zaidi kuliko wangekuwa waende Chuo Kikuu. Wale watakaoenda Chuo Kikuu baadhi waende wakaendelea huko, lakini wengi watakaobaki tungejaribu kuwapeleka ndani ya *Poly-Technics* au *Technical Institute* na *Institute* tunazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa nazo nyangi wakati wa miaka 1970 na 1980, karibu kila sekta na *sub-sector* ilikuwa na shule hapa Tanzania na tulionewa wivu na Afrika nzima. Kwa sababu sehemu ulipokuwa umeme kulikuwa na shule inaendesha na *TANESCO* ya kuwafanya wale vijana wajifunze umeme. Sukari walikuwa na shule ya sukari.

Halafu kila *sub-sector* kulikuwa na shule yake, lakini hizo zimeanza kuffia sasa hivi na nyininge zinaanza kuwa *University* zile *Institute* za kujifunza utaalamu zinageuka kuwa *University*, Ardhi imekuwa *University*. Halafu *IFM* nasikia watakuwa *University*, Mzumbe ni *University*. Kwa hiyo, zile shule ambazo zilikuwa zinatoa maarifa ya kufanya kujitegemea zimefutika. Lakini tusifikirie tena upya ili tuweze kuwa na vijana wanaomaliza masomo na wanaweza kujitegemea. Nilidhani niongelee elimu hapo tu.

Kwa upande wa uchumi nilikuwa na hadithi ndefu, lakini baada ya kupunguziwa zile dakika tano nitasema kwa kifupi tu. Kuna mawili. Uchumi wetu kwa kweli ni uchumi mzuri Tanzania siyo maskini. Tanzania ni tajiri sana, lakini Watanzania ndiyo maskini. Kwa kwa kuwa Tanzania ina kila kitu, ina ardhi, maji tele, maziwa na mito na ina maliasili nyangi kutoka kwenye misitu, samaki, wanyamapori, ina kila aina ya madini yaliyoko ulimwenguni yapo hapa Tanzania. Tuna kilimo cha kuweza kulima mazao ya temperate na mazao ya *tropical* yote tunaweza kuyalima katika hali yetu ya hewa hapa. Tanzania pia ina mifugo ya aina zote. Halafu mwisho ina watu wengi sasa hivi tuko milioni 35 tunaendea milioni 40, kwa hiyo, tungeweza kuondoka na sera zetu ni za kuigwa na nchi nyangi za Afrika. Lakini sasa bado sisi wenywewe kufikiria tufanye nini ili utajiri huu uibuke tuwe matajiri watu, watu tusiwe maskini, tuwe nasi matajiri pia, siyo nchi iwe tayari watu wake wawe maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, umaskini wetu umeanzia tangu ukoloni kwa sababu tulikuwa tumepanwa. Wakati ule Mzungu alikuwa anachukua *the best* katika *cream* ya uchumi. Halafu walifuata wenzetu wa Asia waliokuwa hapa walikuwa wakifanya biashara na sisi tulizuiwa kufanya lolote la kiuchumi la kuijiendeleza hata kwenye mabenki kulikuwa na sheria zinamzuia Mwfrika kukopa fedha au kupewa fedha ya mkopo toka katika mabenki. Baada ya hapo tukawa tumeletwa kwenye biashara ya kilimo, kilimo tulilingizwa tu sehemu ile ya *modern agriculture* ambayo iliunganishwa na uchumi wa Ulaya. Hao nchi jirani yaani kwa Kiingereza tunasema sisi tukawa tumepangwa *ku-produce what we don't consume and consume what we don't produce*. Hiyo ndiyo hali iliyokuwepo, baada ya hapo tumeendelea kuwa hivyo mpaka sasa, tukaenda ku-graduate kuwa na uchumi tegemezi. Kwa hiyo, katika hilo inatubidi tufanye juhudii na bidii ya kujitengenezea utaratibu wa kwenda juu kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofsi*)

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hotuba ya Mheshimiwa Rais mimi naipongeza kwa sababu moja tu kubwa kwamba ametupa mahali pa kuanzia kama mwanasiasa. Mwanasiasa ye yote yule anapenda zaidi

azungumzwe au watu wajadili amezungumza nini ili kuwepo muendelezo wa lile analotaka kulizungumza au lile analotaka kulifanya au kuendeleza yale ambayo anaamini anataka yafanyike.

Mheshimiwa Rais alitumia mifano ya walevi ndani ya hotuba yake na mimi ninavyofahamu walevi ukiacha kando wanywaji ni kwamba huwa wana tabia moja kubwa, kwamba mlevi kawaida anamwona mwenzake ndiyo ameleta, yeche anajiona bado hajaelewa. Sasa mimi kitu kimoja ambacho nimejifunza ambacho kinaendana na hali halisi ni kwamba Mheshimiwa Rais anahitaji *speed* kali ndani ya muda wa miezi 20 iliyobaki akiwa kama Mheshimiwa Rais anataka tupande ndege na ndege iruke. Lakini mimi kwa mwendo tunaokwenda nao, naamini kuna hatari ya Mheshimiwa Rais sijui yeche ndiyo *pilot* kule mbele na amepitia mlango wa ma-*pilot* akaja kujikuta ameondoka na ndege haina mtu kule nyuma. (*Makofi*)

Kama tunataka kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu inabidi tumueleza ukweli wala siyo lazima tutumie hotuba yake kushangilia yale aliyyoyazungumza. Kwa bahati mbaya Mheshimiwa Rais yuko hatua 100 mbele, lakini naamini wanaomsaidia walio wengi wako hatua 60 nyuma. Nazungumza hivyo kwa sababu na ni bahati mbaya kwamba Mheshimiwa Rais hivi sasa anaumwa, kuumwa kwake kunamfanya asisafiri au asifuatilie taarifa ambazo anafikishiwa na wasaidizi wake wa karibu.

Kwa hiyo, nafasi ya kudanganywa ni kubwa, nafasi ya kuja kusoma takwimu na kuamini takwimu ni kubwa, lakini ile hali halisi inaweza ikakosekana kwa yale anayoelezwa. Hii naizungumza ni mifano midogo tu, tutasikia taarifa nzuri kwamba chakula kinagaiwa Wilayani, sehemu zenye maafa ya njaa, chakula kingi kinaingizwa na wafanyabiashara, lakini watu wanaendelea kula mizizi, watu wanaendelea kufa njaa na watu wataendelea kupata taabu. Ni kwa sababu Mheshimiwa Rais naamini ndege imeishaondoka na wote tuko ndani ya ndege. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna usemi wa Kifaransa wanasema: “*Atagenda ati mae achuba.*” Kwa tafsiri nyepesi ni kwamba, jambo usilolijua ni kama usiku wa kiza. Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ukurasa 67 amezungumzia nchi ndogo ya Dominika ambayo eneo lake ni asilimia tano ya eneo la Tanzania na yenye watu milioni 8.7 anasema watu wale wana kasi ya ajabu katika maendeleo.

Mimi nasema Mheshimiwa Rais asishangae kuelea kwa meli na shilingi kuzama. Hawa watu wa Dominika wanafanya kazi kweli kweli hawaendi na blaa blaa. Sasa sisi tunaposifia mambo aliyozungumza Mheshimiwa Rais, sisi tunasema Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya kazi nzuri kama alivyosema inabidi tujisifie.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nasema haitoshi. Huwezi kujilinganisha kwamba unajua kukimbia ukajilinganisha na mtoto wa miaka 10, wewe ukasema kwamba unajua kukimbia au wale warembo wetu wanaokwenda kwenye mashindano tukiwa *Diamond Jubilee* pale anaibuka akiwa mshindi na tunawashangilia na anapata zawadi na tunzo mbalimbali. Akienda huko China anakuwa mshindi wa mwisho. Sasa ndiyo mchezo tunaocheza hapa Tanzania. Tunajiona tunafanya kazi kweli kweli na tunapata kweli kweli, lakini *at the end of the day* ni kwamba sisi ni viwete tu tunajilinganisha sisi wenye, hatuna uwezo wa kukimbia, hatujilinganishi na wale wanaoweza. Mimi nasema tubadilishe *style* ya kujilinganisha, tujilinganishe na wale waliofanya vizuri. Dominika imekuwaje wakainua uchumi wao kwa kasi sana. Nchi ambazo tumepata Uhuru katika kipindi kimoja zimekuwaje zikabadili uchumi wao, wale ndiyo wa kujilinganisha nao, lakini tusije hapa tunajilinganisha tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napitia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatisha kabisa mabilioni ya fedha ambayo yanapotea yanatisha, na wakati huo huo Wizara zinakuja kila mwaka kuomba fedha, na hapo hapo Mheshimiwa Rais anasifia kwamba *TRA* wanakusanya mapato sana. Sasa kukusanya kwenye pakacha ambalo tunajua linavunja. Mimi sioni sababu ya kusifia *TRA* kwamba wanakusanya mapato vizuri na Mheshimiwa Rais anawasifia kwamba wanakusanya mapato vizuri kumbe tunakusanya kwenye pakacha ambalo linavunja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependekeza kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anafanya kazi yake vizuri kama Mheshimiwa Rais anaheshimu taarifa anzopelekewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali tuweke Azimio kabisa kila Wizara ambayo itakuwa na *shot* kila

Wizara zinapokuja kwenye Bunge hili kuomba kuidhinishiwa makadirio ya bajeti zao zisipitishwe mpaka Mheshimiwa Waziri mhusika aeleze fedha zimekwenda wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la rushwa Mheshimiwa Rais amelikwepa hakulizingumzia kabisa na nasikitika kwamba kati ya sifa iliyomfanya Mheshimiwa Rais achaguliwe na Marehemu Baba wa Taifa ampigie debe na kumfagilia ni suala la kupambana na rushwa. Mheshimiwa Rais amebakiza miezi 20, miezi 20 tunajiuliza kwa *speed* hiyo ya ndege yake rushwa hii atawea kucheza nayo! Rushwa anaisemaje ana ubavu wa kupambana na wala rushwa. Sisi tunasubiri miezi 20 ipite tutamuuliza na hata huyo ambaye atakuwa anapitisha kumpigia debe na kumfagilia awe Rais tutamuuliza mzee kwa muda wa miaka 10 ile ahadi ambayo wewe ndiyo iliyokufanya uchaguliwe kuwa Rais kwamba wewe utapambana na rushwa imekuwaje na umepambana na rushwa kwa kiasi gani? Mheshimiwa Rais ajiandae kujibu swali hilo wakati atakapokuwa anamnadi huyo mgombea atakayechukua nafasi yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia na suala la udhaifu wa Vyama vya Upinzani. Katika ukurasa wa 33 wa hotuba yake Mheshimiwa Rais amesema kwamba njia pekee ya kufikia malengo ya maendeleo ya Milenia inahitajika utashi wa kisiasa na Utawala Bora katika nchi maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya Chama Tawala na Serikali yake hawana utashi wa kisiasa wa kuruhusu Mfumo wa Vyama Vingi, hawana na kama utashi haupo Upinzani lazima udhoofike na huu utashi unatokana na dhamira, lazima tukubali kwamba kama tunataka Mfumo wa Vyama Vingi, lazima na Taasisi na vyombo vinavyopaswa kutengeneza mazingira ya Upinzani hufanye kazi lazima tuviondolee udhaifu. Ukiwa na Bunge ambalo halihitaji Mfumo wa Vyama Vingi au Vyama Vingi viweze kufanya kazi lazima utakuta maamuzi yake yako *against* Upinzani. Hila zitatumika kuwa na taratibu na kanuni ambazo kamwe hazitaruhusu upinzani hufanye kazi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kama tunataka kuupata upinzani amba ni madhubuti lazima turekebishe hata Taasisi zetu. Taasisi zetu bado ni dhaifu Mheshimiwa Rais anakimbilia kwa kuangalia Vyama vya Upinzani kwamba ni udhaifu. Lakini hata Taasisi zetu bado ni dhaifu kabisa hazina mazingira ya kuweza kuruhusu Upinzani. Wengine wakimwona Wilfred Lwakatire ni Mpinzani wanafikiri kwamba wamekutana na jini kubwa. Kwa hiyo, sasa udhaifu uko hata ndani ya Chama Tawala, bado ni wadhaifu wa mfumo wenyewe wa Vyama vingi, kwa hiyo marekebisho yanahitajika. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais Mwai Kibaki nilipata bahati ya kukutana naye na alizungumza na sisi kama viongozi wa Upinzani. Alizungumza kitu kimoja ambacho nakikumbuka mpaka leo alisema: "Ninyi Wapinzani kama mnataka kufanikiwa inabidi muendeshe siasa kwa kufuata hali halisi ya mazingira yenu." Sisi upinzani pamoja na Mheshimiwa Rais kuntuona kwamba ni dhaifu, mimi naamini upinzani sasa ndiyo unaimarika. Mheshimiwa Rais anashindwa kuelewa kitu kimoja kwamba unapozungumzia upinzani usiangalie Vyama vya siasa ni pamoja na jamii yenye. Sasa hivi jamii ya Watanzania iliyo kubwa iko kwenye *Opposition*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namaliza kwa kusema kwamba nakubaliana na maneno ya mtu mmoja aliyeniambia kwamba: "Chama cha Mapinduzi kama unazungumza nao wakikwambia tukutane Mwanza, usiwasubiri Mwanza, wasubiri Mtwara." Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia kidogo kuhusu hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami nitoe pongezi kwa mpigo kwa wote waliochaguliwa katika nafasi mbalimbali na kadhalika. Ningependa kutoa pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Rais kwa kutoa hotuba ambayo ni *very powerful, comprehensive* na *authoritative*. Hotuba ya Mheshimiwa Rais sisi wengine wenye macho na masikio imetufungua kabisa, lakini kwa wale wasioona kama rafiki yangu basi tuwaache tu waendelee kutokuona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yamekwishazungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Naunga mkono wale wote waliotutakia mema na walioona hasa hasa umuhimu wa hotuba hii. Lakini

siungani mkono na wale ambao hawana masikio wala hawana macho ya kuona yale yanatokea katika nchi hii. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wangu nilikuwa na mambo mengi ya kuzungumza, lakini naona sasa kutokana na muda niya-*limit* sana sana.

Nataka kusema tu kwamba kama kungelikuwa kuna maeneo matano unaombwa mtu uchague unayoyaona hasa hasa yameleta mabadiliko makubwa katika nchi yetu, kutokana na Hotuba ya Mheshimiwa Rais ningesema kwamba la kwanza ni ujenzi wa miundombinu ya barabara ambao mimi nasema mipango ya namna hii haijawahi kutokeea. Haijawahi kutokeea kwa sababu tatizo wenzetu wa Wizara ya Ujenzi waliliona.

Baada ya kuona tatizo wakaja na mpango kamambe wakaiomba Serikali itenye fedha, wakaomba fedha kutoka nje zikaja na sasa wanaleta mapinduzi makubwa kutoka Mtwara mpaka Mwanza. Kazi zinakwenda vizuri na sote ni mashahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa elimu nao umeleta mapinduzi makubwa katika Elimu ya Msingi na hatimaye Sekondari na hivi sasa wakati nikizungumza, mimi nazungumza kwa furaha kwa sababu Mkoa wangu wa Mtwara kwa mara ya kwanza katika historia, umekuwa ni Mkoa wa pili kwa kufaulisha hawa watoto wa darasa la saba Tanzania na Wilaya yangu katika Mkoa wa Mtwara imekuwa Wilaya ya kwanza katika kufaulisha watoto wa darasa la saba na Kitaifa tumekuwa wa 14. Kwa hiyo, unaweza ukaona hiyo tofauti yangu mimi na wale wasio na macho. Unaweza ukaona, maana yake ni nini, maana ya mabadiliko katika mipango hii.

Tatu, ukiingia kwenye mipango ya afya kwa kweli nako kuna mambo mengi yanayofanyika. Mabadiliko ya utoaji wa huduma za afya katika *Public Health Sector Reform*, Bima za Afya, Bima au Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*Community Development Health Fund*). Hayo ni mambo ambayo yanaleta mabadiliko makubwa katika nchi hii na kuwafanya watu waweze kupata huduma za afya kwa ukaribu zaidi.

Nne, niseme tu kuhusu ukusanyaji wa mapato unaofanywa na *TRA*, kuwa ni jambo kubwa, la mapinduzi na hivi sasa tuna fedha za kutosha za kuweza kuendeleza mipango yetu wenyewe na pia wakati huo huo kuna usimamizi unaoridhisha wa matumizi mbalimbali ya Serikali na sehemu nyingine. Nisingependa kwenda mahali alikokwenda mwenzangu aliyeondoka sasa hivi kwamba, mabilioni na mabilioni yamepotea. Katika utaratibu wowote wa uendeshaji lazima uwepo upungufu ndiyo maana katika *balance sheet* kuna mapato na matumizi. Sasa kwa vyovypote vile kunaweza kuwa na hitilafu ya hapa na pale, haya ni mambo ya kawaida hayatukatishi tamaa. Kila wakati tunachojitahidi ni kuhakikisha kwamba, hayo tunayadhibiti na kadri inavyoendelea sasa hivi hatuna wasi wasi.

Tano, mipango ya mawasiliano ambayo imeunganisha mitandao nchi nzima na sasa hivi tunaweza kuongea kila mahali kwa uhakika bila matatizo. Mafanikio ya aina hiyo hayakosi matatizo. Katika matatizo tumeweza kuona tu kwa upesi upesi kwa kweli niseme kiuwazi kwamba, katika sekta yetu upande wa nishati hapa inaonekana kabisa tumekwama. Tunakwama kwa sababu hali ya upatikanaji wa umeme nchini si ya kuridhisha. Hili tunalisema ili wahusika katika maeneo haya waweze kujizatiti zaidi kuona jinsi gani wanaweza kuboresha sekta zao ili waendane sawa na yale yaliyosemwa na Rais.

Wenzetu wa nishati toka siku nyingi tumewaambia kwamba, jamani vyanzo vyta umeme katika nchi hii ni vingi sana. Ingekuwa toka miaka ya 1970 wamesikia ushauri wetu wa kutumia gesi ya Songo Songo, wa kutumia mkaa wa mawe ya Mchuchuma, wa kutumia maji ya *Stigler's Gorge*, leo nchi hii ingekuwa *ina-export* umeme sio kutegemea kutoka sehemu nyingine. Kwa hiyo, nawaomba wenzangu walione hili kuwa ni tatizo walilomjengea Rais na wajitahidi sana kusahihisha ili twende na wakati, umeme uweze kupatikana kila sehemu nchini.

Halafu pia kuna sehemu nyingine katika sekta kiongozi ya kilimo. Jamani mpaka hivi sasa jembe la mkulima lile la zamani babu zangu walilokuwa wanalimia mpaka leo wanalimia, sasa haya mambo yatakwenda mpaka lini? Ni sawa ukiangalia mifano Mheshimiwa Rais alitoa mingi, lakini mimi nitoe

mfano mmoja tu. Kuna mlevi mmoja wakati anakuja Dodoma kabla hajaingia Dodoma akaangalia nyumba za Dodoma akasema moyoni, jamani Dodoma kuna mashamba mengi sana na mashamba hayo aliyoyaona huyu mlevi eti zile nyumba za Wagogo ambazo wanaweka udongo juu kumeota nyasi labda wengine wameweka karanga na kadhalika. Yeye alifikiri ni mashamba mengi. Sasa huo ndio ulikuwa upeo wake huyu mlevi kuona kwamba, Dodoma kuna mashamba mengi kwenye mapaa.

Sasa mimi nawaomba wenzetu wa kilimo nilivyowaambia pale kwamba askari wa miamvuli washuke kwa taratibu, washuke vizuri ardhini wasiendelee kushuka na kukaa katika mapaa ya Wagogo kuona kwamba mashamba yapo ya kutosha, hapana. Wakishuka chini watakuta maji mengi yanatiririka kwenda baharini hayatumwi.

Mito mikubwa mingi Ruvuma, Matandu, Malagarasi, maji haya yote yangeweza kuchukuliwa ili kuhakikisha kwamba, nchi hii inakuwa na maji ya kutosha ya kunywesha kwenye mashamba yetu. Lakini mkikaa kama mnanning'inia katika nyumba za Wagogo, itakuwa balaa. (*Makofi*)

### **WABUNGE FULANI: Ehee!!!**

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Hapana Wagogo ni mfano tu. Mimi ningeomba sana kwamba kwa kuwa Rais amehutubia hii mara ya pili na mara ya kwanza aliwaita wenzetu kwamba ni askari wa miamvuli na kweli kwa wale askari wa miamvuli waliochapa kazi, tumeshaziona kazi zao zinapendeza kabisa. Lakini wale wanaoning'inia katika nyaya au katika mapaa ya nyumba nao wajitahidi sana washuke ili twende kwa pamoja katika kuhakikisha tunaleta mabadiliko makubwa katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa niseme tu kwamba, mimi naunga mkono hoja, naomba na wenzangu wateremke kutoka kwenye mapaa ya nyumba.

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika Hotuba hii ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa Hotuba yake nzuri, ambayo kila mtu anaikubali isipokuwa sasa inabidi kutumia wajibu wa kupinga pinga ili uwe Mpinzani kweli. Lakini kwa ujumla Hotuba hiyo ni nzuri kila mtu ameielewaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza na suala la rushwa. Kwa haraka haraka sababu muda umepunguzwa, kwa mtu ambaye ana macho anaona ni kwa namna gani Serikali inachukua hatua ya kudhibiti rushwa kwa kiwango kikubwa sana. Ninayo mifano michache, Taasisi ya Kuzuia Rushwa imuboreshwa hivi sasa kila Wilaya iko Ofisi ya Rushwa. Lakini sasa hivi nchi yetu mambo yake yanaonyeshwa kwa uwazi ili kila mtu aweze kuona nini kinafanyika. Kufanya mambo kwa siri siri ndio kunasababisha rushwa. Sasa hivi kila jambo lipo kwa uwazi maana yake ni namna moja nyingine ya kuzuia mianya ya rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale nyuma ilikuwa kila Wizara ina malalamiko ya rushwa na ziko Wizara ambazo zilikuwa ni kama viongozi kwa malalamiko kuhusu rushwa. Lakini leo katika Wizara ya Afya malalamiko yamepungua, Wizara ya Maliasili na Utalii malalamiko yamepungua namna hiyo. Juzi tu tulikuwa tuna kazi ya kugawa chakula cha njaa, pale tungekuwa tunasikia tu Waziri mahindi ameuza, Waziri amefanya hivi, lakini hakuna. Kipindi kigumu Waziri Mkuu na Ofisi yake imesimamia ugawaji wa chakula bila kusikia minong'ono ya rushwa, hii ni ushahidi kwamba, rushwa katika nchi yetu imepungua kwa kasi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze katika masuala mengine mawili ya uwekezaji na uwezeshaji. Nianze na la uwekezaji. Mheshimiwa Rais amekiri kwamba, maeneo machache tu ya nchi yetu ndiyo yanao hao wawekezaji na maeneo mengine wawekezaji hakuna. Maana tuijulize kwa sababu gani wang'ang'anie kukaa sehemu moja. Jibu ni kwamba, wanafuata miundombinu mizuri. Katika eneo hili naomba nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kukamilisha ujenzi wa daraja la Mto Rufiji. Lakini vile vile kwa kazi ambayo sasa hivi inaendelea ya ujenzi wa barabara kutoka Lindi mpaka Somanga.

Ninashukuru sana kwa sababu hii ni njia rahisi, wanatujengea uwezo sisi watu wa Lindi wenyewe kujiendeleza hii njia tukiitumia vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini liko tatizo lingine la umeme. Mwekezaji hawezi kuwekeza sehemu ambayo haina umeme. Mheshimiwa Rais amesema kwamba, tujitahidi kuvutia wawekezaji. Lakini unapopata mwekezaji Lindi unamwambia aje awekeze kwa miundombinu gani; je, kuna umeme, anasema sio wa uhakika. Je, sisi wa Kusini hatumo kwenye mpango huo wa uwekezaji na kama tumo kwa vivutio gani? Nilikuwa naomba sana Serikali ijtihadi kutuhakikishia watu wa Kusini tunapata umeme wa uhakika. Labda nimshukuru katika hili Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa jitihada zake za kutuondolea kero ya maji katika Mji wa Lindi. Tunamshukuru sana yeche na Serikali kwa ujumla wake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu uwezeshaji, wananchi kuwezesha kufanya biashara. Hivi leo iko mifuko ya mikopo ya akinamama na vijana. Lakini mifuko hii ni midogo sana katika Wilaya moja imepewa shilingi milioni moja, shilingi laki tano, sasa utakuta wanaopewa ni wachache sana na kiwango kidogo cha mkopo wanachopewa. Mtu anakopa shilingi laki moja hawezi kufanya biashara nzuri ya maendeleo kwa shilingi laki moja. Juzi Waziri wa Fedha amekiri hapa kwamba, yeche fedha anazo na kama hana sheria inamruhusu kukopa. Nilikuwa natoa rai kwamba, Serikali ifanye uamuzi wa makusudi, itafute walau shilingi 21 bilioni tutoe kila Mkoa shilingi bilioni moja ili watu hao kweli tuwakopeshe fedha za maana. Mtu akipewa mkopo wa shilingi milioni 2 au 3 ana uwezo mkubwa wa kufanya biashara kuliko shilingi laki moja au mbili. Watu wawezeshwe kupitia Mabenki, riba ni kubwa sana watu wengi hawawezi. Kwa hiyo, nashauri Serikali iongeze kwa kiasi kikubwa, uwezo wa Halmashauri wa kukopesha wananchi na kuwapatia fedha nyingi za kutosha.

Lakini vile vile viongozi wa kisiasa kule Mikoani, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, watilie mkazo mkubwa katika uanzishaji wa *SACCOS* na ikiwezekana basi wapimwe kwa mafanikio yao katika hili. Nadhani tukifanya hivyo, tunaweza kabisa kuwawezesa wananchi wetu kufanya biashara. Lakini leo kwa kiwango hiki cha sasa hivi cha mikopo, hawawezi kufanya biashara yoyote ya kuwaendeleza. Tutakuwa tunakopa fedha lakini hawawezi kulipa kwa sababu ni viwango vidogo ambavyo havizunguki na kupata faida kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vile vile nitumie nafasi hii kuupongeza mpango wa MMEM na MEMKWA. Kila mtu mwenye macho ameona mabadiliko makubwa kabisa katika mashule yetu kuanzia majengo, walimu na vitendea kazi. Lakini unapoimarisha Shule za Msingi maana yake unataka watoto wengi wafaulu waende Sekondari. Lakini kwa umaskini wetu ndani ya nchi yetu, wako wazee wengi ambaao watoto wao wanashindwa kusoma Sekondari kwa sababu ya uwezo wao mdogo au umaskini wao. Taratibu za kuwasaidia ambaao hawana uwezo haziko wazi sana, watu wengi hawazielewi. Nadhani Serikali iangalie namna gani itasaidia kuwafanya watoto ambaao wamefaulu lakini wazazi wao hawana uwezo waendelee kupata elimu. Vinginevyo itakuwa watoto wengi wanafaulu lakini wanashindwa kwenda Sekondari na kubakia pale pale na Elimu ya Msingi. Naomba sana Serikali ione ni kwa namna gani tunaweza kuwasaidia hawa watu ambaao hawana uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fursa ambazo nchi hii inazo za biashara kama vile *AGOA* na *EBAG*, si watu wengi wanaolewa fursa hizi zikoje, wanatakiwa wafanye nini. Ni mambo ambayo yako vitabuni, unasikia redioni, lakini bado hatujapata elimu ya kutosha kwamba Watanzania sasa hivi mnayo fursa moja, mbili, tatu. Watu wengi hawalielewi hilo. Kwa hiyo, natoa rai kama ikiwezekana, Serikali iiwezeshe Taasisi ile ya Biashara (*TCCIA*) katika vyombo vyaya habari ili viweze kutoa ufanuzi wa kina na kuwaeleza wananchi waelewe ili na sisi tuweze kutumia fursa hizi vizuri kwa ajili ya sisi wenyewe na nchi yetu kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ni kuhusu Daftari la Wapiga Kura. Nimesikia katika vyombo vyaya habari kwamba, Zanzibar kumeanza chokochoko ya watu kuanza kufukuzana na kuondoana, kutishiana maisha kwa sababu tu mtu ametoka upande mmoja wa Muungano. Naomba nitoe rai kwa Serikali kwamba, suala hili ilichukulie hatua za haraka sana. Inadaiwa kwamba ni njama ya CCM, lakini CCM haiwezi kufanya hivyo. Kwa sababu malalamiko hayo mengi ni kwamba, CCM inachukua watu Bara kuja huku ndiyo inashinda. Kwa hiyo, wao ndio wanawaondoa watu wa CCM. Lakini wajue

kwamba, mionganini mwao Viongozi wao Wakuu nao ni wa Bara huku huku, waanze na hao kwanza. Viongozi wao Wakuu kwenye vyama hivyo hivyo wengine wanatokea Bara huku, wangeanza kwanza wa Kisiju kabla ya hao wa kwetu sisi. Lakini nasema ni hatari kwa sababu tutafika mahali tutashindwa kuelewana hao walioko huku wako kidogo kuliko walioko huku. Naomba vyama vya siasa vitulie, tutumie fursa hii vizuri bila ugomvi wala kuzusha chuki. Lakini nasema chama cha wenzetu hawa kimezoea ugomvi. Tunakuombeni katika hili Daftari la Wapiga Kura na kufukuzwa watu, Mheshimiwa Karim, huna nguvu. Si tabia nzuri na haitoi sura nzuri kwa Muafaka wetu wa CCM na CUF. (*Makofsi*)

Naiomba Serikali ichukue hatua za haraka sana. Zanzibar ni ndogo sana, mkianza kupigana Zanzibar ni siku tatu watu wamekwisha pale. Nasema tuache Serikali ifanye zoezi lake vizuri, sote ni Watanzania. Amekaa mtu pale Unguja miaka 30 au 40 unamwambia sio kwako, kwao ni wapi sasa? Mkianza hivyo watu wote pale si kwao, wengine ni Wangazija kwa Comoro watoke wao kwanza vile vile. Kuna wengine Wadigo na kadhalika lakini ni Wazanzibari sasa hivi. Nasema naiomba Serikali ichukue hatua za haraka kabla hali haijawa mbaya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofsi*)

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyosema, kwa kweli sitarudia kushukuru lakini niseme tu kwamba, kwa kweli Hotuba ya Rais ni kama alivyosema Spika, kipimo chake kwa kipindi cha uongozi wake hakipo, ndiyo amekiweka juzi.

Napenda nianze kwa kunukuu yale ambayo ameyasema Mheshimiwa Rais. Katika ukurasa wa 14, Rais amesema: "Lakini Mheshimiwa Spika, uchumi wa soko lazima udhibitiwe kwa maslahi ya Taifa na walaji. Ili kuwalinda wateja na kuhakikisha kunakuwa na ushindani wa haki kwenye biashara, Serikali immeanzisha Mashirika". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeanzia hapa kwa sababu ninaamini sasa tunafuata uchumi huru, uchumi wa soko. Uchumi wa soko au uchumi wa kijamaa ni utaratibu, kama mzungumzaji jana mmoja alivyosema kuhusu *Leninism* na *Maxism*. Ni lazima kuwepo na *rules of the game*, kanuni za mchezo wenye. Sasa mchezo wa soko huria kitu kikubwa kinachoweza kudhibiti na *ku-regulate* uchumi huo ni kuweka utaratibu wa udhibiti. Nchi yetu ilitangaza uchumi wa soko huria mwaka 1984. Hivi sasa ni miaka 20 inaeleweka wazi kabisa kwamba, kwa kuzingatia Mashirika ya Udhibiti yaliyoanzishwa na ukiangalia yale aliyotaja na mengine hayaanza, mimi napenda kutamka kwamba, matunda yote ya kazi nzuri ambayo tumeifanya kwa kipindi cha uongozi wa Rais kama haikudhibitiwa kwa kuweka Mashirika ya Udhibiti itatuletea kero huko siku za usoni.

Ubepari ni unyama na kwa sababu ubepari ni unyama ni lazima uwe *regulated*. Usipo u-*regulate* aliye na uwezo atamwumiza asiye na uwezo. Sasa hivi leo tunazungumzia tatizo lililopo ambalo linahitaji *regulator* ambaye hayupo. *EURA* tulisema iundwe miaka mitatu iliyopita mpaka leo haijaundwa. Bei ya mafuta kwa sasa ni karibu shilingi 800/=, hakuna mtu ambaye haelewi madhara ya kupanda kwa bei ya mafuta katika uchumi wa nchi ye yeyote ile. Ukishapandisha mafuta ina maana kila kitu kitapanda gharama zake na maisha yatakuwa magumu sana.

Sasa tulikwishaunda Shirika linaloitwa *EURA*, ambalo lingesimamia udhibiti lakini mpaka leo halijaanza. Sasa hawa maaskari wa miamvuli nawaomba twende kwa kanuni za mchezo, tusipofuata kanuni hizo wananchi wetu watateseka kwa sababu ni ukweli kwamba, mahali ambapo uchumi huria au uchumi wa soko mdogo ataumizwa na mkubwa. Kwa hiyo, nashauri sana Serikali katika hili kwamba, udhibiti katika miaka 20 iliyopita bado haujakuwepo. Kuna vipenyo vingi sana vya hawa matajiri kuwaumiza watu maskini. Sasa naiomba Serikali izidishe kasi katika udhibiti. Hilo la kwanza.

La pili, Rais amezungumzia katika ukurasa wa 12 anasema: "Jambo lingine ambalo nitalitilia mkazo katika kipindi changu kilichobaki ni mabadiliko ya fikra za viongozi na watendaji wa Serikali pamoja na Serikali za Mitaa kuhusu nafasi ya sekta binafsi". Hawa watendaji kazi katika Serikali za Mitaa na Serikali Kuu ni kama *Air Hostess* kwenye ndege ya Rais. Hawa ndio wanaopaswa kuhudumia ndani ya ndege hiyo. Kama hawataelewa wajibu wao basi mimi nina wasi wasi sana *take off landing* ya ndege hata huko angani kutakuwa na mawimbi makubwa na mawimbi yanayoweza kutokea kama hayo niliyokuwa

nayazungumzia kwamba, kama hakuna udhibiti kutakuwa na matatizo. Sasa bado lipo tatizo la kubadilisha fikra za watendaji. Hili ni tatizo kubwa na tatizo hili kwa kweli mara nyingi hatuwezi kuwalamu sana kwa sababu sisi tumetoka katika uchumi hodhi tumekwenda kwenye uchumi wa soko huria sasa, vitu hivi viwili unapokuwa katika uchumi huria. Kuanzia mwaka 1967 mpaka 1984.

Mimi ni mmoja wa viongozi ambao wamediriki na nimekuwa katika uchumi hodhi ninalewa kubadilisha fikra za watu kunahitaji kazi kubwa sana, elimu, uvumilivu na watu wakali wa kuwachukulia hatua wale ambao kwa jeuri tu wanakiuka taratibu.

Mfano mzuri juzi katika viwanja 20,000 vinavyogawanywa Dar es Salaam ambao sasa hivi nia ya Serikali ni nzuri sana kufungua makazi kwa kila mtu. Kila mtu apate kiwanja, maeneo ya biashara yawe mengi lakini juzi nilikuwa Dar es Salaam, mimi ni mmoja wa waathirika wa viwanja 20,000. Imenichukua karibu mwaka kupata hati zangu. Nimekwendwa pale huyo *Project Manager* hana habari kabisa. Ukipika ukiangalia ile ofisi yake yenewe ni tatizo. Watu wako kwenye msululu kuanzia hapa mpaka kule nje wanasubiri wapewe haki zao. Sasa madhumuni ya Serikali ni mazuri sana kwa mtu ye yeyote anayeelewa ni pale nilipokuwepo hapo Ofisini nilimkuta mwanamama mmoja anataka kuwekeza katika kujenga Shule ya Msingi na ukitaka nitakupa jina lake. Alikwenda mara ya kwanza kufika pale akaambiwa viwanja hakuna.

Juzi Serikali ikatangaza kwamba, viwanja viwo kwa sababu watu waliokwenda tu kujaza fomu bila uangalifu ukifika mtu ye yeyote unapewa hakuna *screening* yule mama akaambiwa hakuna viwanja. Juzi Serikali ilipotangaza kwamba viwanja vimebaki, yule mama nilimkuta pale amekaa ili aweze kupewa haki ya kupata kiwanja na alitaka ajenge Sekondari mwaka mmoja uliopita. Leo huyu ameathirika kiuchumi kwa sababu kipindi alichotaka kujenga shule ilikuwa mfuko wa sementi ni shilingi 6,800/= leo mfuko wa sementi ni shilingi 7,200/=, huyu ameshaathirika kwa sababu mradi wake *is not viable anymore*. Mradi ule umeshapanda thamani na hawezo kutekeleza. Angeutekeleza mwaka mmoja kabla, maendeleo yanepatikana. Sasa hii nimetoa mfano tuelewane kwamba katika utandawazi, uchumi wa soko, maamuzi ni muhimu sana yachukuliwe kwa wakati unaotakiwa. Ukishachelewa kwa siku kufanya uamuzi umeshachelewesha mambo mengi sana na umekwishaleta maafa makubwa katika chochote kinachotaka kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaloliomba hapa ni kwamba, fikra za wafanyakazi zibadilike na kila mtu aweze kufanya maamuzi kwa haraka. Ile *bureaucracy* ya Serikali iondoke na wote tujuu tuko katika utandawazi. Mwekezaji hatasubiri siku mbili kama anaweza kwenda kuwekeza Kenya. Leo kuna mipenyo sasa hiyo ni hatua yango ya pili ambayo ninaiomba Serikali katika kupambana na umaskini hatua ya pili Serikali ina wajibu wa kutafuta vipenyo. Kwa sababu Serikali ina watalamu, uzoefu na inajua vipenyo viko wapi. Kwa mfano, mwaka 2008 Tanzania itakuwa ni nchi mojawapo ambayo inaruhusiwa kulima maua na yeweze kusafirishwa kwenda nje bila kodi. Sasa mipango hii ni Serikali tu ndiyo inayojoua. Wenzetu walioko nchi za jirani wamekwishaona upenyo huo, wanatafuta wawekezaji katika Tanzania ili *wa-take opportunity*. Sisi hatuyajui, watu wetu hawayajui. Tumepewa *opportunity* za *AGOA* na bila kuzielewa na kuelewa mchezo wa kucheza huko kwenye *AGOA* tunajidanganya. Bado sisi tutatumika kama nyenzo ya kuwawezesha wenzetu waendeleze. Jumuiya ya Afrika Mashariki ipo na sasa hivi tunaweka *tariff* za pamoa.

Kama hatutaelewa *advantage* kama hiyo ya kupanda maua kwa sababu Tanzania inasamehewa kulipa kodi huko nje, watakuja wengine watawekeza hapa. Amini msiamini, raslimali watakazowekeza hapa zitanufaisha nchi zao sio Tanzania, watatupatia ajira kidogo. Maana leo ukichukua kwa mfano, uwekezaji wa bia, shayiri inatoka Afrika ya Kusini. *Obvious* wakulima wa shayiri *South Africa* ndiyo wanaopata faida. Zile kopo za kuwekea *castles*, bia, zinatoka Afrika Kusini. Kama malighafi asilimia 60 au 40 inatoka Afrika Kusini, unajenga uwezo wa ajira ya watu wa Afrika ya Kusini kwa sababu wao wanapata ajira huko sisi kazi yetu ni kujaziwa bia tunywe tulewe.

Sasa mtu anayeelewa uchumi na mtu anayependa nchi yake, unapofikia hatua hiyo ni ya kutisha. Kwa hiyo, nashauri Serikali ione hizo *opportunities*. Ni kweli ndege imewekwa mahali pa kupaa, lakini tusipoangalia ndege hii itatuletea matatizo katika kipindi kifupi inaweza ikapaa ikafika juu. Lakini *Air Hostess* wana matatizo, bado ndege itakuwa na matatizo, itatekwa nyara huko juu. Ndege inaweza kutekwa nyara hawa watu hawakabidhi uchumi wetu. Sasa sikatai tuchukue mwekezaji ye yeyote, kutoka

mahali popote, lakini tum-regulate ili mwekezaji huyo afuate kanuni na sheria za nchi yetu na huyo afuate utaratibu wa kutuletea faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MHE. ESTHERINA KILASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote, naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote, ambaao tumewachagua katika nafasi mbalimbali ndani ya Bunge letu Tukufu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba niungane na Wabunge wenzangu katika kuchangia hoja hii, Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kwa kweli Hotuba ya Mheshimiwa Rais ni nzuri sana, yenye mwongozo, yenye mwelekeo na yenye kutufanya sisi Waheshimiwa Wabunge, tujue ni nini ambacho tumekifanya kwa muda wote wa kipindi hiki cha miaka mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa ni mtovu wa fadhila nisipotoa shukrani kwa niaba ya Wananchi wangu wa Jimbo la Mbarali. Kama alivyozungumza Mheshimiwa Rais, katika kutoa taarifa ya utekelezaji wa kipindi chake chote hiki cha Awamu ya Tatu ni mambo mengi sana ambayo Wananchi wangu wa Mbarali wameweza kunufaika nayo. Nilianza Ubunge wakati Jimbo langu likiwa halina simu, mawasiliano ya barabara pamoja na umeme. Kwa kweli nasema Askari wa Miavuli ambaao Mheshimiwa Rais amejiwekea katika Awamu ya Tatu, wamefanya kazi nzuri sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale ambapo kwa namna moja au nyininge, umeweza kwenda kuona Wizara ambayo inagusa kwenye Jimbo lako, kwa kweli kazi imekuwa ikitekelezwa kwa kadri ya uwezo wa Wizara husika. Kwa hiyo, nina haki ya kuwapongeza na nitoe shukrani za Wananchi wangu wa Jimbo la Mbarali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais nitajielekeza zaidi katika sehemu mbili, kwa sababu ndizo ambazo zinagusa hasa kama fursa ya Wananchi wa Jimbo langu. Nikianzia upande wa mifugo, Mheshimiwa Lekule Laizer jana alizungumza sana kuhusu ufugaji na Mheshimiwa Rais katika Hotuba yake amezungumza sana kwamba fursa mojawapo ya Wananchi wengi ni kwa upande wa mifugo na nimpongeza kwa kuweza kufikiria ubinafsishaji wa hizi *ranches* zote za mifugo ambazo zipo ili kuwawezesha Wananchi waweze kujiondolea umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukizungumzia mifugo, wafugaji wetu wengi ni wachungaji. Katika Tanzania nzima, Jimbo langu ni la pili katika ufugaji, kuna ng'ombe zaidi ya laki sita. Sasa, mifugo hii haipunguzi umaskini kwani imekuwa ni uchungaji. Wafugaji wengi wa kutoka sehemu mbalimbali wamekuwa wakimbia Wilaya hii ya Mbarali. Lakini kwa kukimbia katika Wilaya ya Mbarali kumesababisha kuwa na ukosefu wa maeneo ya malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwhi kumwandikia Waziri hapa kwamba, kwa nini isichukuliwe Wilaya ya Mbarali ikawa kama ni mradi wa majaribio? Tulisema ili tufanikishe na kuondoa ugomvi wa wafugaji na wakulima tutenge maeneo ya kufugia na yatengwe maeneo kwa ajili ya wakulima. Sasa, Wilaya ya Mbarali kwa sababu inagusa kila kabilalau wafugaji, kila mpiga kura wa Mbunge ambaye yupo ndani ya Bunge hili, nina Wamasai, nina Wasukuma, nina Wabarbeig, nina Wagogo na makabila mengine yote yale ambayo yanajihusisha na ufugaji, unaposema iwe ni ya majaribio maana yake itakuwa imemgusa kila Mheshimiwa Mbunge hapa. Kwa maana hiyo tutatengaje haya maeneo? Kwa sababu unaposema tengeni maeneo ya wafugaji, maana yake ni kwamba, Halmashauri ishirikiane na Wananchi katika kutenga maeneo hayo na gharama ya utengeji maeneo ni kubwa sana, si kitu rahisi cha kufanya kwa siku moja. Kwa hali hii tutabaki kuendeleza ugomvi kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumwunga mkono Mheshimiwa Rais kwa Hotuba yake nzuri, ambayo ameitoa na kuangalia nini ambacho atatekeleza na kuwafanya Wananchi waone Chama chao cha CCM kweli kinawaona, Serikali yao ya CCM inawaona, naomba Wilaya ya Mbarali iangaliwe kwa namna moja au nyininge. Katika upande wa kutenga maeneo maana na kuchimbia malambo. Vile vile, Mbarali kuna chanzo cha maji ambacho kinachoanzia eneo la Ihefu na kuingiza maji tena kwenye chanzo cha *Great Ruaha* na wafugaji wengi wamekuwa wakimbia kwenye hiyo sehemu ambayo inaitwa Ihefu na ndiyo

kimekuwa kivutio cha wafugaji wa kutoka Mikoa mbalimbali na huwezi ukawatoa kule. Pamoja na kwamba ni *game reserve*, wamekuwa wakijitumbukiza humo, kwa upande wa wafugaji na wana sababu tosha ya kuwafanya wajitumbukize kwenye hiyo sehemu. Unaposema watoke, wataenda wapi maana ni lazima tuwaandalie sehemu nzuri ambazo tutawaweka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali itaungana na Halmashauri yangu ya Wilaya ya Mbarali au na Uongozi wa Mkoa mzima kuhakikisha kwamba inatilia mkazo, inatusaidia katika kutenga maeneo, inatoa huduma zozote ambazo zitawaweka wafugaji wasiguse kabisa eneo hili ambalo ni chanzo cha maji ambapo pia ni sehemu ya hifadhi ya wanyama, nafikiri kwa kweli tutakuwa tumenafaika na hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, niungane na Mheshimiwa Rais kuanzia ukurasa wa 53 - 58, amezungumzia sana kuhusu kilimo na kilimo alichogusia ni kilimo cha umwagiliaji. Amesema kwamba, mkakati wa Serikali yake katika awamu hii mpaka atakapomaliza kipindi chake ni kuhakikisha kwamba, skimu za umwagiliaji zinafufuliwa na kuhakikisha kwamba zinaboreshwu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya yangu ina skimu zaidi ya 20 na nyingi zilikuwa za majaribio na ilifanywa hivyo kwa sababu eneo hili ni kame, lakini ni vyanzo vya maji. Katika skimu hizo, zinazofanya kazi ni nne tu, ukizungumzia skimu ya Madibira, Ipatagwa, Kapunga na Igomelo, lakini zingine zote zilizobaki hazijaendelezwa. Zilifanywa kwa majaribio maana Wananchi hawajapata ile *ownership* kwamba wanahuksika vipi na waanze vipi.

Ningeomba kuunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Rais kwamba, Serikali ione umuhimu wa kuangalia hizi skimu zote zilizopo nchini ikiwemo na hizi skimu ambazo ziko Wilaya ya Mbarali. Kwa kweli ninaamini kabisa tutaondo umaskini, tutaboresha maisha ya hawa wakulima na kuhakikisha kwamba wanajikwamua kiuchumi.

Vile vile, ningependa nijielekeze kwenye upande wa huduma za afya hasa katika upande wa UKIMWI. Tumesikia hapa Mheshimiwa Rais katika Hotuba yake na sisi tunafahamu na Waziri amekuwa akizungumza kwamba, tatizo la UKIMWI limekuwa ni janga kubwa sana na hakuna dawa ya UKIMWI isipokuwa kuna dawa hizi za kurefusha maisha. Sasa, sisi wenye Majimbo ambayo yako vijijini na tuna hospitali za Wilaya, tumekuwa tukihangaika kwa sababu mgonjwa anapokuwa amezidiwa sana anajua hizi dawa zinapatikana Dar es Salaam kwenye Hospitali ya Muhimbili. Hatujapata uhakika umwambieje mpiga kura au mwananchi wako kwamba aende pale hospitali atapata hizi dawa za kurefusha maisha. Kama hizi dawa zinapatikana bure ni kwa nini zisigawiwe Wilayani?

Ni kwa nini na sisi Wabunge tusipewe taarifa ili unapoongea na Wananchi wako uwaambie kwamba hizo dawa zinapatikana mahali fulani? Pamoja na tahadhari zote za kujizua kupata UKIMWI, lakini pale ambapo mtu ameshapata UKIMWI, tunajua kinga mojawapo ni chakula bora na vijijini chakula tunafahamu ni cha wasiwasni na hasa wakati wa janga la njaa, tuweze kuwaambia kwamba, kuna dawa hizi za kurefusha maisha na wapi zinapatikana. Hata kama ni kidogo, lakini angalau mgonjwa akifika hospitali, Mganga Mkuu wa Wilaya, aweze kuwa na sauti kusema dawa ninazo au aweze kutoa hizi dawa kuliko ilivyo sasa, wagonjwa kusafiri kwenda Dar es Salaam kuhangaika ili waweze kupata dawa za kurefusha maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na hayo mawili, msisitizo mkubwa ni kwa upande wa mifugo. Kwa kweli mifugo inahitaji kuboreshwa kama Mheshimiwa Rais alivyosema.

Baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. (*Makofî*)

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza, nami niungane na wenzangu, kuwapongeza Wabunge mbalimbali tuliochagua kwenda kwenye Bunge la Afrika, *SADC PF* pamoja na Tume ya Huduma za Bunge. Vile vile, niwapongeze wenzetu waliotoka kuhiji, Alhaji Hashim Saggaf, Hajat Asha-Rose Migiro na Hajat Ntimizi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nimpongeze ndugu yangu, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa tena kurudi Bungeni. Kuja kwake siyo tu kwamba, kumefanya Wabunge

kuongezeka kwenye Bunge hili, lakini vile vile Makongoro wameongezeka kwenye Bunge hili. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais, kwa Hotuba yake nzuri sana, Hotuba ambayo kwa kweli inaeleza utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. Niungane na rafiki yangu hapa, Mheshimiwa Aggrey Mwanri kwamba, sasa tuka-*localize* Hotuba hii katika maeneo yetu. Ninasema hivyo kwa wale ambao hawajafanya hivyo, lakini kwa wengine kama Jimbo la Ukonga, kila mwaka tunatoa taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi mwisho wa mwaka na tutaendelea na hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, Hotuba ilikuwa nzuri na imeelezea mafanikio makubwa ambayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imepata. Lakini tujiulize, je, tusingeweza kufanya vizuri zaidi au hapo tulipofikia kwa mafanikio hayo tuendelee tu kujipongeza na kukaa kimya kwamba tumefanikiwa? Jibu ni hapana. Ni hapana kwa sababu pamoja na mafanikio ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, nchi yetu bado ni kati ya nchi ambazo ni maskini sana duniani. Ina maana gani? Ina maana kwamba, kuna maeneo mengi ambayo inatakiwa tujielekeze na Mheshimiwa Rais ameyataja kwenye Hotuba yake. Ndiyo maana nasema kwamba, kwa kweli kama tutatumia dakika zetu 10/15 kwa kupongezana tu, tutakuwa hatujafanya la maana kwa sababu hata Mheshimiwa Rais pamoja na kuelezea yale mazuri, ameelezea maeneo ambayo anadhani tuna haja ya kuboresha zaidi na ndiyo hayo maeneo inatakiwa sisi kama Wabunge, tujielekeze zaidi licha ya kujipongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya udhaifu yapo kadhaa na Mheshimiwa Rais ameyataja mengine. Pamoja na kuwa hakutaja eneo la rushwa, lakini hili la rushwa limezungumzwa sana na Waheshimiwa kadhaa wamezungumza na hasa Mheshimiwa Ibrahim Marwa. Katika ile hotuba ya Mheshimiwa Marwa kama ukinipa nii-*edit* sitatoa hata neno moja. Sana sana ninaweza nikaongeza kwamba: ‘Ndiyo sababu Mheshimiwa Hayati Mwalimu Nyerere aliwahi kusema kwamba, matajiri na wafanyabiashara hawatakiwi kwenye siasa.’ Labda nimalizie hapo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu suala la rushwa limezungumzwa, labda nizungumzie lingine ambalo hata Mheshimiwa Rais amelizingumzia na linaweza likawa linaathiri sana utekelezaji wa maeneo mbalimbali ya kuleta maendeleo kwenye nchi yetu na hii ni kwenye eneo la woga na kutofanya maamuzi, *indecision and inaction* kwenye maeneo mbalimbali na Mheshimiwa Rais amelitaja pale kwenye ukurasa wa 50 na ninanukuu: “Sisi wote hapo ni viongozi, zipo sifa za kiongozi bora, upeo mpana, uwezo wa kupima na kuamua na ujasiri wa kutenda na zipo sifa za kiongozi asiye bora, upeo finyu, uwezo mdogo wa kupima na kuamua na woga na mashaka katika kutenda.”

Mheshimiwa Rais anaendelea katuomba sisi Wabunge, amesema: “Naomba Bunge hili Tukufu, Bunge ambalo ni tumaini la Watanzania, liniunge mkono ili kwa pamoja tuwe na upeo mpana zaidi, tuimarishe zaidi uwezo wetu wa kupima na kuamua na hasa hasa tuwe jasiri zaidi kwa vitendo, kubabaika hata pale ambapo sera ni nzuri eti kwa vile tu kuna kikwazo au mapungufu madogo madogo hapa na pale huleta picha ya watu na viongozi ambao hawajaamua kwa dhati, wanababaika wanakwenda hatua mbele na hatua nyuma.” Mwisho wa kunukuu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Rais ametuomba tuwe wajasiri zaidi. Ina maana gani? Ina maana kwamba, bado tuna woga wa kutenda, ndiyo maana akatuomba kwamba tuungane pamoja naye ili tuondoe huo woga. Nasema hivyo kwa sababu ukiangalia maeneo mbalimbali na ninaweza kusema kwenye Idara na Wizara karibu zote, kwa kweli kuna michanganuo, kuna *write-ups* za kutekeleza miradi mingi sana, ambayo licha ya kwamba miradi yenye ni mizuri inaweza kutekelezwa, lakini imekaa hakuna uamuzi wa kutekeleza miradi hiyo. Sasa, huu ndio woga ambao nasema ni woga wa kutekeleza na kutenda.

Mheshimiwa Rais alishawahi kusema, alituambia Wabunge katika kikao fulani kwamba, anapata tabu Baraza lake halimsaidii. Wakati mwininge mambo ambayo yangeweza kutekelezwa na kuamuliwa na Mawaziri anapelekewa yeche. Sasa hapo nadhani ndiyo kuna tatizo hilo analosema ni uwoga na kusita katika kutenda, kwa kweli inaweza ikatuumiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa Kenya kwenye kongamano fulani la Kimataifa, nikamsikia Naibu Waziri mmoja akisema: “Sisi Kenya (yaani wao kule Kenya), kitu kinachowafanya wakawa bora

kuliko majirani zao ni kwamba wanatenda na mara nyingi wanachukua hata ile miradi iliyochanganuliwa na hawa majirani halafu wao wanatekeleza.” Sisi tunakuwa waoga wa kutekeleza. Sasa, unaweza ukasema kwamba tuna vikwazo, lakini bila kuamua kutenda, hivyo vikwazo utavimaliza vi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna miradi mingi ambayo tungekuwa na maamuzi ya kuitekeleza tungeweza kufanya maajabu katika nchi yetu, lakini tunakuwa na kigugumizi, tunakuwa na uwoga wa kutekeleza. Tumezungumzia mradi wa Mchuchuma kwa mfano, bahati nzuri sasa hivi kigugumizi kinaanza kwisha, lakini ni muda mrefu sana, sasa hivi tungekuwa mbali sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna mradi hata kabla ya Mchuchuma, tumekuwa tukizungumzia Mradi wa *Stigler's Gorge, Rufiji Basin*. Huu ni mradi ambao kwa kweli ungekuwa ni wa *long-term* na endelevu. Mradi ambao hata ukikopa fedha mahali popote ukautekeleza, wajukuu zetu wakilipa mkopo ule, watasema kweli tunaona ni kitu gani walichokopea hela hawa mababu zetu na watalipa mkopo ule hata bila matatizo yoyote, kwa sababu ule Mradi wa Rufiji ungeweza kutoa umeme, masuala ya kilimo, maji, kuzuia mafuriko na utalii. Una uwezo wa kutoa *megawatts* 2100 baada ya *phases* zote, sasa hivi tunatumia *megawatts* 450 na tukauza umeme na mambo kama yale. Lakini tunakuwa na kigugumizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna miradi mingine, hata pale Kipawa kwa mfano, sasa hivi kuna kero ya Wananchi wangu wa Jimbo la Ukonga na hasa wa Kipawa kuhusu upanuzi wa Uwanja wa Ndege kwamba, wanatoka lini. Serikali inakuwa na kigugumizi kuamua, kama fedha hakuna waambieni Wananchi wale bwana endeleeni kujenga na kuendeleza makazi yenu badala ya kuacha wanahangaika kwa miaka yote. Tulipewa miezi miwili kwamba Serikali itaamua wahame lini au walipwe fidia lini, lakini sasa miezi saba, kimya. Habari tulizonazo kwa sababu ya *Mini Budget* ni kwamba, hawawezi kufidiwa, hela haziwezi kupatikana. Waambiwe waendelee na mambo yao ya kila siku ili wajileetee maendeleo kuliko kubaki hivi kwenye umaskini kwa sababu *we fail to make decision*. Kwa kweli ni hatari kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme kwamba, haya mambo ya kutofanya maamuzi siyo tu kwenye Baraza la Mawaziri, hata kwenye Mabaraza yetu ya Madiwani, kwenye Halmashauri zetu na hata humu Bungeni, tuna uoga. Mtu akizungumza kitu cha ukweli bila woga anaonekana ni mtu wa ajabu, lakini yule mnafiki anayesema uongo na kujaribu kukumbatia mambo ambayo hayana msingi katika maendeleo ya nchi, ni ya kibinasi, anaonekana ni wa maana sana. Sasa, halitatuifikisha mbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli tunazo *resources* na ukitaka kujua kwamba tuna *resources* isipokuwa tunazitumia vibaya, angalia jinsi ambavyo *Mini Budget* karibu Shilingi bilioni 90 zinatokana na matumizi ambayo yalikuwa yawe mabaya, lakini yamezuiwa mfano magari na kadhalika. Kumbe kwa mwaka tungeweza kuzuia Shilingi bilioni 200 zisitumiwe vibaya kama magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tulipokuwa tunakwenda Arusha, pale Dar es Salaam kwenye *ALAT* tulikuwa na Wastahiki Meya wanne na Wakurugenzi wanne na mimi Mbunge kama mwakilishi wa *ALAT*. Magari 9 yaliandamana kwenda Arusha, mashangingi na *benz* langu la tisa likiwa nyuma, hakuna *coordination*. Siwalaumu kwa sababu hamna *coordination*, lakini je, Katibu Mkuu akitoka Dar es Salaam anakatazwa kweli kuwa na Wakurugenzi wake watatu kwenye gari moja? Ni lazima kila Mkurugenzi awe na gari lake? Haya ndio matumizi mabaya ambayo tungeweza kuya-save, siyo kwamba tingoje hali mbaya ya njaa ndipo Waziri wa Fedha aingilie aweze kuzuia. Sasa, haya yote tungeyafanya kwa kweli tungeweza kutekeleza mambo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasema tuache woga, tutekeleze kwa ujasiri mambo mbalimbali ambayo yanatutatiza. Tukiacha woga na tukawa wajasiri katika kutenda tunawenza tukafanya mambo makubwa sana, tusiache michanganuo ya miradi ilale kwenye makabati ofisini kwa miaka 10, miaka 20 bila kutenda. Woga wa kutenda ni lazima sasa uishe ili tuweze kwenda kama Mheshimiwa Rais alivyotuasa kwamba, tumsaidie kuondoa woga mionganoni mwa viongozi, mionganoni mwa Wabunge na mionganoni mwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa niaba ya Watanzania wa Wilaya yangu ya Ulanga, naomba kuunga mkono kwa dhati kabisa Hotuba ambayo Rais wetu ameitoa katika Bunge hili. (*Makofî*)

Lakini niungane na wenzangu kuwapongeza wenzetu ambao wamekwenda kutuwakilisha katika Bunge la Afrika, katika SADC na rafiki yangu Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge katika Bunge letu. Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere ni rafiki yangu sana kwa sababu tulikuwa karibu sana, tulikuwa majirani tulipokuwa Arusha. Niseme tu *comrade* karibu sana. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kusema kwamba, katika ukurasa wa 61 Mheshimiwa Rais amezungumzia sana suala la miundombinu. Kwetu sisi wa Wilaya ya Ulanga, tumebahatika sana kipindi hiki kupata pantoni mpya kabisa katika Mto wa Kilombero. Pantoni ile ni nzuri, ni ya kisasa na tulikuwa tunavuka kwa dakika 45, leo hii huwezi kuamini tunavuka kwa dakika 3. Ni kumbukumbu na historia ambayo nadhani inatia moyo kwamba, Serikali ya CCM kwa kweli inatekeleza ahadi zake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kwamba, nimekuwa karibu sana na Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, amenithibitishia kwamba, katika kipindi kifupi kijacho, Wilaya ya Mahenge, Ulanga, hasa pale Makao Makuu, tutapata simu ya *Celtel*. Ninamshukuru sana ndugu yangu, Mheshimiwa Profesa Mwандосya, kwa jinsi anavyokuwa karibu na matatizo ya Wizara yake. Katika hali isiyo ya kawaida, huwezi kuamini nilipoenda kuzungumza suala hili ofisini kwake, aliinua simu na kusema yafuatayo: "Watu wa *Celtel*, pelekeni simu Mahenge na kuanzia sasa mnieleze kila siku ni lini mtapeleka simu Mahenge." Huyo ni Waziri anaitwa Mheshimiwa Profesa Mark Mwандосya, Askari wa Mwavuli. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mheshimiwa Magufuli, sitaki kusema, amenishirikisha kwenye pantoni tangu makontena yalipoingia bandarini alisema: "Unaona hayo." Yalipoteremka Kilombero alisema: "Unaona hayo." Alipofungua pantoni alisema: "Unaona hayo." Hao ndiyo mimi nawaita *comrade*. Anasema na anatekeleza, watu wengine unaweza ukawaita ndugu tu inatosha, lakini *comrade* ni suala lingine. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme jambo moja ambalo ni tatizo. Sasa hivi tunaendelea na tutaendelea kupata misaada na Serikali itaendelea kupata mikopo kutoka maeneo mbalimbali duniani, lakini nina matatizo si ya kawaida kwa Wilaya ya Ulanga hasa Jimbo la Ulanga Mashariki. Tarehe 6 Februari, 2004 niliuliza habari ya maendeleo ya barabara ya Mahenge - Isongo - Mzelezi - Mwaya - Libenanga mpaka Mbuga na Chirombola, nikapata majibu mazuri sana. Lakini Serikali yetu imekopa *ADB* Shilingi bilioni 5 kwa ajili ya barabara hiyo na kilomita zinazotakiwa zitengenezwe ni kilomita 51 tu, Mahenge Mjini - Isongo - Mzelezi - Chirombola - Mwaya mpaka Mbuga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika barabara hiyo Mkandarasi anayeitwa *Mberu Constructor Limited*, ndiye aliyepewa ukandarasi huo kwa matumaini na taratibu zote zimefuatwa juu ya kupewa ukandarasi wake. Amewaaajiri akina mama kule Mahenge wanafanya kazi ya kokoto, wanafanya kazi ya kupiga mawe, wanafanya kazi ya kubeba mchanga na akina baba wameajiriwa kama vibarua katika njia nzima kwa nia nzuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda kukwambia leo kwamba, pamoja na majibu ambayo Mheshimiwa Waziri alinijibu hapa, Mheshimiwa Zakia Meghji ni Waziri mmoja mwenye uzoefu mkubwa sana na kwa bahati nzuri sana msingi wa Uwaziri wake ni kuwa Mkuu wa Mkoo na mara nyangi watu wanaoanza hivyo ndiyo wale ambao wanaitwa wanatoka vijiweni, wana mambo mengi mazuri.

Sasa, wale akina mama wa Mahenge, kokoto zao zilichukuliwa, wale akina baba ambao wamefanya kazi usiku na mchana katika barabara ile mpaka leo tunavyozungumza, hawajalipwa. Wameandamana kwenda kwa Mkuu wa Wilaya, wameandamana kwenda Polisi, wameandamana kuja

kwangu, wakilalamika kwamba tunaomba tulipwe, lakini Mkandarasi anayeitwa Mberu haeleweki na wala hajulikani anafanya nini.

Mbaya zaidi ni kwamba, yeye ni *contractor*, ana mikataba na *contractors wadogo (sub-contractors)*, ni mtu wa ajabu sana huyu, matokeo yake ni kwamba, kazi haifanyiki, madaraja ambayo yamewekwa makalvati hivi sasa yale makalvati yanapasuka. Sasa, nilitazamia kuwa baada ya swali lile angalau Waziri angetusaidia kwanza kuchukua hatua ya haraka ya kuhakikisha taratibu za kisheria zinafuatwa ili asimamishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lipo lingine, baada ya mazungumzo yangu Mheshimiwa Meghji, alifanya vizuri sana, amelisukuma suala hilo, safi sana. Amelisukuma suala hilo mpaka wiki iliyopita Mkandarasi Mberu amelipwa Shilingi milioni 70.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukuthibitishia zile pesa zote milioni 70 hazikwenda Mahenge, nimepigwa simu jana kwamba, hakuna aliyelipwa. Yule bwana Mberu alikuwa na utaratibu wa kuchukua pesa Dar es Salaam kwa hundi kupeleka Benki ya Mahenge. Sasa hapeleki, ana-cash pale Dar es Salaam, amepata zile shilingi milioni 70 anapeleka kwenye miradi mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naanza kupata majibu kwamba, kumbe zile kura ambazo Rais wetu anapata ‘hapana’ ni kwa sababu hiyo. Wale Wananchi wa Mbuga wanampenda Rais wao, lakini wale akina mama wa shida ya chumvi, *uniform* hawanunui, Mberu hawamwoni. Hivi akienda kupiga kura ya *Captain* atanipigia mimi, lakini kwa Rais anapiga ‘hapana’.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa tusaidiane katika suala hilo, limekuwa gumu sana kwangu. Mheshimiwa Waziri, ameniomba tukutane, tufanye mpango wa kwenda Mahenge. Lakini la ajabu zaidi na napenda niliambie Bunge kwamba, wale *subcontractors* wanaipeleka Serikali ya Tanzania Mahakamani na wanaipeleka *ADB* Mahakamani, kwa habari za jana, kwamba yuko Mkandarasi amepewa pesa za *ADB*, lakini hakuna kazi ambayo imefanyika na wala hawalipi wale ambao wanafanya kazi.

Wanatupeleka Mahakamani kwa ajili ya mtu mmoja anaitwa Mberu, huyu mtu ni mtu ambaye siyo wa kawaida, lakini kwa nini bado hotuba inasema kwamba inafikiriwa atapewa muda zaidi wa miezi mitatu?

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe kwako kwamba, ipo haja ya vyombo vyetu au wataalam wetu wawasadie hawa Askari wa Miavuli kwa hakika mambo anayofanya *Mberu Constructor* huko Mahenge ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa kusema kweli napata shida sana kuendelea kuzungumza suala lingine. Naomba kusema tu kwamba, naunga mkono hoja, nitafurahi iwapo tatizo la Wananchi wa Mahenge kulipwa pesa zao litashughulikiwa. Ahsante sana. (*Makofsi*)

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii, kushukuru na kuwapa kheri za mwaka mpya Wabunge wote. Ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge, waliochaguliwa kuingia katika Bunge la Afrika na kumpongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, ambaye ameteuliwa na Rais kuingia katika Bunge hili. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kuipongeza Hotuba ya Rais, ambayo imetupa changamoto kubwa sisi Wabunge na wananchi wote wa Tanzania. Hotuba hii inatupa mwelekeo mzuri, lakini pia imetupa historia nzuri juu ya uchumi wa nchi yetu jinsi ambavyo umeweza kukua hatua kwa hatua toka awamu hii ya tatu ilipoingia madarakani.

Hotuba hii imedhihirisha jinsi Awamu ya Tatu ya Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, ilivyotekeleza kwa makini, Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2000. Yapo mambo mengi sana ambayo Hotuba hii ya Rais imeweza kueleza waziwazi, maendeleo yaliyopatikana na takwimu ambazo zimetolewa kuhusu maendeleo.

Sasa kwa sababu Hotuba ni nzuri, ninaelewa wananchi wameiunga mkono. Lakini kwa sababu watu ambao hawataki tu kwa makusudi kuona mazuri ambayo yametendeka katika kipindi hiki, yasitupe fadhaa na kutufanya sisi tukate tamaa, tumuunge mkono Rais wetu kwa kipindi hiki cha miezi 20 aliyosema imeabaki ya kubaki madarakani na itupe matumaini ya kuendelea kufanya juhudhi mbalimbali ili tuweze kuitekeleza vizuri hii Hotuba na yale ambayo yamewekwa katika mpango wa maendeleo wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikizungumzia suala la umaskini kama alivyozungumzia Mheshimiwa Rais katika Hotuba yake, kwa kweli kimsingi Rais ametuomba wananchi wa Tanzania tubadilike, ili tuweze kuuondoa umaskini ni lazima wananchi wote wa Tanzania tubadilike tufanye kazi kweli kweli. Wakati wenzetu wanatembea ni lazima sisi tukimbiie ili tuweze kupata maendeleo ya kweli.

Tukitumia vizuri ushauri wa watalaam na tukiutumia ipasavyo, utatusaidia sana kuweza kuondokana na matatizo ya umaskini tunaouzungumzia hivi sasa. Lakini sharti kila Mtanzania akubali kufanya kazi na siyo kama ilivyo hivi sasa, kuna asilimia kubwa sana ya Watanzania ambao hawatumii nguvu zao kuzalisha mali au kufanya kazi ili kuweza kuliongezea Taifa hili mapato. Ikiwezekana inabidi Serikali itoe sera kali na sera hiyo ifuatilie kwa makini, ilazimishe au ihmize kwa namna yoyote ile ili mradi kila mtu aweze kufanya kazi halali na aweze kusaidia kujenga Taifa hili ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la usalama wa nchi yetu, usalama, utulivu wa nchi hii ni tunu ambayo ni lazima tuilinde kwa gharama yoyote, tusikubali mtu yeyote kuchezea hii tunu maana ikiporomoka au ikiharibiwa tujue kabisa tutaingia katika matatizo na kuipata itakuwa vigumu. (*Makofi*)

Tunakumbuka hadithi ya watu waliokuwa wanafari baharini na mtumbwi wakiwa wengi, lakini katika mtumbwi wakawa wanabishana, wengine wanasema twende mbele, wengine wanasema hapana turudi nyuma. Lakini katika kundi hilo alikuwepo mtu mmoja ambaye alikuwa hataki kubishana ila alikaa chini ndani ya mtumbwi, alijaribu kuutoboa ili mtumbwi ule uzame. Wenzake walipogundua kwamba huyu ameshatoboa na maji yameanza kuingia na walijua kabisa wako katika bahari kuu ambayo hawawezi kuokolewa kwa urahisi. Wewe mwenzangu Mtanzania unafikiri walimfanya nini? Huyu mtu ni wa kumuinua na kumtosa baharini ili atangulie na akitangulia mle baharini itakuwa ni halali yake. Sasa mtu anayechzeza utulivu na usalama wa nchi hii ni sawa sawa na mtu anayetoboa mtumbwi, tukimtosa itakuwa ni halali yake kwa sababu sisi tunataka usalama katika mtumbwi wetu, tubaki na utulivu ili tuweze kufika salama huko tuendako. Kwa hiyo, tunawaomba wale wenzetu wanaochezea amani na utulivu wa nchi hii, waache kabisa kwa sababu ni hatari kwetu na ni hatari kwao na tukiwagundua kazi ni moja tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwekezaji katika nchi hii, yapo mambo mengi mazuri yamezungumzwa kuhusu suala hili, mimi ninayo machache ya kuchangia. Kilio cha Wabunge wengi siku nyingi imekuwa ni kilio cha kutafuta mbinu mbalimbali ili tuweze kuondokana na umaskini. Sasa viro vitu ambavyo ni lazima tuzingatie ili tuweze kufanikiwa. Umeme hautoshi na siyo wa uhakika, maji hayatoshi au hayapatikani kwa uhakika, usafirishaji vivyo vivyo, mawasiliano hali kadhalika. Sasa unapomwita mtu kuja kuwekeza wakati vitu vya msingi havipo vya kutosha unaanza kupata mashaka kwa sababu wawekezaji hawakujitokeza. Kwa nini wawekezaji hawa wanataka kuwekeza Dar es Salaam peke yake au sehemu zile ambazo miundombinu hii niliyoitaja ipo? Ni kwa sababu wanajua wakiwekeza vitu vyao vitakwenda kama wanavyotaka. Sasa Mikoa mingine hii kwa mfano, Mara, Kigoma, hakuna chocotte, wanapiga kelele ukienda Rukwa hakuna miundo mbinu inayohitajika, unategemea lini mwekezaji aende kule? Tusikie kilio cha Watanzania kwa kuwa tunahitaji umeme zaidi ili tuweze kuwekeza na kuweza kuzalisha zaidi kwa ajili ya manufaa ya nchi hii. Miundo mbinu iangaliwe na iweze kuimarishwa. Umeme tunapozungumza usambazwe nchi nzima ni kwa ajili ya maendeleo ya nchi nzima na siyo kwa ajili ya watu wachache. (*Makofi*)

Kuhusu miundo mbinu ya reli, Serikali isipokubali kuwekeza pesa nyingi katika chombo hiki, *TAZARA* wala *TRC* itafika mahali vyombo hivi vitaanguka. Kama upo urasimu wa kubinafsisha hivi vitu tuhakikishe kwamba, urasimu huo unaondolewa ili tuweze kufanya kazi kwa manufaa ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la maendeleo katika elimu, nampongeza Mheshimiwa Rais, jinsi alivyotoa takwimu sahihi kuhusu maendeleo katika elimu na ninaomba nichukue nafasi hii, niweze kuwapongeza wananchi wa Mkoa wa Rukwa kwa jinsi ambavyo matokeo ya wanafunzi wa darasa la saba mwaka huu yamekuwa mazuri na tumeshindwa kuweza *ku-accommodate* au kuwachukua wanafunzi wote waliofaulu kuingia katika shule za sekondari kwa sababu ya upungufu wa shule. Lakini hii ni changamoto kwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa, wananchi wa Jimbo la Kalambo na wananchi wa Wilaya ya Sumbawanga ili waweze na wao kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa shule za sekondari ili tuweze kuchukua wanafunzi wote waweze kuingia shule za sekondari.

Kuhusu suala la kilimo ni lazima tufuate ushauri tulioupata katika hotuba hii. Serikali hasa Wizara ya Kilimo na Chakula, ihakikishe kwamba, mbolea inapatikana kwa wakati, madawa yanapatikana kwa wakati hasa kwa Mikoa hii ya Rukwa, Mbeya, Iringa na Ruvuma ili wananchi waweze kushiriki vizuri zaidi kuzalisha mazao kwa ajili ya kulisha Taifa hili. Kama Serikali itaendelea kutotoa ruzuku, nina uhakika hatutafanikiwa. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba hii. Ahsante sana. (*Makofsi*)

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais, ambayo mimi naiunga mkono moja kwa moja na kusema kwamba, ni hotuba nzuri sana na ni dira ambayo tungeweza kusema ni mwongozo mzuri sana katika kutekeleza Ilani ya Serikali ya Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakwenda moja kwa moja katika kuchangia, pengine nianze kusema wazi kabisa kwamba, sisi Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla tumefarijika na utendaji wa Mheshimiwa Rais, hasa katika eneo la barabara. Miaka minne iliyopita ilikuwa inachukua saa tano mpaka sita kutoka Songea mpaka Mbinga. Sasa hivi tunatumia chini ya saa moja na nusu. Katika kipindi hicho hicho magari yalikuwa hayaandi Litui, lakini sasa wafanyabiashara wanakwenda na gari ndogo mpaka Litui kwa mwendo wa saa mbili toka Songea mpaka Litui kwenda na kurudi. Kwa hiyo, haya kwa kweli ni mambo ambayo hayana budi kupongezwa. Kadhalika mawasiliano katika sehemu nyingine za Mkoa wa Ruvuma ni mazuri na sasa hivi njia zote zinapitika kwa msimu wote. Kwa hiyo, tunapongeza sana. (*Makofsi*)

Lakini la pili, ningependa niipongeze sana Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kwamba sasa hivi hata kijijini ninakotoka tunapata mawasiliano ya *Celtel*. Kwa hiyo, tunashukuru sana. Sasa haya ni baadhi ya mambo ambayo yamefanyika kwa kipindi kifupi sana. Pia katika suala la elimu (MMEM) sisi ni moja kati ya watu ambao tumeweza sana kujenga madarasa zaidi ya mara tatu ya yale ambayo tulikuwa tumepata fedha Serikalini. Kwa hiyo, ningependa niwapongeze sana wananchi wa Mbinga kwa jinsi walivyoweza kujitolea katika suala la ujenzi wa madarasa. (*Makofsi*)

Lakini zaidi katika kipindi hicho hasa ikizingatiwa kwamba, baada ya kubinafsisha Benki ya iliyokuwa ya Taifa ya Biashara mwaka 1997, Wilaya ya Mbinga ilikuwa na matawi ambayo yalibaki kama *NMB*, lakini mpaka leo yalikuwa hayajatoa mikopo. Lakini suala hili liliathiri sana maendeleo ya wananchi wa Mbinga, lakini hata hivyo, hatukukaa hivi hivi, wananchi wa Mbinga kwa kushirikiana na viongozi wao, waliweza kuhamasika baada ya kupata mwongozo sahihi wa Serikali kwamba, tuanzishe Benki za Wananchi na kwa kweli wananchi wameitikia, Benki imeanzishwa kwa muda wa miezi sita wameweza kutoa mikopo kwa wakulima wadogo wadogo, mikopo kwa wafanyakazi na wafanyabiashara. Kwa hiyo, tunaamini kwamba, tendo la kuanza kutoa mikopo litatusaidia sana. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio haya tuna matatizo. Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunapongeza sana kwa kutembelea Mbinga. Hali kadhalika tunapongeza sana Mheshimiwa Makamu wa Rais, naye aliitikia wito wa kutembelea Wilaya ya Mbinga pamoja na Mawaziri, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandomsy, Mheshimiwa Omari Ramadhani Mapuri, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Mheshimiwa Charles Keenya na Mheshimiwa *Brig. Gen.* Hassan Ngwilizi, hawa wote walipata nafasi ya kutembelea, tunawashukuru sana. Lakini lazima niseme tuna tatizo moja, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipofika aliona mengi tu mazuri, lakini ilibidi awashiwe vibatari wakati wa kutia sahihi. Hatukufanya hivyo makusudi, tulitaka kuonyesha hali halisi. (*Makofsi*)

Suala la umeme Mbinga ni suala zito sana kama ungewauliza wananchi wa Mbinga mnachagua nini, watakuambia tatizo lao ni umeme. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Mbinga wenyewe wakazi zaidi ya 23,000 mwaka 1996 ilifanyika sensa ilionekana kwamba, kuna jenereta 30 za kuwashia umeme. Kwa hiyo, karibu kila nyumba inakuwa na jerenereta lake, linatumia mafuta ya taa, *petrol, diesel*. Jinsi wanavyoweka waya hakuna chombo chochote kinachoangalia kama kazi inafanyika kiusahihi au laa, hakuna ukaguzi. Sasa naogopa kwamba, hili lenyewe tu linaweza kuwa ni hatari. Wilaya ile ni ya wakulima wa kahawa, tunalima kahama asilimia 20 inayotoka Tanzania. Kuna mitambo ya kumenyea kahawa zaidi ya 30 tunaita *central coffee periphery*, pamoja na *mini coffee periphery*. Kila mtambo unatumia jenereta yake. Kadhalika kuna viwanda vitatu vya kukoboa kahawa (*Coffee Curing Plant*) na kimoja cha kusaga na kukoboa ngano, ambavyo vyote vinatumia jenereta zake. Yako maeneo ya machimbo ya madini, ziko taasisi mbalimbali zote zinahitaji umeme.

Kwa msingi huo ungeweza kusema kwamba, Wilaya ya Mbinga hasa Jimbo la Mbinga Mashariki ni kama *light industrial area*. Kwa hiyo, jawabu kwa kweli ilitakiwa Serikali ione kwamba, watu wanaojituma kama watu wa Mbinga inawapa *priority* katika hilo suala muhimu. Ninyi wenyewe Waheshimiwa Wabunge, mmeona hapa juhudzi za watu wa Mbinga wanavyojaribu kusindika kahawa na kahawa ya Mbinga kwa mara ya kwanza inasifiwa ni moja ya kahawa bora duniani na tunajitahidi. Lakini tunachoomba Serikali nayo ione kwamba suala la umeme katika maeneo ambayo watu wanajituma ingekuwa ni la msingi zaidi kuliko mambo mengine. Naamini kabisa wananchi wa Mbinga sasa hivi wanasiakia na kilio chao kinaelekezwa kwa Serikali kwa sababu hili ni jambo ambalo hawana uwezo. Sasa watu wa namna hii wanaojituma, wanaojitolea, basi Serikali nayo iwaunge mkono. Mimi nasikitika ninaposikia wengine hapa mara wameweka umeme kwenye nyumba ya makuti mpaka wanalaumiana. Nikasema wenzetu huku wana bahati gani? Sisi tumejenga nyumba safi, Waziri Mkuu ni shahidi, lakini tunatumia vibatari, kweli haki inatendeka hapa? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishi Serikali kama watu wa Mbinga wamejitolea kiasi hicho, basi ni vizuri nayo iwaunge mkono. Serikali imetumia fedha kuweka nyaya za umeme, *transformer*, lakini hakuna umeme, kuna tatizo gani? Hivi kweli hamuwezi mkachukua hatua za dharura kutuokoa sisi katika janga hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ujumbe huu umeifikia Serikali na nina imani kubwa na Serikali yetu na naamini kwamba, suala hili la umeme angalau kwa hatua za muda mfupi, litafanyiwa kazi wakati kwa kweli tunasubiri suala la muda mrefu, nao ni umeme wa Mchuchuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, nasema tena naunga mkono hotuba hii. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. (*Makofî*)

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa Hotuba yake ambayo ni makini sana, ya kukumbukwa yaani ya kihistoria na ni Hotuba ambayo inatupa faraja na matumaini juu ya huko tunakokwenda kimaendeleo. (*Makofî*)

Vile vile namshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya yake anazidi kuimarika siku hadi siku kama alivyotueleza ye ye mwenye. Kwa kweli yatupasa wote, kwa moyo wa dhati, kuzidi kumwombea kwa Mwenyezi Mungu, ili apone kabisa na aweze kutimiza wajibu wake wa kuliongoza Taifa letu kwa muda uliobaki, akiwa na afya njema, kamilifu na timilifu. Vile vite tumwombe Mwenyezi Mungu, ili amkamilishie kazi yake amalize vema na hatimaye ndege ya maendeleo ya Taifa letu itakapokuwa inapaa, basi mkono wa Mwenyezi Mungu, utuelekeze kwa baraka tele kwa nani awe rubani wa kumbadili Rais Mkapa, hivyo tuweze kuendelea kuruka katika anga za maendeleo ya kisasa kwa salama, amani na mafanikio. Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Afrika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo ningependa kulizungumzia juu ya mambo aliyyoyazungumzia Mheshimiwa Rais, ni hili alilolisema kwamba, nchi yetu haiwezi kushinda umaskini wa kipato, kwa hadaa za ahadi za kupewa fedha mfukoni kwamba, jambo hili Serikali haiwezi kulifanya. Chama chochote kile hakiwezi kufanya hata kama sera zake ni za kuweka watu mapesa mfukoni,

haiwezekani kwa hali halisi. Kiongozi yeoyote yule hawezi kufanya ila linalowezekana kama alivyoeleza yeeye ni kuwapa watu fursa ya maendeleo kama hivi ambavyo Chama cha Mapinduzi kimetekeleza au tumetekeleza wajibu wetu tuliuweka katika Ilani ya Uchaguzi kuwa na barabara vijijini, ili wananchi waweze kupata nafasi ya kupeleka mazao yao sokoni, mifereji ya kilimo cha umwagiliaji maji kurahisisha kilimo kwa ajili ya wananchi. Shule mbalimbali ambazo zimejengwa kwa mpango wa MMEM ili kuwawezesha watu wetu kuwa waelewa katika mambo ya kilimo, mambo ya biashara na kadha wa kadha, kuwapa nafasi ya mikopo ili wapate mitaji ya kuendeleza mambo yao. Mafanikio kama haya ndiyo yanayoweza kuleta maendeleo kwa wananchi. (*Makofî*)

Sasa utakutaka jambo ambalo linasikitisha, wapo watu ambao pengine wanatafuta uongozi au uwakilishi wa namna moja au nyingine, ambao huahidi kutoa fedha, kuwapa watu fedha mifukoni na huzigawa fedha, halafu huzigawa kwa ujasiri kama vile akiulizwa yule atakayemwuliza atampa fedha mfukoni, halafu jambo linakwisha. Kwa hiyo, hii imageuza sasa siasa tunakuwa na biashara ya siasa na hili ni jambo la hatari kwani hii ni mianya ya rushwa. Viongozi wetu walijujengea misingi ya maendeleo na uongozi katika nchi hii kama Mwalimu Julius K. Nyerere, hatukuwahi kumwona hata siku moja akipita huko vijijini au mahali popote pale akigawa hela au Mzee Abeid Amani Karume au Mzee Rashid Kawawa au Marehemu Edward Sokoine na kadhalika. Hawajawahi kufanya hivyo, hili ni jambo jipya ambalo ni la hatari lazima tulipige vita. Hawa wanapotosha dhana sahihi ya kuleta maendeleo na kuondoa umaskini. (*Makofî*)

Sasa watu wa namna hii kama wakipewa uongozi au uwakilishi basi italazimu waanzu kutafuta fedha kwa njia za haramu ili waendelee kugawa hela. Lakini baadaye watakuja kukuta kwamba, hawezi kuwagawia watu wote hela, watakuta ni watu wachache sana wamepata hela na baadaye watakuta zimeisha. Zikiisha basi ndiyo mwisho, njia ya mwongo ni fupi. Kuna Msemo wa Kihehe unasema "uwudesi wudindang'asi" Unafika mwisho wa njia basi huwezi kuendelea mbele zaidi. (*Kicheko/Makofî*)

Katika Historia ya Afrika, viongozi wale waliokuwa na tabia ya kugawa hela badala ya kutoa fursa kama Mfalme Haille Selasie, alikuwa anagawa hela, watu waliumizana alipokuwa akigawa hela, lakini baadaye alikuja kuangamia kwenye Mapinduzi ya Ethiopia na historia yake ikawa ndiyo imekwisha. Rais Mobutu Seseseko, badala ya kuwapa fursa wananchi wa *DRC*, alikuwa anakusanya yeeye na akawa anazigawagawa zaidi ya kuzitumia yeeye. Yalipokuja mapinduzi ililazimu kukimbia nchi na alifia nje ya nchi yake, mpaka leo hakujawa na madai ya kuomba mwili wa Mobutu Seseseko urudi *DRC*. Kwa hiyo, ni vema mambo haya hasa sisi tulio katika Chama cha Mapinduzi, tuongoze kupiga vita mtindo huu ambao unaweza kuharibu mkondo wa maendeleo yaliyo sahihi, ambayo yamedhihirika katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi na maendeleo yanaonekana kwa macho. Tuachane na dhana potofu hizi za kugawa pesa ambazo ni za hadaa, hila na ulaghai. (*Makofî*)

Jambo lingine ambalo limenifurahisha sana ni jinsi Rais alivyozungumza juu ya maendeleo ya wakulima, wafugaji, wavuvi na wafanyabiashara wadogo, ndiyo watu wetu hawa walio wengi. Amelizungumzia suala la Ushirika. Bila kuelezea kwa undani ningependa tu nimnukuu kwa namna alivyoeleza Mheshimiwa Rais, katika Hotuba yake anasema: "Mheshimiwa Spika, idadi kubwa ya Watanzania ni wakulima, wafugaji na wavuvi. Kwao na kwa hali halisi ya nchi yetu, ipo njia moja tu ya uhakika ya kuwawezesha kutumia fursa za kuijendeleza katika mazingira ya uchumi wa soko. Njia hiyo ni Ushirika. Pamoja na matatizo yote yaliyovisibu Vyama vya Ushirika, bado ukombozi wa uhakika wa wakulima, wafugaji, wavuvi na wafanyabiashara ndogo ndogo ni umoja kupitia Ushirika. Nguvu ya mnyonge ni umoja". (*Makofî*)

Hili ni jambo ambalo limenipatia nguvu kwa sababu nimekuwa nalizungumzia sana kwa watu ninaowawakilisha katika Jimbo la Kalenga. Sasa ni sawa kwa mfano, sisi wanasheria kukiwa na *judgement* ambayo inaleta misingi fulani ya Mahakama iliyo juu yako kama *High Court* au *Court of Appeal*, basi tunasema *in a set precedent*. Kwa hiyo, baada ya hapo unafuata jinsi ambavyo imeeleza ile Mahakama iliyo na kauli juu yako. Sasa Rais ndio mwenye kauli juu yetu na haya ndiyo maneno yake. (*Makofî*)

Sasa baada ya kusema maneno haya, basi ni vema tuungane wote hasa sisi wa Chama cha Mapinduzi, kuhakikisha kwamba, watu wetu wanaungana, wajenge vyama ambavyo vinaweza kweli

vikawaleta maendeleo kama hivi ambavyo sasa amesema tutaanzisha fursa ya kuwa na mikopo ya *export credit guarantee schemes*.

Kwa hiyo, kwa mfano, kama sisi wa Mkoa wa Iringa vyama hivi vinaweza mbali na kuzalisha mazao mbalimbali lakini vinaweza kununua mazao kwa wanachama wao na watu wengine na vikaweza kuuza kwa nchi jirani za *SADC* kama Malawi, Zambia, Zimbabwe na kadhalika. Kwa hiyo, watakuwa wananchi wetu wamejiingiza katika maendeleo ya kisasa. Kwa hiyo, dhana hii ya maendeleo ni vema wananchi waielewe kwamba ni dhana sahihi na ya kweli na tuwe makini katika utekelezaji wake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ahsante. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa shughuli za asubuhi tunaishia hapo. Mjadala utaendelea tena jioni. Jioni ataanza Mheshimiwa Margaret Mkanga, ajiandae. Baada ya hapo nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 06.58 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia*)

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti*

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza jioni ya leo ili niseme machache kuhusiana na Hotuba kamilifu ya Mheshimiwa Rais. Kwangu mimi Hotuba ya Rais nimeiona kama ni maagizo mahususi kwa viongozi na nchi yote kwa ujumla. Nia ya Hotuba hii kwa ujumla nilivyoiona tumeshauriwa kuongeza kasi ya utekelezaji wa shughuli zetu katika kila sekta za maisha yetu. Hivyo basi, kwangu Hotuba hii naiona imekuwa ni maagizo na maagizo haya ni dira ya utekelezaji katika shughuli zetu kisiasa, kiuchumi na kijamii, kwa mtazamo na kasi mpya.

Baada ya kuzungumza hilo, naendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa sababu ametoa msukumo mpya wa utendaji kwa kuainisha maeneo matano ambayo yamo katika ukurasa wa pili mpaka wa tatu. Lakini zaidi nimefurahishwa sana pamoja na mengine yote na mafanikio yote ambayo kwa kweli siwezi kuyarudia, wenzangu tangu jana walikuwa wanayazungumzia, nimefurahishwa sana na dhamira yake alioionesha kamili kabisa ya kuongeza asilimia ya uwakilishi wa wanawake ndani ya Bunge na vyombo vingine vyote vya maamuzi ifikapo 2005. (*Makofî*)

Pia aliahidi na licha ya kuahidi, nadhani ni kujaribu kutekeleza maamuzi ya Mikutano ya *SADC* kwa sababu leo asubuhi kwenye Vyombo vya Habari kuna nilichokifurahia pia. *Mozambique* Waziri Mkuu wa sasa hivi ni mwanamke. Kwa hiyo, viongozi wetu wanajaribu kutupa fursa hizo tuweze kuonesha uwezo wetu kama wanawake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo ningependa kuyazungumzia kwa undani zaidi, kidogo ni kama ushauri kwa sababu hoja hii ilipokuwa inawasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, alisema nia iwe Wabunge kuweza kutoa ushauri ili angalau msukumo huu mpya uweze kutekelezeka vizuri zaidi. Maeneo mengi yametekelvezwa, lakini basi kama kulikuwa na upungufu tuisaidie Serikali kueleza hayo mapungufu kusudi hiyo *gear* mpya au ya nyongeza iweze kupigika vizuri. Kwa hiyo, nitazungumzia suala la elimu na baadaye labda kwenye sekta isiyo rasmi.

Nikianzia na sehemu ya elimu ni kwamba, suala la elimu nililiona ni muhimu hata katika Mikutano ya Kimataifa, ambapo malengo ya maendeleo ya *millennium* iliorodhesha kama lengo lake la pili kwamba ifikapo mwaka 2015 kila mtoto wa kike na wa kiume nadhani nchi zote tu duniani watoto hawa wawe wamepata elimu angalau ya Shule za Msingi kwa wote kwa ujumla wao na kwamba Benki ya Dunia na hapa ninanukuu: "Elimu ni maendeleo".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa elimu nimeongeza kwamba, elimu ni mwanga kwa sababu bila elimu mambo mengi mtu huwezi kuyatambua sawasawa hasa ya dunia ya leo. Kwa msingi huo

ni kwamba, elimu ni jambo la msingi kabisa la mwanzo. Ninatoa pongezi za dhati kabisa kwa Serikali kupitia Wizara ya Elimu kwa kubuni mpango wa MMEM na ambao tumeambiwa sisi tutaukamilisha kabla ya mwaka 2015 au miwili tu ijayo tutakuwa tumeshafuta ujinga kwa watoto hawa wa rika dogo, ndivyo ilivyo. Katika Hotuba ya Rais ameodrodhesha mafanikio yote ukurasa wa 32 mpaka 33.

Lakini pamoja na pongezi nyingi na matokeo mazuri yote yaliyoonekana, madarasa, uandikishaji umeongezeka, kufaulu kwa wanafunzi kumeongezeka. Ningependa kushauri na kusikitika kidogo tu, lakini sana ni kushauri. Nakubaliana kwamba idadi ya wanafunzi imeongezeka, wale wanaoandikishwa asilimia 50 ya wote wanaoingia kila mwaka, lakini wasiiasi wangu ni kwamba, hii asilimia ni asilimia ngapi ya watoto wenye ulemavu ambao wameweza kuandikishwa wakaweza kuingia madarasani wakasoma katika kipindi hiki cha MMEM? Wasiwasi huo unatokana na kwamba, ninavyofahamu kwa *research* ndogo kabisa, uandikishwaji wa watoto wenye ulemavu umekuwa na matatizo kwa sababu kwanza kuna tatizo la walezi na wazazi kuwaficha watoto wale wasiende shule. Pili, kuna tatizo ambalo linajitokeza mzazi atamchukua mtoto wake kumpeleka shule, walimu wanakataa kumpokea. Mimi wala siwalaumu walimu hao wala siwashangai, ni kutokana na kwamba hata akimpokea mtoto kwa mfano wa udhaifu wa akili itakuwaje? Kwa sababu shule zetu nyingi zina ukosefu wa mazingira au mahitaji maalum ya kukidhi elimu ya watoto kama hao. Kwa mfano, hakuna walimu wa kutosha wanaomudu kufundisha watoto wa aina hiyo. Kwa hiyo, hata Mwalimu Mkuu akimpokea yule mtoto na hakuna mwenye taaluma hiyo atamfanya nini na sio mmoja au wawili?

Huko mashulen i kwetu, majengo yetu, hili nalisema tangu mwanzo kabisa, wala hayakidhi haja. Hizo *wheelchair* zitaingizwaje kwenye majengo yenye ngazi nyingi? Inakuwa ni matatizo. Vitabu je kwa wasioona, vipo vya kutosha? Hakuna! Vifaa kama tape, hakuna. Sasa kwa kweli inakuwa ni matatizo. Kwa hiyo, pamoja na kwamba uandikishaji umepanda, nina wasiiasi kwamba, hawa wenzangu wa kundi langu bado malengo ya *millennium* ya 2006 kwa upande wetu hayatakuwa yamewafikia.

Ushauri hapo ni nini? Ushauri wangu ni kwamba, ili watoto hawa waweze kweli kumudu kupata masomo kama wenzao, naiomba Serikali ishughulikie upya kabisa kwa msukumo mpya uwekwe kwa ajili ya elimu ya watoto wenye ulemavu nichini. *Failure to do that*, basi hii jumla jumla kwamba wote wamekwenda shule, sisi kama watu wenye ulemavu ni wale watu wachache tu ambao watamudu kwenda shule.

Lingine ambalo nalishauri kwa sababu kila kitu kinakwenda na sheria na sera, ninaomba sheria zote zinazohusiana na masuala ya elimu, basi zirudusiwe tuzione zinabadilika ziendane na wakati kwa *ku-accommodate* kikamilifu watoto wenye ulemavu. Kwa mfano, Sheria ya mwaka 1978 *section* ya 56, ina matatizo yake, iwekwe sawasawa kusudi watoto hawa waweze nao kufaidika. Ninafahamu kwamba, elimu ya watu wenye ulemavu inatolewa na Shule za Mashirika ya Dini na kweli hapo nitoe pongezi. Mashirika ya Dini sasa hivi ndio yanayohangaikia sana mambo haya kuliko Serikali.

Kwa hiyo, Serikali iweke msukumo basi kuzisaidia Shule hizo kuzipa ruzuku kwa sababu zinainsaidia mzigo huo na kwa kweli ni mkubwa kwa sababu elimu ya watu wenye ulemavu ina gharama. Haya matumizi ya ziada ni gharama. Sasa basi shule hizo zipewe ruzuku ili ziweze kusaidia kikamilifu kwa sababu zimeisaidia Serikali.

Matatizo hayo na vikwazo hivi viko pia kwenye Shule za elimu ya kiwango cha Sekondari. Shule zetu za Sekondari zina matatizo hivyo hivyo, wengi wanashindwa kumudu. Kwa hiyo ni wachache tu ambao wanaweza kutoka Darasa la Saba wakaenda *Form One*, wakamaliza vizuri hata *Form IV*, matatizo yako mengi tu. Pamoja na kwamba katika kutahiniwa wanatahiniwa kama watu wa kawaida lakini wana matatizo mengi hawa. Utaambiwa huwezi kwenda huku kwa sababu umeishia *Division Four*. Lakini hiyo *division four* mmeiangalia huyu mtu alikuwa wa aina gani mpaka amejitahidi kuipata hiyo *division four* au *three*? Kwa hiyo, bado kwa kweli kuna matatizo makubwa.

Napongeza Taasisi za juu kama Vyuo Vikuu vimeanza angalau kuliona hilo kwamba, Wanachuo wenye ulemavu nao wana nafasi yao ya kuweza kupata elimu ya juu kwa kurekebisha mambo kadhaa. Ni mwanzo mzuri lakini bado tuna mengi ya kufanya. Hapa ninasema hivi, Shule za watoto viziwi ni chache. Iko moja tu mimi naijua ya Buguruni labda na chache mbili, tatu za Tabora zinazoendeshwa na Mashirika

ya Dini. Hawa wana akili kweli. Kwa masomo ya sayansi wanaweza sana kwa sababu wana-concentrate kwa kutazama na kufanya kwa mikono yao, wengi tunawaacha hivi hivi. Sekondari nadhani iko Ruvu tu basi. Chuo Kikuu ndio hawana nafasi kabisa viziwi kwa nchi yetu hii. Sasa haya mambo tunayafanya? Mbona hawa wangejitegemea wakisoma baadaye wanaweza kuwa sio mzigo kwa familia zao? Naiomba Serikali iangalie hayo.

Hotuba ya Rais imesema yafuatayo, nanukuu: "Tutafanya kila tuwezalo kuwapeni elimu." Basi hao katika hali hiyo ya kutoa elimu tuweze kuzingatia pia mahitaji ya watoto wenyewe ulemavu kwa sababu iwe ni elimu ya wote.

Kingine ambacho ningependa kuchangia kwa haraka haraka ni sehemu ya uchumi hasa ile sekta isiyo rasmi ukurasa wa tatu mambo haya yamesemwa. Hapa napongeza Halmashauri kwa sababu zimeanzisha kubuni maeneo maalum ya biashara na ya kuwa endelevu lakini rai yangu ni kwamba katika maeneo hayo, wafanyabiashara wenyewe ulemavu ambao wengi hufanya biashara ndogo ndogo, hawana uwezo hawa, wapewe kipaumbele cha kwanza kugawiwa maeneo hayo ya biashara kuliko ambavyo Mijini sasa hivi utakuta wanazagaa ovyo ovyo, wanabomolewa vibanda ovyo. Sasa katika maeneo maalum hayo, wapewe kipaumbele kusudi na wao waweze kujikwamua katika dimbwi la umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, nashukuru sana. (*Makofî*)

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja ya Hotuba ya Mheshimiwa Rais, aliyoitoa hivi karibuni na ninaunga mkono mia kwa mia. (*Makofî*)

Awali ya yote, ningependa kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge, ambao wamechaguliwa au tumewachagua wiki iliyopita kuijunga na Bunge la Afrika. Pia, napenda kumpongeza Mheshimiwa Sophia Simba, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge katika *SADC PF*. (*Makofî*)

Pia nampongeza Mheshimiwa Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, kuwa Mbunge katika Bunge la Tanzania. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, ambao kwa mwaka huu wamewahi kwenda kuhiji na kurudi salama. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba ya Mheshimiwa Rais kusema kweli ni kigezo kikubwa sana na kipimo kikubwa sana cha wale wengine ambao wataomba Urais kwa siku zijazo. Kwa hiyo, nadhani haya tuyazingatie kabisa katika kutafakari nani awe Rais kwa kipindi kijacho. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba hii mimi naiona ni ya Kimataifa kwani Mheshimiwa Rais pia amewapa changamoto wapinzani. Anawaambia Wapinzani wawe imara, wawe katika harakati za upinzani uliokomaa, sijawahi kuona na haijawahi na haijapata kutokea. Kwa hiyo, anawasisitiza kwamba wafanye juhudhi ya kuleta upinzani. Sasa hilo sio jambo bayaa kwa Wapinzani, ningependa waelewe hivyo kwamba ni mafanikio makubwa sana kama Kiongozi wa nchi wa Chama cha Mapinduzi anawaambia Vyama vingine waongeze nguvu. Mnataka nini zaidi ya hapo kama sio baraka kubwa hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nachukua nafasi hii kumtakia kheri Mheshimiwa Rais, aendeleee kupata nafuu ili aweze kurejea katika afya yake aliyokuwanayo hapo awali. Pia nachukua fursa hii kumpongeza kwa kishindo Mheshimiwa Rais, ametusaidia sana kutufikisha hapa tulipo kimaendeleo. Lakini pamoja na mafanikio yake yote, bado anasisitiza kwamba, 2005 ataachia ngazi. Sio jambo la kawaida katika viongozi wa Afrika, bila shinikizo lolote na akaamua kufanya hivyo na akalitangaza. Labda tu hii ni changamoto kwa wale wanaowania nafasi hiyo kujiardaa na kuona kama wataweza kufanikiwa katika kipindi kijacho. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa hali hiyo aliyotunesha bayana kwamba yuko tayari kuachia ngazi 2005. Mara nyingi viongozi wa aina hii wakipanda ngazi wakishafika juu, kwa kawaida wanaharibu ile ngazi kusudi wasiweze kushuka tena, lakini yeye ameamua kuimarishe ngazi ile ili aweze kushuka tena 2005, namshukuru sana. (*Makofî*)

Hotuba aliyotoa Mheshimiwa Rais kusema kweli inatuongoza, ni dira kubwa na inajaribu kuboresha mawazo yetu, inajaribu kutupa changamoto katika kupambana na hali ngumu ya uchumi

tuliyonayo. Sio hivyo tu, tunahitajika kutokana na hotuba ile, tuboreshe utekelezaji wetu, tuboreshe uwajibikaji wetu na mengineyo. Lakini ili kuipa uhai hotuba hii, napendekeza yafuatayo:-

Kwa hivi sasa tuharakishe kupeleka chakula cha njaa katika Majimbo yetu yote. Kwa mfano, Liwale hali sio nzuri katika Vijiji vipatavyo kumi na kitu hivi, Naoro, Nangano, Kibutuka, Kiperewe, Mirui, Kimambi, Ndapata na Vijiji vinginevyo. Nadhani hivyo ndivyo hali ilivyo katika Majimbo mengine. Kwa bahati mbaya kabisa Liwale sisi hatuna mawasiliano ya haraka, kwa hiyo, tunaathirika kwa kiasi gani, hakuna mtu anayejua. Kwa hiyo, huwezi kuona pitcha ya Mwana-Liwale aliyeathirika kwa njaa katika magazeti tuliyonayo sisi hapa. Naomba hili litiliwe maanani kwa ajili ya upelekaji wa chakula katika Majimbo yetu ili tuweze kuboresha na kuipa uhai Hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Namshuruku sana Mheshimiwa Lukuvi, kwa kipindi cha siku tatu, nne hivi, nilikuwa nazungumza naye ana kwa ana nikifuutilia chakula cha njaa na ninapenda kumhakikishia kwamba, nimeshapata tani 100 na leo hii zinasafirishwa kupelekwa Liwale. Nakushukuru sana kwa msaada wake huo na ninaishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kunisaidia kwa kiasi hicho na pia tumeahidiwa kupata tani 100 nyingine. Nashukuru sana na ninatoa *salute*. (*Makofi*)

Lingine ambalo nimeliona ambalo lazima tulikazie macho, tuache ukataji wa magogo, jamani miti inalia porini humo! Ukija Liwale sasa hivi kuna magari ambayo hatujawahi kuyaona lakini ya tani 50 yanabeba magogo. Tangu lini wananchi wakasema miti au misitu ni kero kwa wananchi? Nani kasema hivyo? Sisi sasa hivi tunapata mvua ya kutosha kule kutokana na hiyo miti, hebu Serikali itueleze, tunapata kiasi gani kutokana na hii miti ambayo inakatwa? Kusema kweli hakuna mtu wa kuwatetea, labda mimi hapa nilipo ndio nijaribu kutetea.

Tatu, ningependa pia kuona kwamba, wakati huu Waheshimiwa Wabunge wenzangu iwe ni wakati muafaka kwa kutafuta njia ya kutoa fidia kwa wananchi wanaoathirika na wanyamapori kama vile ilivyo kwa Jimbo langu la Liwale. Hawa wanyamapori ndio wanaua wananchi wetu na ndio wanaharibu mazao yetu kiasi cha kwamba bado Serikali inalalamika kututufutia chakula cha msaada. Naomba tuzingatie jinsi gani tunaweza kulitatta tatizo hili kwa kulipa fidia wananchi watakaoathirika, aidha mazao yatakayoharibiwa na wanyama hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naomba Serikali ihmize kupeleka mtandao wa simu kila Wilaya. Sasa hivi naelewa wazi kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu hawezi kupata taarifa yoyote mara moja kutoka Liwale pamoja na kwamba Liwale ni sehemu mojawapo ya Tanzania, lakini haina njia ya kupata taarifa yoyote haraka. Kwa hiyo, ningemba huu mtandao amba hapa Dar es Salaam, Dodoma na Miji mingine umesambazwa kwa fujo, basi sasa tutafute mikakati ya kupeleka katika Wilaya zile. Namshukuru sana Mheshimiwa Profesa Mwandsya, kwa juhudzi zake lakini tena naomba aongeze kasi kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Mawaziri na Manaibu wao waongeze kasi ya kufanya ziara katika Majimbo yetu. Hii itawasaidia kuelewa kwa undani zaidi hali halisi ya kila Jimbo. Hakuna *general formula* katika haya Majimbo tuliyonayo na tuachane kabisa na hiyo tabia ya kujibu hoja za Wabunge kwa kutumia makaratasi kwa *Desk officers* wetu. Mimi nadhani mkishaona mtaelewa wazi hali halisi ya maeneo yetu kikamilifu na mkaweza kutusaidia kimaendeleo. (*Makofi*)

Pia, nachukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri, amba kwa kipindi hiki kuanzia 2001 mpaka 2003 wametembelea Jimbo la Liwale ambalo pia ni Wilaya. Nao ni kama wafuatavyo: Mheshimiwa Ngwilizi, Mheshimiwa Mama Zakia Meghji, Mheshimiwa Mbawala, Mheshimiwa Kikwete, Mheshimiwa Mary Nagu, pia namshukuru sana Mbunge mwenzangu wa Walemaruvu amewahi kutembelea Jimbo langu hivi karibuni Mheshimiwa Mkanga, nakushukuru sana. (*Kicheko/Makofi*)

Kwa hiyo, ningewaomba au nazidi kutoa taarifa kwenu kwamba, naomba sana mtembelee Majimboni kwetu mwone hali halisi. Mlango wa Liwale au geti la Liwale liko wazi na mnakaribishwa na ninategemea kwamba Mawaziri wote kwa kipindi kilichobaki mtawezza kututembelea ili muweze kutoa msaada zaidi kusukuma maendeleo ya Jimbo hilo la Liwale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, ningeomba pia kurudia kusema kwamba, ninaunga mkono tena mia kwa mia Hotuba ya Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa. Ahsante sana. (*Makofsi*)

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nitoe mchango katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais na nianze kwa kuiunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofsi*)

Pili, nichukue nafasi hii kuwapongeza Wabunge wenzetu waliopata fursa ya kutuwakilisha katika vyombo mbalimbali ambavyo Wajumbe wake wanatoka katika Bunge hili. Wako wenzetu wanaotuwakilisha katika Bunge la Afrika na wengine *SADC* na pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kujiunga na Bunge hili.

Kimsingi, kabla sijaingia kwa undani sana katika hotuba yangu, nichukue nafasi hii pia kuishukuru sana Serikali kwa kufanikiwa kwa kweli kubinafsisha Kiwanda cha *SPM Mgololo*, kiwanda ambacho sisi kama wananchi wa Mufindi kilikuwa kinatutia hofu kubwa, maisha yetu yalikuwa katika shaka kubwa. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali na kumwahidi mwekezaji aliyechukua kiwanda hiki kwamba, sisi wananchi wa Mufindi na Mkoa wa Iringa kwa ujumla, tutashirikiana naye. Labda jambo moja tu ambalo napenda kuieleza Serikali ni kwamba, Serikali ikamilishe ile barabara ya Nyigo - Mgololo ili iweze kuwa inatumika na ili iweze kuwa ni ya manufaa kwa mwekezaji kwa sababu barabara hii inaweza kuwa kikwazo katika suala zima la uzalishaji katika kiwanda kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiona Hotuba ya Mheshimiwa Rais kama ni hotuba nzuri sana na ninaiona hotuba hii inatupa ujumbe kwamba hatima ya maisha yetu yako mikononi mwetu na kwa maana hiyo mtu akikwambia kwamba hatima ya maisha yako yako mikononi mwako, nadhani anakufundisha jambo lililo zuri, ambalo kwa kweli kama Watanzania ni vizuri jambo hili tukalielewa na haina sababu sana ya kuendelea kukosoa mapungufu ambayo wako watu wanasema yako ndani ya hotuba hii. Lakini mimi nadhani hotuba hii ni bora na haiwezi kuwa bora zaidi ya hapo. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama lipo jambo zuri ambalo pamoja na kwamba Serikali imetenda mambo mengi katika kipindi hiki, nafarijika sana na ufanisi mkubwa uliooneshwa na Serikali katika Mradi wa MMEM. Mradi huu kwa kweli umefanyika kwa ufanisi mkubwa sana na kwa sababu ni mradi uliofanikiwa labda pamoja na kupongeza, kwa ujumla tuwashukuru wenzetu wote waliotusaidia kufanikisha katika mradi huu. Tuwashukuru waliousimamia lakini pia tuwashukuru waliotukopesha pesa hata tukafanikisha mradi huu. Kwa hiyo, kwa ujumla wahisani wetu mbalimbali na wale waliotukopesha, nitumie fursa hii kuwashukuru sana kwa sababu kwa kweli wamefanya kazi ambayo ni ya historia katika maisha yetu.

Katika mradi huu kwa kweli ningeshauri Mradi wa MMEM uwe mradi endelevu. Unajua tunayo matatizo ya *culture of maintenance* hasa katika majengo. Tunajenga majengo mazuri au Serikali inafanya vitu vizuri sana, lakini taratibu za kuendelea kukarabati ili uzuri huo uendelee kudumu, mara nyingi imekuwa ni tatizo ndani ya nchi. Kwa hiyo, nashauri kwamba, Wizara inayohusika itengeneze utaratibu kwamba majengo haya mazuri yaliyojengwa karibu nchi nzima, yaendelee kuwa mazuri kwa maana kwamba, yaendelee kupata ukarabati wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini tulichoifunza katika mradi huu? Bila shaka sote tunafahamu kwamba, nchi yetu iliwhi kufikia asilimia 90 ya vijana wake waliokuwa shule na baada ya kuweka ada na michango mbalimbali. Asilimia 90 hiyo ikaporomoka mpaka kufika asilimia 56. Kwa hiyo, Mradi wa MMEM umetufundisha nini baada ya kufuta baadhi ya ada na michango? Katika Mradi wa MMEM mimi nilichojifunza kikubwa ni kwamba, ada na michango ni sehemu moja ya vikwazo vya ukuaji wa elimu katika nchi yetu. Sasa hivi tumefanikiwa vizuri katika MMEM na sasa hivi tunayo programu ya *SEDP*, ambayo inatarajia kuanza hivi karibuni. Ningependa kuishauri Serikali kwamba, kama MMEM imefanikiwa kwa sehemu kubwa kwa kufuta ada na michango, basi mradi huu wa *SEDP* uliangalie hili pia ili nao uwe ni mradi utakaofanikiwa.

Nasema hivi kwa sababu iwapo tulipata shida kubwa ya kusajili wanafunzi kwa ada ya Sh.3,000/= katika Shule za Msingi, itakuwaje ada ya Shilingi arobaini elfu iliyopo sasa katika Shule za kutwa za Serikali za Sekondari? Naamini na hili linaweza kuwa kikwazo, tunaweza tukajenga majengo mazuri kwa kutumia programu hii ya *SEDP* lakini tusipate wanafunzi. Kwa hiyo, naishauri Serikali *seriously* iangalie suala la ada katika Shule za Sekondari, katika Mradi wa *SEDP* ambao unatarajia kuanza hivi karibuni. (*Makofî*)

Lakini pia pamoja na uzuri wa Mradi wa MMEM, nadhani liko jambo moja muhimu lililosahaulika katika mradi huo na jambo hilo muhimu ni maslahi ya walimu. Walimu katika nchi hii ni watu wanaofanya kazi kubwa sana. Ni kweli kuna wakati Serikali iliona umuhimu wa kuwapa *allowance* maalum mwanzoni mwa miaka ya 1990, sasa baadaye ikaonekana kwamba, *allowance* hii ingizwe katika mshahara. Ikawa *consolidated* ikaingia katika mshahara lakini sasa kwanza, *allowance* hiyo ikaanza kukatwa kodi na kwa kweli uamuvi ule pamoja na kwamba ulikuwa mzuri lakini umepitwa na wakati. Wakati umeshakuwa mwingi mno, miaka imekuwa mmingi sasa, *consolidation* ile ilifanyika miaka ya 1994 au 1995, sasa ni zaidi ya miaka kumi. Mimi nasema kwa sasa *consolidation* ile haina faida tena.

Kwa hiyo, Serikali ijaribu kuona namna gani itaboresha maslahi ya walimu ambao kwa kweli wanafanya kazi huko Vijijini na wanaishi maisha ya shida sana. Ni kweli walimu, pamoja na kwamba nao ni watumishi kama wafanyakazi wengine, lakini walimu wana matatizo maalum na walimu wana kazi maalum na kwa kweli nchi hii lazima iangalie Ualimu kama ni kazi maalum ili programu hizi za elimu katika nchi yetu ziwe za manufaa. Kwa ufupi, naweza kusema, mishahara ya walimu ni midogo mno, Serikali ijaribu kuona namna ya kuongeza mishahara yao na mafao yao mbalimbali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo lingine kwa ufupi, nalo ni suala la kilimo. Nimekuwa nikijuliza mara nyingi kwa nini sekta nyingi wawekezaji wanakuja kwa wingi sana kuja kuwekeza, lakini sekta ya kilimo hapana, kwa nini? Jibu ambalo naweza kulisema kwa ufupi ni kwamba, sekta ya kilimo ina matatizo mengi, ambayo inabidi Serikali iyatature. Matatizo ya sekta ya kilimo ni mengi mno na kwa kweli kwa jinsi ilivyo sasa ni ndoto kuamini kwamba kuna mwekezaji atakuja kuwekeza katika sekta ya kilimo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachia mbali hewa ambayo binadamu wamepewa bure na Mwenyezi Mungu, kujulisha ni wajibu wa mwanadamu mwenyewe na ni wajibu wa kwanza baada ya hewa anayopewa bure na Mwenyezi Mungu. (*Makofî*)

Sasa hivi hapa tunalalamika sana suala la njaa, kila mahali njaa, lakini mimi naweza kusema kwa ujasiri kabisa kwamba, maamuzi tunayopata sasa ni kutokana na maamuzi mabaya yetu sisi wenyewe, maamuzi mabaya ambayo tumeyafanya. Ninataka nikuambie Taifa hili lilifika mahali lilikuwa linatumia mbolea za chumvi chumvi tani 165,000 kwa mwaka. Sasa tunatumia tani 65,000 kwa mwaka halafu tunashangaa njaa hii inatoka wapi. Haiwezekani, mtu yejote mtalaam akija kuangalia nchi yako anaanza, daftari yako ya matumizi ya mbolea unatumia kiasi gani cha mbolea! (*Makofî*)

Akija kuona unatumia mifuko 165 hana haja ya kwenda huko shambani, kwa sababu anajua huko shambani hakuna kitu. Nidyo ukweli wenyewe. Wakati mwingine nilikuwa nakumbuka ile jiografia yangu ya shule ya msingi, nilikuwa naambiwa kule Argentina kuna *Zone* inalima nafaka na Serikali inaangalia hiyo *Zone*. Tulikubaliana hapa kwamba, Mikoa minne ya Kusini ipewe jukumu la kulisha nchi na *tuli-subsidize* kwa kiasi kikubwa.

Sasa tukasema tulianza pale tuliposema sasa ruzuku tunafuta. Sasa tunalalamika njaa. Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, ambaye alisema kabla yangu, amezungumza kuhusu njaa na siyo yeye tu wengi wamezungumzia. Lakini ukweli ni kwamba, lazima tufanye maamuzi ya dhadi ya *ku-subsidize* mbolea. Lazima kabisa bila hivyo tutafuta mchawi usiku na mchana hatutampata, mchawi ni sisi wenyewe. Tufanye *serious subsidy* unasema unafanya *subsidy* ya chakula, ya mbolea bilioni 3, bilioni 4, *are we serious?* Mapato ya siku moja ya nchi ndiyo una-*subsidize* mbolea na unatarajia ujilishe, *is not possible.* (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *seriously* mimi nashauri kwamba, Serikali ilifanyie kazi suala la *subsidy* ya mbolea na nchi hii itapata chakula na tutauza na leo chakula ni biashara duniani. Mimi nasikitika sana. (*Makofî*)

Kwa hiyo, nafikiri kwa hayo machache ambayo nimesema Serikali imeelewa na mbolea hii ambayo tunasema sasa ni ya *subsidy* ya shilingi 14,000 kwa mfuko, mbolea hiyo bado ni gharama kubwa mno, wakulima hawawezi kuimudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofî*)

**MHE. NAZIR MUSTAFA KARAMAGI:** Akhsante sana Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu leo. Kwanza, nataka vile vile kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzetu wote, waliochaguliwa katika nyadhifa mbalimbali kutuwakilisha Afrika, *SADC* na hata Mheshimiwa Makongoro Nyerere, aliyejiunga na Bunge katika kipindi hiki kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais. (*Makofî*)

Ningependa kuchangia katika maeneo mawili kwa haraka haraka kwa sababu ya muda. Nikianza na eneo la mapinduzi ya kiuchumi. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais na Serikali yake yote, kwa kazi kubwa waliyoifanya kurudisha heshima ya nchi yetu ikatambuliwa Kimataifa kuwa na *international credibility*. Hii ni kazi kubwa sana na imefanyika katika *environment* ya utulivu kwa sababu tunajua nchi nyingi katika kufanya mageuzi ya kiuchumi lazima ujifunge mkanda na uweke vitu ambavyo wakati mwagine havipendezi kwa wananchi wako lakini vikiwa na maslahi ya huko usoni. Hili limeweza kufanyika hapa Tanzania kwa utulivu na kwa sasa hivi tumeanza kupata matunda yake. Kwa hiyo, nataka kumpongeza Mheshimiwa Rais na Serikali yake yote. (*Makofî*)

Sera sahihi ya ubinafsishaji mwanzoni tulanza kwa kuiona mbaya na kwa kupigiwa kelele na watu wengi ambaeo walikuwa hawajaiielewa sawasawa, lakini sera hiyo imeweza kuleta imani kwa wawekezaji wengi, imefanya nchi yetu ipate imani kwa wawekezaji wengine ikiwa na maana kwamba, wawekezaji sasa wana uhakika, vitega uchumi vyao viliyowekezwa hapa Tanzania viko salama na havitabinafsishwa. Sisi ambaeo tuko katika Kamati ya Uwekezaji na Biashara, tumepata bahati ya kutembelea viwanda mbalimbali hapa Tanzania na tumejionea sisi wenye kasi ya ufufuaji wa viwanda hapa nchini na hata vingine vinaendelea kujengwa. Amini msiamini kuna bidhaa ambazo zinatoka kwenye viwanda hapa Tanzania ukiziona huwezi kuamini kama zimetengenezwa hapa Tanzania. (*Makofî*)

Katika kila maendeleo kuna matatizo yake na Mheshimiwa Rais ametoa dukuduku lake kwamba, maendeleo ya kasi kubwa sana asilimia zaidi ya 80 yanaonekana Dar es Salaam na hii ni dukuduku ambayo ni msingi kweli kwa sababu Tanzania ni kubwa sana na wananchi walio wengi wako vijijini. Maeneo ambayo *yana potential* ya kuwa kama Dar es Salaam ama kukaribia Dar es Salaam, yapo isipokuwa tu yanahitaji ufunguo na miundombinu katika maeneo haya.

Sisi Wabunge kutoka Kagera tumeifarijika kusikia Serikali ikitamka humu Bungeni kwamba, Mkoa wa Kagera ni mmoja wa Mikoa ambayo unapata mvua karibu mwaka mzima na ina uwezo wa kuweza kuchangia ipasavyo katika kutoa chakula cha kulisha wananchi hapa Tanzania iwapo Mikoa mingine inapatwa na ukame. Sasa baada ya kusema hayo, tungependa Serikali iitupie macho Mkoa wa Kagera kwa mambo yafuatayo:-

Kwa kipindi kirefu sana Mkao wa Kagera umepata matatizo ya mawasiliano, hii ikiwa na maana haina usafiri wa uhakika wa meli, meli zetu ambazo zipo ni za zamani sana. Haina uhakika wa ndege kwa sababu kiwanja chetu ndivyo kilivyo hivyo na tumeweza kutoa rai yetu ya kutengeneza kiwanja cha ndege huko Kagera na Mheshimiwa Waziri mhusika, ameahidi kwamba, hili amelisikia lakini lipo katika mipango ya mbele sana. Lakini sasa tungeomba kwa muda mfupi uliopo angalau hicho kiwanja kiwekewe lami ndege iweze kutua nyakati zote. (*Makofî*)

Kitu kingine ambacho kinaweza kuwa ufunguo katika Mkao wetu wa Kagera hususan Bukoba, Bukoba Vijijini ni Wilaya Mama katika Mkao wa Kagera, wengine wanaweza wakabisha hilo, lakini ndivyo ilivyo. Lakini uamini usiamini, umeme ni kama asilimia 2 katika Jimbo la Bukoba Vijijini, kuna

maeneo makubwa Bukoba Vijijini kama Tarafa za Bugabo, Tarafa ya Kyamtware, ambazo zimezunguka Ziwa, zinaweza kuchangia ipasavyo kama zingekuwa na umeme wa kuweza kuweka viwanda nya samaki. (*Makofit*)

Tuna Tarafa ya Rubale na Tarafa ya Katerero ambazo zimezunguka Ziwa la Ikimba. Maeneo yaliyozunguka Ziwa la Ikimba, maarufu kwa *Ikimba Area*, pakiwepo na nyenzo ya umeme yaweza kuwa chimbuko kubwa la kilimo na viwanda vidogo vya *agro products*. (*Makofit*)

Najua kwamba, Serikali katika Bajeti ya 2000/2001 iliweka fedha kwa kitu hicho hicho lakini kama ilivyo ahadi hiyo haikuweza kutimia, bado ingali kwenye vitabu na wananchi wote wa Bukoba Vijijini wanaliangalia na wana hamu sana tena sana ya kuingia katika ndege ya Rais kusudi wakati ikipaa na wenyewe wasije wakaachwa nyuma. (*Makofit*)

Sasa kwa ufupi vile vile nilitaka kuchangia suala la utandawazi, Mheshimiwa Rais kama alivyoeleza katika Hotuba zake mbalimbali kwamba, utandawazi una faida zake na utandawazi una athari zake. Tanzania si kisiwa, kwa hiyo, hatuwezi kuepukana na huo utandawazi. Lakini kama nchi inabidi kupambana nao. Najua kwamba, utandawazi ni *global* lakini kwa mchango huu tu ningependa kugawanya katika sehemu mbili, *micro* na *macro*. Katika *micro* kwa haraka haraka haya ni mazingira ambayo ni sekta binafsi, inashindana na viwanda mbalimbali ama nchi mbalimbali katika soko ambalo linauza bidhaa sawa.

Kwa hili Serikali mchango wake ni mkubwa vile vile lakini si mkubwa sana, ni kuhakikisha kwamba, Mtanzania ambaye ana viwanda ama Mtanzania ambaye ni mkulima ambaye yuko katika kushindania biashara zake *ana-play* katika *level field*. Ili kufanya hivyo nafikiri limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi ni kuhakikisha kwamba, gharama za vitendea kazi ama *inputs* haviwekewi kodi zisizo za lazima na inapowezekana mahali pengine panabidi kupewa ruzuku ili tuweze kushinda vizuri.

Lakini kubwa ambalo nilitaka kuzungumzia ni katika *macro level*. *Macro level* ni nchi inavyoshindana na nchi. Nchi inavyojiwekeea mikakati yenye ili kuweza kufanya wananchi wake ambao wako katika nchi yake kushindana na utandawazi. Nchi inabidi kuangalia *strategic advantages* gani ambazo inaweza kuzitumia ili kuweza kushindana. Kwa hili nitatoa kama mfano, Tanzania imezungukwa na nchi tano ambazo ziko *land locked* lakini tuna mkakati gani kama Taifa wa kuzifanya hizi *land locked countries* zione bandari yetu ya Tanzania ni kama bandari yao. (*Makofit*)

Hili ni suala la muhimu sana kwa sababu sasa hivi tunashuhudia kwa mfano, Reli yetu *TRC*, Reli ya Katu imeshindwa kubeba shehena kutoka Bandari ya Dar es Salaam na mizigo inayotoka viwandani na tunaona malori yanakuja hapa Dodoma, hii inaashiria nini? Inaashiria kwamba kwanza, bei zetu huko mikoani zitakuwa kubwa na pili ambalo linatisha katika utandawazi ni kwamba, ushindani wetu Tanzania kama bandari au bidhaa zetu hazitakuwa *competitive* katika nchi zetu za jirani. Hii imetokana na kwamba, labda hatukuona reli yetu ya kati kama *strategic unit*. Kitu ambacho tunacho, ambacho tunaweza kukitumia katika utandawazi ili kuweza kushindanisha Tanzania na nchi nyingine. (*Makofit*)

Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofit*)

**MHE. NJELU E.M. KASAKA:** Nakushukuru Mwenyekiti, kwa kuniruhusu nizungumze. Kwa kuwa muda hautoshi na mimi nitazungumza kwa kifupi sana na kwanza naipongeza Hotuba ya Rais na taarifa yake aliyoitoa imeelezea mafanikio katika kipindi chake cha miaka minane iliyopita. (*Makofit*)

Ninachotaka kusema tu ni kwamba, kuna mambo machache kwa mfano kama lile la utandawazi ambalo mzungumzaji wa mwisho alikuwa analizungumzia na mimi nataka nilizungumzie. Utandawazi ni mashindano katika uwanja mmoja ya watu wasiolingana. Kwa hiyo, mnaingia katika mashindano watu ambao hamlingani, lakini kila mmoja anajaribu kufanya analoweza ili aweze kufanikiwa. Ninachosema ni kusema kwamba, utandawazi haukwepeki. Sisi hapa tunachohitaji kukifanya ni kwamba, utandawazi lazima uongozwe, uelekezwe, usimamiwe ili uweze kuleta manufaa kwa wananchi walio wengi. Vinginevyo utandawazi kama hautawekewa taratibu kama hizo utakuwa ni utajiri wa makampuni yatakayokuwepo hapa nchini na Watanzania wachache watakaopata uwezo wa kusogelea makampuni

hayo. Walio wengi watabaki maskini. Kwa hiyo, tuseme tu kwamba, utandawazi haukwepeki, tuseme haukwepeki lakini tuchukue hatua za tahadhari za kurekebisha na kuelekeza utandawazi tuukaribishe vipi. (*Makofî*)

Linaloungana na hilo, makampuni yanayokuja nchini tusipoyawekea utaratibu hata ajira wananchi wetu hawatazipata za kutosha. Sasa hivi tayari kuna manung'uniko, makampuni mengi yanayokuja hapa nchini hayawaajiri watu wetu walio wengi. Yanawaajiri wachache wengine kutoka nje wanawaleta hapa nchini na hatujakuwa na utaratibu mzuri wa kuwazuia wasilet watu wao hapa badala yake waajiri wananchi wetu na wengi wanaoajiriwa sasa hivi hawapewi ajira ila ni vibarua tu ambao wanafukuzwa kila baada ya wiki mbili, wiki tatu, wanaondolewa katika kazi hizo. Nendeni mkaone *Restaurant* nyding pale Dar es Salaam hakuna ajira za kudumu, wanabadilisha kila baada ya wiki mbili. (*Makofî*)

La pili, ninalotaka kuzungumzia ni suala la kipato. Kipato kimekuwa kikipewa tafsi nydingi. Lakini mimi nilifikiri kwa nchi maskini kama Tanzania, tusijingize kwenye falsafa ya kutaka kujua ni umaskini wa namna gani ambao Mtanzania anakuwa nao au hana. Ninachotaka kusisitiza hapa ni kwamba, umaskini ambao tunataka tuuzungumzie sisi ni umaskini wa kipato. Mwananchi asipokuwa na kipato hatakwenda hospitali kupata dawa, hatanunua dawa, hatamwona Daktari. Asipokuwa na fedha hatamshonea mtoto wake *uniform*, hatampeleka sekondari.

Kwa hiyo, jambo kubwa hapa ni umaskini wa kipato ndiyo tuuvekee umuhimu sana. Hivyo ni wajibu wa Serikali kuweka mazingira ambayo yatawezesha wananchi wengi wafanye kazi zenye kuleta tija na wapate kipato. Hilo ndiyo la msingi katika mazingira yetu sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulizungumzia hapa ni suala la Utawala Bora. Utawala Bora usipowekewa misingi mizuri au usiposimamiwa vizuri, nchi yetu itajikuta katika mazingira magumu. Lazima uwepo usimamizi wa kutosha katika mazingira yetu, lazima uwepo na uwajibikaji. Sasa mambo mengi yanafanyika bila uwajibikaji na mambo mengi yanaharibika hakuna hata mmoja anayejibika katika ngazi yoyote ile na tusipoweza kuwajibishwa watu waliokabidhiwa madaraka, hatutakuwa na mafanikio, tutakuwa tunaimba Utawala Bora, tunaendeleza nchi yetu lakini kumbe hatujafika mahali popote. Hivyo ndiyo sababu mambo mengi yanaharibika hapa nchini kwetu na kila mmoja anabaki kama alivyo na hakuna anayechukuliwa hatua au kuwajibika ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utawala Bora pia na kuheshimu madaraka, watu waheshimu amri zikitoka kwenye ngazi ya juu kwenda kwenye ngazi ya chini, lazima watu waziheshimu. Lakini hivi leo watu wanatamka maneno yote ya kipingana na viongozi wao na hawachukuliwi hatua yoyote na yanapotolewa maagizo hayatekelezwi na mifano tunayo. Mwaka 2003 hapa tulizungumzia habari za mbao mtu aliényang'anywa na DC wa Chunya, Bwana Ramadhani Kadu, Waziri hapa akaagiza kwamba, zirudishwe, hazijarudishwa mpaka leo na wamezuia wamekaa tu pale. Hawataki kutii amri za kiutawala. (*Makofî*)

La mwisho ambalo ninataka nilizungumzie kwa sababu muda wenywewe unakuwa ni mdogo hautoshi, nataka na mimi nigusie suala la rushwa na maendleo ya nchi yetu. Nchi yetu kwa kweli sasa hivi rushwa ipo na wala tusije tukadanganyika tukafika mahali tukasema kwamba, rushwa imekwisha, bado ipo. Matukio mengi yametokea, mimi mwenyewe hapa nilikuwa na ndugu yangu mmoja alikuwa na matatizo kule Mbeya, nilikuwa napigwa simu hapa kwamba wanahitaji hela, wanataka wapelekewe pesa, ili yule bwana aweze kufanyiwa utaratibu wa kesi yake aweze kutoka. Mambo kama haya yapo, yanasmuba watu na tusipoangalia nchi yetu itakuwa na mgogoro mkubwa huko tunakowenda, wachache watakaoajiriwa kutokana na ujanja ujanja na walio wengi watabaki maskini na italeta migongano katika jamii nchini mwetu. (*Makofî*)

Mgongano katika nchi yetu utatokea pale wachache watakapoonekana wametajirika sana kwa njia ambazo hazielezeki na walio wengi wanabaki maskini. Tungezungumza kwamba, nikijumlisha katika hilo la rushwa na utawala, ni kwamba ili mtu aweze kufanya rushwa lazima avuruge taratibu mahali pa kazi alipo na leo hii nilikuwa namsikiliza Yussuf Makamba, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam alisema, kiongozi yejote anayefumbia macho jambo linapoharibika, huyo mtu ni mchafu. Ingawa hakufanua maana ya uchafu ni nini lakini nataka niendelee kusema kwamba, kwa kweli mtu aliyefanya rushwa jambo

linapotokea hawezi kulikabili kama inavyopasa, ataogopa kulikabili kwa sababu yeye mwenyewe ni mhusika. Au anagopa kwamba na yeye watamwuliza kwamba na wewe je, mbona na wewe uko katika hali hii?

Kwa hiyo, nataka kusisitiza kwamba, tukitaka kupambana na rushwa tuangalie taratibu zetu, wale tulioakabidhi madaraka, wanatekeleza vipi, wanatekeleza kwa kufuata sheria na taratibu zilizotungwa ama kila mmoja anajifanya mambo yake? Hapa viongozi wetu wanalamika mara nydingi kwamba, watu hawatii maagizo, watu hawafuati taratibu zilizowekwa na ni mianya hiyo ndiyo inayosababisha pawe na rushwa katika jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu kusema kwamba, tukitaka kufanikiwa haya ambayo Mheshimiwa Rais ameyazungumza, Mheshimiwa Rais anajaribu kuyafanya mafanikio yake kuwa ni machache, yatakuwa yanaharibiwa ama yanaweza kurudishwa nyuma kutokana na watu kujingiza kwenye vitendo ambavyo si vizuri ni vitendo vya rushwa. Rushwa inaharibu nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu kusema kwamba, tulipokuwa tunazungumzia tafsiri ya umaskini nilitaka nizungumzie na tafsiri ya umaskini. Nchi yetu ya Tanzania inasemekana kwamba ni maskini. Lakini umaskini wetu siyo kwamba hatuna *resources* katika nchi yetu. Tunayo dhahabu. Mtu mmoja alikuwa anawatania Wasukuma hapa, akasema Wasukuma wamekalia dhahabu, wamekalia almasi. Lakini bado ni maskini. Kwa hiyo, mali yoyote ile kama haijatafsirwa kuwa fedha na ukahitaji hizo kupata huduma au kupata mali au kupata bidhaa, bado wewe ni maskini. Kwa hiyo, tusije tukatoa tafsiri potofu, kwamba maadam sisi tunazo mali katika nchi yetu, kwa hiyo sisi ni matajiri. Hatujawa matajiri bado, mpaka ule utajiri tuuibue pale ulipo, tuutafsiri katika mambo ya fedha na tupate fedha tuweze kununua bidhaa. Kwa hiyo na wananchi wetu wanaozurura zurura hawa bado ni maskini tunahitaji kuwasaidia, hata wafugaji lazima tuwasaidie waweze kutumia mali walizo nazo kuondoa umaskini wao, kama hawawezi kula chakula kizuri, hawawezi kuvala vizuri, hawawezi kusomesha watoto wao, bado wanahitaji kusaidiwa ili waweze kuondokana na umaskini katika nchi yetu.

Kwa hiyo, nchi yetu bado ni maskini, na tufanye mambo kwa bidii, tufanye mambo kwa uangalifu na Serikali yetu ijaribu kuongoza taratibu zote hizi mbalimbali ili wananchi wake waweze kufanya kazi zitakazowawezesha kupata mali, kupata fedha, kupata ajira, kupata mapato ili waondoe umaskini unaotukabili. (*Makofsi*)

Si suala la Serikali kuwapelekea mifukoni fedha. Hatusemi kwamba Serikali iwawekee wananchi mifukoni fedha, tunachotaka kusema ni kwamba, Serikali iandae taratibu zitakazowawezesha watu kufanya kazi zenye tija, kufanya kazi zinazoleta mali, waweze kuleta mazao wanayoweza kuyauza. Waweze kupata masoko kwa ajili ya mazao yao. Kwa njia hiyo, ndipo tutakapopambana na umaskini. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na mimi nakubaliana na Hotuba ya Mheshimiwa Rais, naiunga mkono, ilikuwa ni hotuba nzuri ambayo inatakiwa kufanyiwa kazi. Ahsante sana. (*Makofsi*)

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Ahsante Mwenyekiti. Kwanza kabisa, mimi naiunga mkono Hotuba hii ya Rais. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii inaendeleza maagizo yale ambayo aliyatoa wakati akifungua Bunge hili Novemba, 2000. Katika hotuba hii amezungumzia mambo mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge wamekwisha yajadili au kuyasemea, lakini nitasemea mambo matatu tu.

Kwanza, Mheshimiwa Rais amesema tukifanya kazi nzuri tujisifu na kujisifu kwetu siyo maana yake kazi imekwisha. Katika kutazama sekta mbalimbali ambazo zimefanya kazi nzuri, naona lazima na mimi niwe *on record* kuwa nazisifu. Kwanza ni ujenzi wa barabara, tunaziona kabisa barabara zinakarabatiwa, zimejengwa mpya na madaraja yamejengwa. Kabla ya Awamu ya Tatu, barabara zilikuwa karibu zimefutika. Lakini sasa tunaziona, nchi inafunguliwa. Wilaya yangu inanufaika na barabara ambayo sasa inatoka Dodoma mpaka Singida na Mwanza na wananchi wangu wa Wilaya ya Iramba wamesema nilete shukrani kwa niaba yao kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi. (*Makofsi*)

Pili elimu, tumeona MMEM imefanya maajabu, mambo mazuri kabisa. Elimu imepanuka, madarasa mengi yamejengwa na nyumba za walimu.

Tatu, mawasiliano, leo hatuwezi kungojea simu Ofisini, tupo hapa na kila mtu na simu yake. Hilo ni wazi kabisa kazi nzuri imefanyika. Mmi nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Wilayani kwangu Iramba, *Celtel* sasa inaanza kujenga mitambo pale. Sasa ningemwomba tu baada ya kukamilisha Makao Makuu ya Wilaya waendelee kwenye Miji Midogo kama ya Kinampanda, Ndago, Shelui, nayo ipate mawasiliano ya *Celtel*. (*Makofi*)

Tatu, Sekta ya Mawasiliano, Wizara ya Nishati na Madini, kazi imefanyika nzuri sana, tunaona na madini yetu sasa yameongezwa katika *foreign reserves* za Taifa. Lakini ningemwomba Mheshimiwa Waziri kuwa, Iramba ni mojawapo ya Wilaya ambazo zina madini ya dhahabu nyingi sana ambayo ipo katika *Lake Victoria Gold Fields Basin* sasa miaka mitatu au minne, hivi *Barrick International Corporation* wamekuja kufanya *prospecting* kwa muda mrefu sana. Lakini sasa wameondoka pasipokutoa ripoti. Sasa ningeomba Mheshimiwa Waziri, afuatilie na kuwauliza matokeo ya shughuli yao ya *prospecting* kusudi tujue kama Iramba kuna dhahabu?

Nne, mifugo na maji. Wizara hii imefanya kazi nzuri sana tunaona kila mahali. Lakini katika jimbo langu kuna matatizo ya magonjwa na wataalam walioko Mkoani Singida hawajafanya kazi yoyote, naomba Mheshimiwa Waziri, ajaribu kuwasitisiza wafanye kazi inayoonekana pia kuhusu magonjwa kwenye maeneo ya mifugo huko Wilayani Iramba.

Tano, kuna Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara hii hajjatufanya kazi yoyote katika Wilaya yangu, kwa sababu kuna mahali pengi ambapo pangefaa katika kazi za utalii lakini hawajaja kusaidia masuala ya uvuvi. Kuna Ziwa la Kitangiri ambalo lina ndege wa aina mbalimbali amba wanatoka Sweden na Siberia wanakuja pale wakati wa *winter*, amba wanakuja pamoja na kukaa wakati wa baridi, itakuwa baridi na hao ndiyo ingekuwa kivutio kwa utalii. Lakini ningeomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na wavuvi wa Ziwa la Kitangiri, waone umuhimu wa kuwasaidia, wanajifanya tu kazi zao lakini ukweli ni kuwa wanahitaji kusaidiwa nyenzo na vitu vingine vingine ambavyo vinaweza kuendesha kazi zao.

Kuna suala la kilimo, Wizara ya Kilimo na Chakula vile nionavyo ndiyo itakuwa kama injini ya ndege ya Mheshimiwa Rais. Injini hii naiona kama sasa imechoka inatakiwa kuwa *overhauled* kwa sababu hii ninazunguzia kwa sababu suala la kilimo ni suala siyo la kuendeleza chochote sasa ni suala la *ku-overhaul*, ni suala la kuleta mapinduzi na mageuzi katika sekta hii. Sina ugomvi na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, wale waliozungumzia kuwa kilimo cha jembe hakituendelezi popote. Lakini nina ugomvi kama kilimo cha jembe baada ya miezi mitatu ya mvua jembe linawekwa uvunguni kwa miezi mingi wakati wa kiangazi.

Mimi nasema hivyo kwa sababu katika Wilaya ya Iramba hatuna hata bwawa moja ambalo linatumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji mabwawa mengi ambayo tunayazungumzia ni kwa ajili ya matumizi ya mifugo. Hata hivyo natoa shukrani zangu kwa kuanza kujenga bwawa la Masagi. Mheshimiwa Waziri aliniahidi wakati wa bajeti mwaka 2002 kutujengea mabwawa mawili. Sasa ningemwomba Mheshimiwa Waziri kuwa sasa fedha zipelekwe kwa ajili ya kujengea bwawa la pili la Mto wa Kirondali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimetumwa na wapiga kura wangu na wananchi wa Iramba Magharibi kuwa wao katika Bonde la Wembele wanahitaji maji kwa ajili ya kumwagilia mashamba yao. Maji haya yanaweza kuvunwa kwenye Milima ya Senkenke. Kuna mito mingi na makorongo mengi. Mvua inaponyesha maji yanaleta mafuriko bondeni. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula aone umuhimu wa kutazama mradi huu kama ni mradi muhimu ambaa utachangia kuleta mageuzi katika suala zima la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa Mkoloni tulikuwa na kilimo cha umwagiliaji na palikuwa na Idara ya Umwagiliaji baadaye ikafutwa sasa ni wakati muafaka Idara hii ifufuliwe au waanzishe kisheria

Wakala wa Kumwagilia. Wale wataalam wasikae mikoani kama *TANROADS* wakae Wilayani kusaidiana na Halmashauri kuelekeza ujenzi wa mabwawa vijijini. (*Makofi*)

Naomba kama itawezekana hii injini ifanyiwe overhaul mapema ili kusudi kabla ya miezi 20 na ndege itakapopaa ipae na abiria wa sekta ya kilimo. Sasa kama hii ndege itakuja kuondoka na asilimia 85 ya wakulima wataachwa hii itakuwa imechukua abiria gani kama sio wakulima wadogo wadogo wa vijijini? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la kilimo ni suala la kuleta mapinduzi sio kuendeleza kwa sababu tunahitaji wananchi waweze kuvuna mara mbili au tatu kwa mwaka hata makali ya njaa hayangkuwepo. Nchi nyingi ambazo ziko katika kanda za majangwa na Sahelian hazina njaa wala ukame, ukame na njaa katika nchi yetu ni ya kujitakia kwa sababu hatujachukua tahadhari yoyote kujikinga tunangojea tu tukumbwe na majanga ya njaa na ukame. Kwa hiyo, ni vema sasa baada ya kupata matatizo ya njaa kali mwaka huu Wizara ijiandae kuhakikisha kusiwe na njaa na ukame katika miaka ijayo tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hotuba hii ya leo.

Awali ya yote kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge niwatakie Kheri na Baraka ya mwaka mpya Waheshimiwa Wabunge wote na tumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba ametujalia tumeona mwaka huu 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili niungane na wenzangu kumpa pole Mheshimiwa Rais na kumwombea kwa Mwenyezi Mungu kwamba aendelee kupona kwa haraka ili aweze kusukuma gurudumu hili la maendeleo la nchi yetu na ndege kweli iweze *ku-take off* na tusije kupata Askari wanaoning'inia nje bila kufikia malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile niwapongeze Wabunge wote waliochaguliwa katika Bunge la Afrika, Bunge la *SADC* na Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere kwa kuteuliwa kuwa Mbunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kwa kuunga mkono hotuba ya Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mawazo yangu, hotuba hii ni mwelekeo wa maendeleo ya nchi yetu. Hotuba hii imegusa kila nyanja ya maendeleo ya nchi. Ili iweze kweli kufanikiwa na ili iweze kweli *ku-takeoff* basi kila Askari wa Mwamvuli na wale watendaji wake wanahitaji waende kwa kasi hiyo hiyo, ama sivyo tusije tukaachana njia panda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili binadamu aishi kuna mishipa ya damu inazunguka inaleta uhai mwilini na moja ya uhai wa nchi ni uchumi lakini ili uchumi ufufuke unahitaji mawasiliano. Niipongeze Serikali hii kwa maelezo yake Mheshimiwa Rais kwa jinsi alivyofungua barabara za nchi hii. Kwa kweli kazi iliyofanya ni kubwa na unaona mabadiliko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile niipongeze Serikali kwa kuanzisha *Road Fund* ambayo inasimamia na kugawa fedha kwenye Halmashauri kuhakikisha kwamba kila Halmashauri leo isiweze kusema kwamba wameshindwa kutengeneza barabara zao na atakayeshindwa sasa kweli itakuwa ni uzembe wa Halmashauri na sio uzembe wa Serikali kwa sababu uwezo unatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudhi hiyo, nina ushauri katika maeneo yafuatayo. Moja, Mheshimiwa Rais amesema anasikitishwa kuona kwamba asilimia 80 ya mapato ya Serikali yanatoka Dar es Salaam. Lakini sasa utafanyaje? Wakati tuko kwenye Kamati za Bunge kule Dar es Salaam nilichangia hoja ya umeme wa Mchuchuma na umeme wa makaa ya mawe.

Sisi ni nchi ya ulimwengu wa tatu na tunataka wawekezaji toka nchi zilizoendelea lakini sijui kama kweli tunakuwa makini kujifunza kutoka kwao kwa sababu nchi zote tegemeo lao kubwa la umeme ni makaa ya mawe. Sasa kulikoni sisi tunataka *JET oil* ya mabilioni kwa nchi maskini kama ya Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Lindi sasa unachangia katika kuzalisha umeme kutokana na gesi iliyopo katika kisiwa cha Songsongo. Gesi inavutwa inakuja Somanga toka Somanga inakuja Dar es Salaam. Sasa mimi nilikuwa nawauliza wenzangu hivi mlishtamwona mtu anachukua ndizi Dar es Salaam akazipeleka Bukoba au Tukuyu? Si ataonekana mwendawazimu maana kule ndio kuna ndizi, sasa wewe uzitoe huku ambako hakuna unabeba unapeleka Bukoba au unapeleka Mbeya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachosema umeme wote uko Dar es Salaam leo mnatoa Mkoa wa Lindi ambako hakuna umeme mnapeleka huko huko kwenye ndizi nyingi wakapate zaidi hawa wasionacho watapata wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam wanatoa mchango zaidi kwa sababu wana wawekezaji wengi na wa aina mbalimbali nani atakuja Lindi, Mtwara au Bukoba mahali ambapo hakuna umeme? Uta-*develop* vipi EPZ kama huna umeme? Tulifanya semina ya EPZ hapa na DG wa NDC katika kujibu hoja aliniambia Lindi na Mtwara msahau EPZ kwa sababu hamna umeme, hamna *infrastructure*. Sasa katika hali hiyo, sio kweli kwamba tutaigawa nchi hii katika sehemu yenye maendeleo na isio na maendeleo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri kwamba tusiende katika foleni maana yule anayetangulia na wengine mnakuja nyuma, wengine wataachwa nyuma kabisa. Ili tuweze kwenda wote kwa pamoja basi twende katika *extended line* wote mmpangana katika mstari mnakwenda pamoja. Mkienda pamoja basi kile kidogo mllichonacho wote mnakipata lakini mkianza foleni wewe tangulia mimi nakuja ndio wengine kweli watabaki kule nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi liliulizwa swalii na kaka yangu Profesa Maghembe akasema Nyumba ya Mungu wanazalisha umeme je, vijihi vinavyozunguka Nyumba ya Mungu kama Panda, Kiti cha Mungu hawapati umeme? Jibu lilitoka ni kwamba fedha zimeandaliwa na zipo, lakini kwa umeme wa kutoka Somanga kwenda Lindi, fedha hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijihi nya kwetu vinaitwa Nangulukulu, Mandawa, labda na sisi tujibadilishi tuviite Bakuli ya Mungu, Meza ya Mungu, labda na sisi fedha zitakuwepo maana umeme unaanza Somanga unaambiwa pale fedha zinatafutwa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna tetesi kwamba mradi ule umebakiza fedha katika fedha zilizokopwa Benki ya Dunia. Je, Serikali ina kigugumizi gani kujenga hoja ya msingi kwamba Lindi na Mtwara hawana umeme na tayari wako Somanga pale kuutoa pale kuupeleka Lindi ni Sh.34bil na fedha zimebaki kwenye Sh.70bil *what's wrong?* Na sisi tunahitaji umeme angalau tupate wawekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa natania mimi nina *e-mail* lakini nikienda nyumbani kule nikikaa wiki mbili, tatu sina *internet*, hivi *internet* utaiweka bila umeme? Ukirudi huku Dar es Salaam kuja kuchokonoa tena unakuta *e-mail* ime-jam watu wanakuambia unaufutwa na nimeshabadili mara mbili.

Sisi katika Mikoa ya Kusini tunahitaji tupate umeme wa uhakika, tupate wawekezaji na tupate viwanda. Mji kama wa Lindi vijana hawana kazi kabisa kwa sababu hakuna mwekezaji wa aina yoyote, hakuna kiwanda cha aina yoyote. Naomba hili lizingatiwe tuende pamoja na tusiwe kwenye mstari mmoja ametangulia mwingine amebaki nyuma, ni hatari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ningependa kuchangia kwenye suala la elimu. Niipongeze Serikali kwa kazi nzuri inayofanyika ya kujenga madarasa ya MMEM na kwa kweli imebadilisha sura na sasa inakupa matumaini unapofika shulenii. Lakini naomba tuwe na usimamizi wa karibu sana kwa sababu yako maeneo tumefanya kazi nzuri mno lakini yapo maeneo kazi iliyofanyika bado ni ya uzembe. (*Makofi*)

Vile vile naomba nitoe ushauri ili tuhakikishe watoto wetu wanapata elimu kamili na sio semi-literacy basi mipango yetu iende sambamba. *Registration* imefanyika kubwa na nzuri na tumevuka malengo lakini madarasa ni machache na Walimu ni wachache. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofsi*)

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nichangie hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kweli Watanzania wote waliposikia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais wamefurahi sana na wamesema ni dira ya kampeni, kuna majibu yote ya masuala ya kampeni ya mwaka 2005. Watu wengine katika Majimbo yetu na sehemu nyingine walikuwa wanauliza tukiwaambia walikuwa hawalewi lakini hotuba hii tunamshukuru sana Rais imegusa kila sehemu. Sasa kazi ni kwetu kuifuata hotuba ilivyotoka na kuwaambia watu ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwombea Mheshimiwa Rais, Mwenyezi Mungu amjalie apone haraka matatizo yake ya kuumwa ili aweze kufanya kazi za Watanzania bila maumivu yoyote. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapitia maeneo machache tu kwa sababu hotuba hii labda utoke njie ya hotuba lakini kama uko ndani ya hotuba huwezi kusema maneno mengi. Hotuba yako haiwezi kuwa zaidi ya Rais utakuwa unaokoteza maneno. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii naomba waboreshe maeneo ya *ranch*. *Ranch* zinakuja na mfumo wa kupewa wenye uwezo wa kufuga hili litatuletea matatizo. Naomba pale kwenye ranch parekebishwe, vijiji vinavyopakana na ranch vipewe maeneo ya kufuga sio lazima wenye uwezo ndio wapewe zile *ranch*.

Kwa mfano Mkata nina vijiji vyangu pale wamepeleka maombi, kwanza *standard* ya maombi yenye vigezo vilivyowekwa mle mfugaji wa kawaida hawezi kuomba hata kidogo kwa sababu vinamtaka awe na mtaji, awe na uwezo wa kufuga, awe na ujuzi halafu afuge kisasa.

Sasa ukichampeleka mfugaji ninayemfahamu mimi kwa mfano wale wafugaji wangu wa Kidui yuko Laibon pale ana ng'ombe 3,000 sasa ukamnyima eneo unasema wewe hufugi kisasa humtendi haki. Sasa tunaomba na Laibon katika kijiji cha Kidui Kilosa cha wafugaji waongezewe eneo tu bila kujali vile vigezo.

Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Mifugo, wale watu hawarudi tena Arusha, Laibon ni Mmasai mfugaji wa juu sana halafu ana uwezo mkubwa sana, rafiki yangu sana. Sasa vigezo hivi hawezi kuweka huyu. Jana nakushukuru nilipokuja ofisini kwako ulinipa maneno mazuri sana kwamba tutaangalia na vijiji sasa naomba hilo ulichukue kama hivyo lilivyo litakuwa limeboresha hotuba ya Rais, *Mkata Ranch* kwenye hotuba ya Rais imo sizungumzi njie ya hotuba, imo hiyo. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie masuala ya *National Park* namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Zakia Meghji kwa suala zima la hoteli ya *Mikumi Lodge*. Sasa hivi kama ni wageni wanaoleta hela ya kigeni *Mikumi National Park* ina wageni wengi sana. Ile Kamati ilikwenda pale mwezi wa jana wageni ni wengi sana. Tatizo letu Mheshimiwa Waziri ni hoteli. Tumewaita wawekezaji wamejenga hoteli lakini hazifikii *standard* ya *Mikumi Lodge*.

Nakushukuru kwa nini kwa sababu ulisimamisha hotuba yangu nilipozungumza mwaka 2000 kwamba mwekezaji yule aliyewekwa pale asimame ukamsimamishe mara moja na umeweka Polisi pale sasa tunataka watafutwe wawekezaji wajenge ile hoteli, waikarabati na mimi najitahidi kutafuta nimeandika barua nyingi na nini lakini naomba mwekezaji pale, tafadhalii sana sehemu nyingine zinakuwa ni huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la *National Park* kwenye hotuba limo lakini tulizungumza kwamba ikiwezekana na kunusuru wale wanyama, juzi hapa Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa anasema wanyama wanakula *cement*, sijui lami na nini nikashtuka sana nikasema hivi kuna tatizo tena lingine?

Sasa tutazame namna ya kuchepusha ile lami sasa kama kweli wanakufa na lami tena mimi niliweka matuta yale kwa ajili ya kupunguza *speed* wanyama wasigongwe sasa imetokea, naomba sana hili Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi lifuatilie vizuri. Kweli wakati wa jioni baridi ile wanapenda kulala kwenye joto la lami sasa kama kweli tena wanalamba ile *cement* ile wanakufa naomba sana mnipelekee ujumbe kwa Mheshimiwa Rais sasa ile barabara ichepushwe Nkata, Kimamba, Kilosa, Zombo, Mikumi tutakuwa tumeshawanusuru wale wanyama. (*Kicheko*)

Wakati tunatafuta hiyo mipango mikubwa tuombe basi hata darubini kubwa ya kutazama wanyama wanapogongwa kuna watu bado wanakimbia. Sasa hili Mheshimiwa Waziri Zakia Meghji unaliweza hili tulete ile tochi kubwa ya kuangalia mbali wale wanaogonga kuwe na darubini kubwa ya kuangalia hao wanaokimbia, nilishaomba sana geti mkasema geti hapana itakuwa ni usumbufu sasa na darubini kubwa nayo tunamwangalia toka anavyotoka Dodoma hata ikiwezekana itokee hapa Dodoma mpaka Mikumi na Mbunge nione kwamba mnyama amegongwa bado inaleta taabu hii lakini hata ikiishia Dodoma, Mikumi yenye mpaka na mpaka sio mbali lakini hata kama inapiga hapa jioni na mimi naangalia basi wanyama watakuwa wamepona. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo cha Pamba, tumelivalia njuga na tunataka tuweke rekodi kwa sababu hii pamba tunaizungumzia tumechukua nafasi ya Mbeya sasa tunataka ilimwe Kilosa na Mkoa mzima wa Morogoro. Sasa tatizo naona Wizara ya Ushirika na Masoko inaangalia sana Mwanza na Shinyanga, tunaomba na Kilosa tuangaliwe. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilizungumza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko alifurahi tu lakini hatujakaa tukazungumza. Nilikuwa na *DC* wangu tunaomba mbegu iongezwe kule maana sasa kwetu ndio msimu wa kupanda pamba na nimewaambia bila matatizo bei ni Sh.300 kwa kilo naomba isibadilike tena pamba nydingi mkasema tunapunguza bei itatuletea matatizo kwenye uchaguzi. Tunaboresha hotuba ya Rais hapa ni pamoja na uchaguzi. Tumesema bei itakuwa Sh.300 kwenda mbele sasa isiwe tena Sh.300 kushuka chini tumeharibikiwa tutakuwa haturekebishi tena hotuba hii. (*Makofit/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la sukari mimi silisemi kwa sababu tulikwishesemba na bahati nzuri sasa amekuja Mheshimiwa Towagale Kiwanga aliliweka vizuri kweli juzi nilimsikiliza vizuri hapa alikuwa ametoa *data* namna ya kukuza kilimo cha sukari. Muwa unavyolimwa Kilombero tunaweza kulisha nchi nzima na nchi jirani na tukapeleka nje. Sasa tunalo tatizo ninyi Serikali mnasema *industrial sugar* sio mahali pake kujengwa katika kiwanda cha Kilombero hivi hayo majibu mapesi mapesi hayo mmeyapata wapi? Industrial sugar ndio mahali pake kwa sababu sasa hivi kwenye hotuba imesemwa kuna tani 228 viwanda vyote mwakani tunafika 300 ndio mahitaji ya nchi kwa nini sasa tusijenge *industrial sugar*?

Haya mambo mengine tunasema tulinde viwanda vyta sukari na tuwalinde wawekezaji sasa tukianza kuwanyima hayo mahitaji kwa watu wenyewe uwezo kama *ILOVO* hatuwatendei haki. Naomba *cabinet* ilitazame hili naona kama inalitazama kwa jicho la husuda hivi naomba walitazame kwa jicho la huruma kwamba sasa jengeni na mkubaliane mambo mazuri ya kuwekeza...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, naomba uelekeze mazungumzo yako kwenye Kiti.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Unajua haya masuala ya sukari unaweza kujisahau kwa sababu sukari ni tamu na tunazungumza vitu vitamu Mwenyekiti. (*Kicheko/Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nadhani Serikali imesikia na mimi nimemwelewa Mwenyekiti kwa hiyo nitaliweka vizuri kuangalia kwenye Kiti. Lakini niseme tu kwamba *TPC* wanalima

sukari, Kilombero, Mtibwa na Kagera mwakani viwanda hivyo ni hodari kweli kweli na vinaenda vizuri, tunawashukuru Wabunge wanaotoka maeneo hayo wametoa ushirikiano mkubwa. Mimi nasema Wabunge mnaotoka maeneo yenye viwanda nya sukari tushirikiane kwenye jambo hili sio linaonekana la Wegga peke yake mpaka tukubaliwe kuweka *industrial sugar* kwenye viwanda vyetu kimoja cha Kilombero kinatosha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu wengi wamezungumza sana humu ndani ni kweli sasa hivi watoto wanapasi mimi kwangu watoto 400 hawana pa kwenda hatujajenga Sekondari za Kata lakini tatizo ni kwamba pengine kinachochangia ni ada ya Sekondari. Mwaka jana niliuliza swali humu wakasema Serikali inajitahidi kulitazama hili jambo sasa tunaomba kwenye bajeti hii Serikali ilitizame suala hili.

Kama tumefuta ada ya Shule za Msingi watoto ni wengi kuliko watoto wa Sekondari na Shule za Msingi ni nyingi kuliko Sekondari sasa leo ukisema Sekondari walipe sisi Wabunge tunakuwa na taabu kweli kweli.

Mimi nilipokuwa nakuja Bungeni hili nimeacha kila mzazi anasema Mbunge nikopesha hela watoto wangu waende halafu wewe nitakuangalia wakati wa mazao, sasa Wabunge tuna hela jamani kwa nini lisitazamwe kwa ujumla wake na Serikali ifute tu ada ili Wabunge tupumue kidogo na jambo hili? (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sijui wenzangu yaani ukisikia tu matokeo ya Sekondari yametoka basi Mbunge kaa nyumbani vingenevyo utaambiwa umekimbia Jimbo kwa sababu wanafumuka Mbunge mtoto wangu amepasi sina hela sasa hivi naomba nikopeshe, naomba nikopeshe, sasa ishara hiyo inaonyesha kwamba hatutetei vizuri suala hili tunaomba tukubaliane lifutwe, futa ada watoto wasome. Mbona Kenya juzi hapa wamepata utawala wa Mseto wamefuta sisi tunasubiri nini? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pensheni, Bajeti ya mwaka jana imesema pensheni imepanda basi wanakuja wastaifu nyumbani wanasema Mheshimiwa Mbunge mlisema mnapandisha kutoka Sh.8,000-12,000, tukatoka Sh.12,000-20,000 toka walivyosikia na Hansard wanazo zile pesa hawajapewa. Mheshimiwa Mramba anafanya nini, sijui kama yuko humu ndani hili jambo lina uzito gani? Tusijikanganye wenyewe wana CCM. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nitoe shukrani zangu za dharti kwa kupewa nafasi hii adimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa mchango wangu, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kuingia kwenye Bunge la Afrika, Bunge la SADC na vile vile Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Rais ilikuwa ni hotuba nzuri yenye maagizo hasa kwetu sisi ambao ametuita Askari wa Miamvuli. Sisi hatuna uchaguzi na kwa kupenda tutatekeleza yale yote ambayo ametaka yaende kwa kasi na kwa kasi ambayo anaitegemea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu ndani nilikuwa nafuatilia sana majadiliano ya Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwashukuru na kuwapongeza kwamba wamekubali vipaumbele nya Serikali.

Serikali ilipanga vipaumbele kwenye elimu, maji, barabara, afya, utalii na mengine machache. Ukiufatilia michango ya Wabunge wengi wameona kwamba sekta zile zimetekeleza wajibu wao kama wanavyotakiwa na mimi nashukuru sana kuliona hilo na kukubali vipaumbele nya Serikali ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Rais wetu ambaye tunampenda sana kwa uwezo wake mkubwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutoa vema hoja ya kujadili hotuba ya Mheshimiwa Rais. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi wa Umma). Ni jukumu la Watumishi wa Umma kujenga utumishi uliotukuka na wenye tija. Nami kama Waziri nina kazi ya kuandaa sera na kuhamasisha watumishi wote watekeleze wajibu wao.

Watumishi wa umma ni lazima wawe mstari wa mbele katika kutekeleza yale yote ambayo ni jukumu tulilopewa na Mheshimiwa Rais kwa ufanisi, uadilifu na kwa kujituma. Watumishi wa umma kwa kiasi kikubwa ndio msingi wa utawala bora. Kwa hiyo, lazima wawe mstari wa mbele kuchochaea ukuaji wa uchumi na kuinua maisha ya wananchi wetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno ya Mheshimiwa Dr. Batilda Buriani, mengi yamefanyika na katika kipindi kifupi. Alikiri kuna mafanikio katika kila sekta. Utumishi wa umma ni utumishi unaogusa sekta zote hivyo sio rahisi kupata mafanikio yoyote ya maendeleo bila ushiriki na ushirikiano wa watumishi wa umma. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni mafanikio katika elimu basi kulikuwa na mwalimu ambaye ni mtumishi wa umma na ndiyo maana katika kuzingatia kipaumbele cha Serikali katika bajeti ya mishahara walimu wametengewa asilimia 54 wakati wenyewe ni asilimia 49 ya watumishi wa umma. Kama ni kwenye barabara kuna wahandisi na katika afya tuna madaktari na manesi ambaeo wote hawa ni watumishi wa umma. Hivyo basi ni vigumu kuongelea mafanikio tuliyopata hivi sasa bila ushiriki wa watumishi hawa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu mwenyewe Mheshimiwa Rais ambaye ni rubani wetu kasema tukumbuke kujisifu lakini na watumishi wa umma lazima nao tuone wamechangia ipasavyo. Ila nawaomba watumishi wa umma na sisi wote tusibweteke kwa sababu mafanikio haya hayajatufikisha pale ambapo tunataka. Bado tuna mengi ya kuboresha ndiyo maana Mheshimiwa Rais ametupa jukumu kubwa na amesema jukumu letu kubwa ni kubadili mitazamo. Watumishi wa umma lazima waone kuwa wao ni msingi wa kuwezesha sekta binafsi na wananchi kuleta maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia *programme* ya uboreshaji wa utumishi wa umma ambaeo Waheshimiwa Wabunge mnaifahamu tumebadilisha sheria, miundombinu, taratibu na kanuni za uendeshaji wa Serikali ili kwenda sambamba na matakwa ya wakati huu. Kwa kuwa haitoshelezi tu kubadilisha sheria, kanuni, taratibu na hata mifumo, kazi kubwa iliyombele yetu ni kubadilisha mitazamo ya watumishi wa umma ili tuweze kupiga hatua zaidi na ile ndege ambayo Rais anataka aache inapaa iende kwa kasi na itufikishe kwenye maendeleo ambayo Watanzania wanatarajia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii pia kwa sababu muda ni mfupi kujibu hoja ya Mheshimiwa Msindai aliyozungumzia kuhusu Sheria Na. 8 ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2002. Ningependa kufafanua kuwa kwa mujibu wa Katiba yetu, Tanzania ni nchi moja na Katiba inatambua kuwepo kwa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Sheria hii inafafanua zaidi mgawanyo wa madaraka kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, inatoa madaraka, inaboresha utendaji na inasisitiza uwajibikaji katika ngazi mbalimbali.

Kupitia sheria hii mamlaka ya ajira, usimamizi na nidhamu yapo katika kila Halmashauri. Mabadiliko yaliyopita au marekebisho yaliyofanywa ya sehemu ya 6(6) yameturudisha nyuma kidogo, lakini niliahidi katika Bunge hili na ninaendelea kuahidi kwamba marekebisho mengine yatafanyika baada ya kupitia taratibu zinazotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Sheria hii kila mtumishi atapimwa kupitia matokeo ya kazi na si vinginevyo. Kwa hivyo maafisa wagani kama hawafiki kwa wakulima basi wale wazembe itabidi waachie ngazi. Pia kwa kupitia Mkataba wa Huduma kwa Mteja tunawaomba wananchi kutusaidia kuwafichua watumishi wazembe na kuhakikisha kuwa vigezo vyta huduma vilivyobainishwa katika Mikataba hii vinatekelezwa. Kwa kupitia mabadiliko haya makubwa yaliyopitishwa na Bunge lako watumishi watalazimika kuwa waadilifu na watendaji wazuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile sheria inawabana waajiri wasiochukua hatua yoyote pale panapokuwa na utovu wa maadili. Kwa sheria hii sasa, Tume ya Utumishi wa Umma itakuwa inasimamia mienendo ya waajiri wote. Wale ambao hawatachukua hatua kwa manufaa ya Taifa itabidi Tume ya Utumishi wa Umma iwawajibishe na iwave nafasi hiyo wengine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine inayosisitizwa ni maadili ya watumishi. Juhudi kubwa zinafanywa kuhakikisha kuwa kila mtumishi anaolewa maadili ya utumishi wa umma na anayaafuata. Hii itapunguza kwa kiasi kikubwa utovu wa nidhamu na hata rushwa katika sehemu za kazi. Kama watumishi watapimwa kwa matokeo ya kazi hawatakuwa na muda wa kuomba chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la rushwa ni suala gumu, lakini naomba nieleze kwamba kwa kweli kwa vigezo ambavyo *Transparency International* na kwa maneno ya Waheshimiwa Wabunge wengine rushwa imepungua lakini haijaisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mwaka 2001, kwa vigezo vyâ *Transparency International* tulikuwa wa kumi kwa kuwa na kiwango kikubwa cha rushwa. Takwimu zao za sasa zinaonyesha kwamba sisi tupo wa 20, maana yake rushwa imepungua. Sasa hivi tupo mbioni kuunda Kamati za Maadili katika Wizara na Idara mbalimbali za Serikali kusimamia kwa ukaribu zaidi maadili ya utumishi yakiwemo uzembe na mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge mbalimbali katika kuchangia hotuba wamezungumzia pia uondoaji wa mianya ya ukabila na udini hasa katika ajira. Katika utumishi wa umma mianya hii ingweza kuwepo katika ajira na upandishwaji vyeo. Sasa hivi ajira zote na upandishwaji vyeo ni kwa njia ya ushindani, ambapo kazi zinatangazwa na wale wenye sifa wanaitwa kwa usaili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ningependa kuwashukuru sana Wabunge kwa kutoa mchango wao, lakini naomba tuone kwamba watumishi wa umma ni sehemu ya mafanikio na kama tunataka mafanikio zaidi ni lazima tuwe nao. Utumishi wa umma ndiyo unaohakikisha amani, utulivu na utawala wa sheria na mimi kama msimamizi wa utumishi wa umma nitahakikisha kuwa juhudi za makusudi zinafanywa kubadilisha utumishi ili uwe na mtazamo wa kuwawezesha na kuwajenga wananchi kuijendeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wengine kumwombea Mheshimiwa Rais afya njema ili aweze kutekeleza wajibu wake wa kutuongoza sisi ili tuendelee kupaa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa nidhamu ya utumishi wa umma niunge mkono hotuba hii na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mwenzetu mmoja anataka kutoa maelezo binafsi. Kwa hiyo, nitaomba Mheshimiwa Waziri atoe hoja ya Kuahirisha Bunge.

#### KUAHIRISHA BUNGE KABLA YA WAKATI WAKE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mujibu wa kifungu 21(6), naomba Bunge lako Tukufu liahirishwe sasa kabla ya muda wake hadi kesho saa tatu asubuhi.

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lydia Boma, kwa kutumia Kanuni ya 21(9) anataka kutoa maelezo yake. Kwa hiyo, nampa nafasi aendelee na kutoa maelezo yake. Karibu Mheshimiwa Lydia Boma.

## **HOJA BINAFSI KUHUSU MADHARA YATOKANAYO NA WANYAMAPORI**

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ni moja ya nchi chache sana duniani iliyo na aina nyingi za wanyamapori na kwamba inawatunza na kuwalinda katika maeneo mbalimbali. Kati ya wanyama hao wengine ni wakali na wana madhara makubwa sana kwa binadamu na mali zao, wengine ni wapole na hawana madhara kwa binadamu. Pengine mara moja moja kwa upande wa uharibifu wa mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapotokea kuwa wanyama wakali hao wanapoleta madhara kwa watu na uharibifu wa mali zao, sisi wawakilishi wa wananchi hao tulimo humu Bungeni hatuwezi kukaa kimya tukiona hali hiyo inaendelea. Ni wajibu wetu kwa mujibu wa Katiba ya nchi hii kuiarifu Serikali ili ichukue hatua za kufaa ili ama kuzuia hali hiyo isitokee ama kuiondoa kabisa ili kuwaepusha wananchi wetu na hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali niliyioieleza hapo juu imekuwa ikitokea mara kwa mara kwa wananchi wa baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Mtwara ambapo wanyama hao wakali kama vile simba, chui, tembo na mamba wamekuwa wakileta madhara makubwa ya vifo na kuacha majonzi kwa jamii, kuuliwa kwa mifugo yao na uharibifu wa mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kutokana na hali hiyo matatizo mengine yanayotokana na hali hiyo ni kwa wananchi kutokwenda kwenye mashamba ya mazao yao kulima, kupalilia ama kuvuna kutokana na kuogopa kuuliwa au kudhuriwa na wanyama hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazo takwimu kidogo za kuthibitisha haya ninayoyasema:-

- (a) Uharibifu wa mifugo katika Wilaya ya Newala. Mwaka 2000, wanyama pori husika ni chui na simba, aina ya mifugo ni ng'ombe, mbuzi na kondoo. Idadi ya mifugo iliyouawa ni 40. Thamani yake ni shilingi 450,000/=.

Mwaka 2001, wanyamapori husika ni chui, aina ya mifugo ni mbuzi. Idadi ya mifugo iliyouawa ni tisa na thamani yake ni shilingi 90,000/=. Mwaka 2002, wanyamapori husika ni chui, aina ya mifugo iliyoharibiwa ni mbuzi, idadi ya mifugo iliyouawa ni nane. Thamani ya mifugo ni shilingi 60,000/=.

Mwaka 2003, wanyamapori husika ni simba na chui, aina ya mifugo ni mbuzi, idadi ya mifugo iliyouawa ni 24. Thamani ya mifugo ni shilingi 240,000/=.

- (b) Watu waliouawa au kujeruhwa na wanyama hao katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita Mkoani Mtwara ni kama ifuatavyo:-

Mwaka 2000/01, watu waliouawa ni 12, waliojeruhwa ni 23. wanyama waliohusika ni mamba, simba, chui na tembo.

Mwaka 2001/02, watu waliouawa ni 13, waliojeruhwa ni 30, wanyama husika ni simba, chui na mamba.

Mwaka 2002/03, watu waliouawa ni 12, waliojeruhwa ni 26, wanyama husika ni simba, mamba, chui na nyati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 21 Juni, 2002, niliuliza swali Bungeni kwamba Serikali ilikuwa haioni umuhimu wa kuwafidia wananchi ambao ndugu zao huuawa na wanyama wakali. Majibu ya Serikali yalikuwa, gharama ya kufanya hivyo ni kubwa sana ambayo Serikali haiwezi kumudu.

Aidha, katika majibu hayo hayo Serikali ilisema kuwa Sheria Na. 12 ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya Mwaka 1974, haizungumzii suala la fidia. Hivyo Serikali haiwajibiki kutoa fidia kwa wananchi wanaoathirika na madhara ya wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua hii naomba niiulize Serikali. Je, wananchi wataendelea kupata madhara haya mpaka lini? Kwa kuwa upo utaratibu wa kuziangalia sheria zetu mara kwa mara ama kwa lengo la kuzifuta zile ambazohaziendi na wakati ama kuzifanya mabadiliko ya hapa na pale ili kukidhi matakwa ya hali halisi.

Je, kwa nini Serikali isiwelete sheria hiyo Bungeni ili iangaliwe upya kwa lengo la kuwafidia waathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa ushauri, kama Katiba ya nchi inavyosema, Serikali iziangalie upya sheria zote zinazohusiana na tatizo hili kwa njia moja ama nydingine ili kuruhusu wananchi waathirika wafidiwe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninashauri Serikali katika kuziangalia sheria hizo itilie maanani ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha kuwa vyanzo vyote viwili vya mapato ya nchi ambavyo ni wananchi na wanyamapori vinakuwa salama na viendelee kuliletea pato Taifa hili. Tofauti na hali ya sasa ambapo wanyamapori wanalindwa zaidi na sheria hiyo ya mwaka 1974 kuliko wananchi amba hawaruhusiwi hata kuwaua wanyama hao wanapofanya uharibifu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maelezo yangu binafsi ili kuitaka Serikali iyafanyie kazi. Aidha, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kunisikiliza na kunivumilia katika muda huu wote amba nimekuwa nikitoa maelezo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imesikia hoja binafsi ya Mheshimiwa Lydia Boma, Mbunge wa Viti Maalum na itayaifanyia kazi na kutoa majibu katika Bunge lijalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofî*)

**MWENYEKIDI:** Waheshimiwa Wabunge kabla hatujiamua hoja hiyo iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri tumepata vikaratasi vingi, vinasema mbona Waziri anaanza *ku-wind up* ndiyo sisi wengine hatuchangii. Ninayo orodha hapa, leo tulikuwa tumepanga watu 19 lakini wamechangia watu saba, kwa hiyo walibaki wapo 12.

Leo tulichukua wale amba hawajawahi kuchangia kabisa, lakini tunao karibu kama sita hivi, jumla watakuwa kumi na nane. Kwa mpango wa dakika kumi kumi hizi, tutaangalia kesho, lakini mnajua kwamba ikifika kwenye saa saba basi tutakuwa tumeshamaliza mijadala na kwa hiyo tutaahirisha kwa ajili ya mtoa hoja baadaye hapo jioni.

Kwa hiyo, nafikiri tutaendelea na majadiliano asubuhi kama kutakuwa na mabadiliko yoyote basi tutawasili ana subuhi.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Saa 12.44 jioni Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa Tarehe 20 Februari, 2004 Saa Tatu Asubuhi*)

